

# Ualimu kwa Vitendo

Kitabu cha Mwallimu Tarajali

**Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali,  
Msingi na Elimu Maalumu**



Taasisi ya Elimu Tanzania





# Ualimu kwa Vitendo

**Kitabu cha Mwalimu Tarajali**

**Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali,  
Msingi na Elimu Maalumu**



Taasisi ya Elimu Tanzania



© Taasisi ya Elimu Tanzania 2024

Toleo la kwanza 2024

ISBN: 978-9912-756-47-2

Taasisi ya Elimu Tanzania

Eneo la Mikocheni

132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi

S.L.P. 35094

14112 Dar es Salaam

Simu: +255735041170/735041168

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri, wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.



CONTENTS	
Orodha ya vielelezo .....	vi
Shukurani .....	vii
Utangulizi.....	viii
<b>Sura ya Kwanza: Mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.....</b>	<b>1</b>
Dhana ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji .....	1
Aina ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji .....	1
Mambo yanayoathiri mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji .....	3
Umuhimu wa kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji .....	4
Kanuni za kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.....	5
Kuandaa na kutumia mazingira katika ufundishaji na ujifunzaji.....	7
Zoezi la marudio .....	9
<b>Sura ya Pili: Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji .....</b>	<b>10</b>
Dhana ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji .....	10
Uchambuzi wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji.....	11
Zoezi la marudio .....	42
<b>Sura ya Tatu: Zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia .....</b>	<b>43</b>
Zana na vifaa vya ujifunzaji.....	43
Utengenezaji wa zana za kufundishia na kujifunzia .....	44
Uhifadhi wa zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.....	45
Uandaaji wa kivunge cha zana .....	47
Zoezi la marudio .....	49
<b>Sura ya Nne: Darasa salama, changamshi na jumuishi .....</b>	<b>50</b>
Dhana ya darasa salama .....	50
Darasa changamshi .....	53
Darasa jumuishi .....	56





Upangaji wa darasa kwa kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi .....	59
Upangaji wa zana za kufundishia na kujifunzia .....	62
Kona za ujifunzaji .....	64
Zoezi la marudio .....	66
<b>Sura ya Tano: Usimamizi wa darasa wakati ufundishaji na ujifunzaji....</b>	<b>67</b>
Dhana ya usimamizi wa darasa.....	67
Kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa.....	70
Mbinu na zana shirkishi, jumuishi na changamshi .....	71
Zoezi la marudio .....	72
<b>Sura ya Sita: Teknolojia na vifaa saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji .....</b>	<b>73</b>
Teknolojia na vifaa saidizi .....	73
Sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji.....	74
Ufundishaji na ujifunzaji katika darasa kubwa na jumuishi .....	75
Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji .....	76
Zoezi la marudio .....	78
<b>Sura ya Saba: Ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa.....</b>	<b>79</b>
Dhana ya ujifunzaji nje ya darasa .....	79
Mambo ya kuzingatia wakati wa kupanga shughuli nje ya darasa .....	80
Tathmini ya ujifunzaji nje ya darasa .....	83
Zoezi la marudio .....	86
<b>Sura ya Nane: Upimaji, tathmini na utoaji mrejesho wa ufundishaji na ujifunzaji .....</b>	<b>87</b>
Kutumia mbinu na zana za upimaji katika ufundishaji na ujifunzaji.....	87
Ufuatalilaji wa maendeleo ya ujifunzaji .....	89
Kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi.....	90



Kutumia taarifa za matokeo ya upimaji katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji .....	93
Kuboresha utendaji wa mwanafunzi.....	93
Kuboresha utendaji wa mwalimu.....	94
Zoezi la marudio .....	96
<b>Sura ya Tisa: Ushauri na unasihi katika ufundishaji na ujifunzaji .....</b>	<b>97</b>
Kubaini wanafunzi wenyе mahitaji ya ushauri na unasihi.....	97
Mambo yanayohitaji ushauri na unasihi kwa wanafunzi.....	100
Kutoa huduma ya ushauri na unasihi kwa mwanafunzi.....	102
Utoaji wa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wa elimu ya awali .....	103
Utoaji wa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wa elimu maalumu.....	104
Utoaji wa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wa elimu ya msingi.....	104
Zoezi la marudio .....	106
<b>Faharasa.....</b>	<b>107</b>
<b>Bibliografia .....</b>	<b>109</b>

**Orodha ya Vielelezo**

Kielelezo 2.1: Ujifunzaji kwa kutumia mchezo wa kadi za namba.....	12
Kielelezo 2.2: Mgeni mwalikwa akifundisha magonjwa ya kuambukiza binadamu .....	14
Kielelezo 2.3: Majadiliano katika vikundi.....	21
Kielelezo 3.1: Kivunge cha zana .....	48
Kielelezo 4.1: Usfundishaji na ujifunzaji katika darasa salama .....	51
Kielelezo 4.2: Mfano wa darasa jumuishi .....	56
Kielelezo 4.3: Mpangilio wa darasa jumuishi .....	60
Kielelezo 4.4: Baadhi ya kona za ujifunzaji .....	65
Kielelezo 7.1: Baadhi ya shughuli za ujifunzaji nje ya darasa .....	82
Kielelezo 9.1: Ushauri <del>ha</del> unasihi .....	103



### Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi zilizoshiriki kufanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwalimu tarajali. Kipekee, TET inatoa shukurani kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, vyuo vya ualimu Tukuyu, Bustani, na Kinampanda.

Pia, TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:

**Waandishi:** Bw. Gwido M. Kalobona, Bw. Frank X. Mbunda, Bw. Dickson D. Msangi, Bw. Christopher A. Matheo na Bi. Chonge Z. Tukwa

**Wahariri:** Dkt. Wadrine Maro, Dkt. Ibrahim Nzima na Bi. Angelista Joseph

**Msanifu:** Bi. Eva G. Kwai

**Mehoraji:** Bw. Godwin J. Chipanya

**Mratibu:** Bw. Gwido M. Kalobona

Vilevile, TET inatoa shukurani za kipekee kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha zilizofanikisha kazi ya uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

Taasisi ya Elimu Tanzania

**Utangulizi**

Kitabu cha Ualimu kwa Vitendo kimetayarishwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali, Msingi na Maalumu iliyotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia mwaka 2023.

Kitabu hiki kina sura tisa ambazo ni: Mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji; Mbinu za kufundishia na kujifunzia; Zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia; Darasa salama, changamshi na jumuishi; Usimamizi wa darasa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji; Teknolojia na vifaa saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji; Ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa; Upimaji, tathmini na utoaji wa mrejesho; na Ushauri na unasihi katika ufundishaji na ujifunzaji.

Maudhui ya kitabu hiki yamewasilishwa kwa njia ya matini, kazi za kufanya, michoro na picha mbalimbali ili kukuwezesha kujenga umahiri uliokusudiwa katika kila sura. Kila sura ina mazoezi ya kutosha yatakayokuwezesha kupima uelewa wako kuhusu maudhui husika. Hivyo, unapaswa kufanya kazi zote na mazoezi yote yaliyopo katika kitabu hiki pamoja na kazi zingine utakazopewa na mkunfunzi ili kujenga umahiri uliokusudiwa.

Kitabu hiki kimeandaliwa kwa ajili ya mwalimu tarajali kukuza ujuzi wake kwa kufanya shughuli mbalimbali zilizopendekezwa na siyo kujifunza kwa kukariri. Mwalimu tarajali unapaswa kuelewa kwamba, kitabu hiki pekee hakiwezi kujitosheleza kukujengea umahiri bali unapaswa kusoma vyando vingine vya taarifa mtandaoni na maktaba kama vile magazeti, majarida, makala na vitabu vya ziada. Kwa kufanya hivyo, utaweza kupanua kiwango chako cha maarifa na uelewa katika eneo lako la kitaaluma.

Kwa matumizi endelevu ya kitabu hiki, unapaswa kukihifadhi vizuri na kukitumia wakati uwapo chuoni na kipindi cha likizo.

Jifunze zaidi kupitia Maktaba Mtandao: <https://ol.tie.go.tz>.



Taasisi ya Elimu Tanzania





## Sura ya Kwanza

# Mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji

### Utangulizi

Mazingira katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji yanazingatia msingi wa ushirikiano wa karibu kati ya mwalimu na mwanafunzi. Mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanajumuisha mazingira halisi, ya kisaikolojia, mahitaji ya mwanafunzi kitaaluma, kihisia, kijamii na hali ya umiliki wa ujifunzaji. Katika sura hii, utajifunza dhana ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, mambo yanayoathiri mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji na kanuni za kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Vile vile, utajifunza kuandaa na kutumia mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuchagua, kupanga na kutumia mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya awali, msingi na elimu maalumu.



Fikiri

Maandalizi ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji

### Dhana ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji

Mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanajumuisha mazingira halisi, kijamii, kiutamaduni na kihisia yanayoweza kuathiri ufundishaji na ujifunzaji. Mazingira haya yanajumuisha mpangilio wa darasa, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia, mbinu na mikakati ya kufundisha inayotumiwa na mwalimu, pamoja na hali ya jumla ya darasa inayowezesha mchakato wa ujifunzaji. Vile vile, Mazingira ya ujifunzaji yanahusiana na namna mwanafunzi anavyojifunza, ikiwa ni pamoja na ari ya kujifunza, uhusiano baina ya wanafunzi, mwalimu, wazazi, walezi na wadau wengine katika jamii.

### Aina ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji

Mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanaweza kugawanya katika aina mbalimbali kama ifuatavyo:

**Mazingira halisi:** Yanajumuisha miundombinu ya shule kama vile majengo ya madarasa, maktaba, maabara, na maeneo ya michezo. Miundombinu yenye





hali nzuri na salama huwezesha wanafunzi kujifunza kwa usalama na hivyo kuboresha uzoefu wa ujifunzaji wao. Vile vile, mpangilio wa darasa, ikiwemo madawati, viti, meza na vifaa vya kufundishia unaweza kuimarisha ushiriki na nidhamu ya wanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

**Mazingira yasiyo halisi/ ya uigizaji:** Mazingira ya mtandaoni yaliyoundwa ili kuiga mazingira yanayofanana na halisi katika shughuli za kujifunza. Mazingira haya yanamwezesha mwanafunzi kutumia maarifa na ujuzi wao katika miktadha inayoakisi mazoezi yao ya kitaaluma. Uigaji unaweza kutoa nafasi ya kujifunza katika mazingira salama ambapo wanafunzi wanaweza kujaribu mbini mbalimbali na kujifunza kutokana na makosa yao huku wakipata fursa ya kupata ujuzi muhimu na kujenga kujiamini.

**Mazingira ya kijamili na utamaduni:** Hali ya kijamili ya wanafunzi, kama vile familia zao na hali ya kiuchumi, inaathiri mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Jamii na familia zinaweza kuchangia rasilimali ili kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Mawazo na mitazamo ya kitamaduni kuhusu elimu yanaweza kuathiri ufundishaji na ujifunzaji. Katika jamii zinazohamahama ufundishaji na ujifunzaji unaweza kuhusisha mfumo wa darasa linalotembea ili kuweza kuwafikia wanafunzi walipo au kujenga miundombinu ya mabweni ili kuwawezesha wanafunzi kushiriki katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

**Mazingira ya kibinasi:** Mahitaji maalumu ya wanafunzi, ikiwa ni pamoja na wale wenye ulemavu au changamoto za ujifunzaji, yanapaswa kupewa kipaumbele ili kuimarisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mazingira yanayozingatia mahitaji haya yanawezesha wanafunzi kufikia malengo yao ya kitaaluma, kihisia na kijamii. Aidha, ujuzi, mafunzo, mtazamo na mitindo ya walimu kuhusu ufundishaji ni muhimu katika kuhamasisha mazingira ya ujifunzaji.



### Kazi ya kufanya 1.1

1. Tembelea shule ya msingi iliyo karibu na chuo chako na fanya uchunguzi wa kina kuhusu aina za mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Andaa taarifa ya uchunguzi wako kisha, weka kwenye mkoba wako wa kazi.
2. Kwa kutumia maktaba ya chuoni kwako na vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni baini namna mazingira ya kisaikolojia na kijamii yanavyoathiri ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya awali, msingi na elimu maalumu.





Zoezi la 1.1

1. Eleza umuhimu wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya awali, msingi na elimu maalumu.
2. Fafanua namna unavyoweza kutumia teknolojia ili kuwezesha ujifunzaji kwa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi na elimu maalumu.
3. Bainisha namna mazingira yanavyoweza kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

### Mambo yanayoathiri mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji

Baadhi ya mambo yanayoweza kuathiri mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ni pamoja na:

**Vifaa vya kufundishia:** Upatikanaji na hali ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vitabu vya kiada na ziada, kompyuta, na vifaa vya maabara vinachangia moja kwa moja katika ubora wa ujifunzaji. Kwa mfano, darasa lenye kompyuta za kisasa linaweza kuunganisha wanafunzi kwenye shughuli za mtandaoni ambazo zinaongeza uelewa wao. Vifaa saidizi, kama vile vifaa vya kusikia kwa wanafunzi wenye changamoto ya kusikia, vinaweza kuboresha uwezo wa kushiriki katika ujifunzaji.

**Miundombinu na mpangilio wa darasa:** Mpangilio wa madawati au meza katika maeneo ya kujifunzia unaathiri ushiriki wa wanafunzi. Kwa mfano, madawati au meza yaliyopangwa kwa duara yanaweza kuchochea mijadala na ushirikiano, wakati madawati yaliyopangwa kwa safu yanaweza kuimarisha umakini wa mwanafunzi mmoja mmoja. Miundombinu kama taa na hali ya hewa ni muhimu; darasa lenye mwanga wa kutosha na hali nzuri ya hewa linaweza kusaidia wanafunzi katika ujifunzaji.

**Mehango wa walimu:** Stadi za ufundishaji, mtazamo, na maarifa ya walimu pamoja na mbinu wanazotumia zinaathiri moja kwa moja mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Walimu wenye stadi za kutumia mbinu za kufundishia wanaweza kuimarisha ujifunzaji kushirikisha wanafunzi katika mchakato ufundishaji na ujifunzaji.

**Nafasi ya mwanafunzi:** Hii inahusisha utayari, ari na mahitaji yao ya ujifunzaji: utayari na motisha wa mwanafunzi vinachangia uwezo wa mwanafunzi kupata maarifa na stadi mpya na kuzichakata kwa njia ambayo hubadilisha tabia au kuleta matokeo chanya yanayotarajiwa ya kitaaluma. Kimsingi, huu ni uwezo binafsi wa kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kujifunza. Motisha huchochea





tabia na utendaji wa mwanafunzi. Wanafunzi wanapohamasishwa watakuwa chanya na wenyewe nguvu zaidi darasani na kuelekea kujifunza kwao. Wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu, kama vile ugumu wa kujifunza, wanaweza kuhitaji matumizi ya mbinu maalumu. Mbinu hizo zinajumuisha mipango ya masomo inayowasilishwa kwa njia ya picha na maandiko.

**Mchango wa wazazi na jamii:** Ushirikiano wa wazazi na jamii katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unaweza kuboresha ujifunzaji shulenii. Kwa mfano, wazazi wanafuatilia maendeleo ya watoto wao shulenii wanaongeza uelewa na ufaulu wa watoto wao. Vilevile, wazazi na wadau wengine katika jamii wanaweza kutoa vifaa kama vile vitabu vyatia, vifaa vyatia maabara, na zana nyingine za kufundishia na kujifunzia.

**Hali ya kijamii na utamaduni:** Hali ya kijamii na kiuchumi ya wanafunzi inaweza kuathiri mazingira ya ujifunzaji. Wanafunzi kutoka familia zenye hali duni wanaweza kupata changamoto ya upatikanaji wa vifaa vyatia kujifunzia jambo linaloweza kuathiri ujifunzaji wao. Shule zinazowapa wanafunzi chakula na vifaa muhimu vyatia kujifunzia zinaweza kusaidia kupunguza tofauti hizi na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

#### **Umuhimu wa kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji**

Kuandaa mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji ni muhimu kwa sababu hutoa fursa sawa ya ujifunzaji kwa wanafunzi wote. Mazingira bora ya ujifunzaji huwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao bila kujali tofauti zao za kijamii na kiuchumi. Aidha, mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji husaidia katika kuboresha afya ya kimwili na kiakili ya wanafunzi. Mazingira yanayozingatia usafi, mwanga, na hali ya hewa inayofaa yanawczesha wanafunzi kujifunza kwa ufanisi.

Mazingira yanayozingatia mahitaji ya kisaikolojia ya wanafunzi huongeza kujiamini na kupunguza msongo wa mawazo. Wanafunzi wanapokuwa katika mazingira huru, wanakuwa na hali ya ujasiri kutoa maoni kwa kujiamini. Msaada wa kisaikolojia kwa wanafunzi, unachangia kujenga hali nzuri ya kiakili kwa wanafunzi na kuwasanya wajiamini katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Mazingira bora yanachangia katika kuendeleza ujuzi wa kijamii na maadili kwa wanafunzi. Wanafunzi wanaposhirikiana katika kazi za vikundi au shughuli za michezo, wanajifunza kuhusu ushirikiano, uvumilivu, na kuheshimiana, stadi ambazo ni muhimu kwa maisha yao ya baadaye. Walimu wanapaswa kuandaa mazingira ya ujifunzaji yanayoruhusu shughuli za kijamii kama michezo na sanaa. Mazingira haya husaidia kuimarisha uhusiano baina ya wanafunzi.



za kufundisha zinazochanganya maandiko na michoro kwa wanafunzi wenye changamoto za ujifunzaji kulingana na mahitaji yao.

**Upatikanaji wa rasilimali:** Kuandaa mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji kunahitaji uwepo wa rasilimali za kutosha kama vile vifaa vya teknolojia, vitabu, maabara, maeneo ya michezo na vifaa vyake. Shule inayotoa vitabu vya kiada kwa wanafunzi wote bila ubaguzi inawapa wanafunzi fursa sawa ya kujifunza. Maabara zilizo na vifaa vya kutosheleza huwapa wanafunzi fursa ya kujifunza kwa vitendo na majoribio. Uwepo wa maeneo ya michezo na vifaa vyake huchangia katika kujenga afya ya wanafunzi kwa njia ya michezo.

**Kuboresha mpangilio wa darasa:** Mpangilio wa madawati, viti, meza na vifaa vya kufundishia unapaswa kuimarisha ushirikiano na mawasiliano baina ya wanafunzi na mwalmu. Kupanga madawati kwa mtindo wa duara au vikundi kunaweza kurahisisha mijadala na kazi za pamoja, na kuchangia katika ujifunzaji.

**Matumizi ya teknolojia:** Teknolojia inapaswa kutumika kikamilifu katika mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Kompyuta, ubao wa kielektroniki, na programu wezeshi za kielimu vinaweza kuboresha ufundishaji na kurahisisha ujifunzaji. Shule inayotumia programu za kielimu na mawasiliano kama vile darasa mtandaoni, hasa katika mazingira ya ujifunzaji wa mbali, inawapa wanafunzi fursa ya kujifunza popote walipo, hivyo kuendelea na masomo bila usumbu.

**Uhamasishaji wa ushiriki:** Mazingira ya darasa yanapaswa kuchoechea ushiriki wa wanafunzi katika ujifunzaji. Walimu wanapaswa kutumia mbinu za ufundishaji zinazowapa wanafunzi fursa ya kujieleza, kuuliza maswali, kuibua hoja na kushirikiana katika kutatua matatizo. Mwalimu anaweza kutumia majadiliano, ambapo wanafunzi wanajadili mada fulani na kisha kutoa mrejesho kwa darasa zima. Matumizi ya maswali ya kuchoechea fikra tunduizi au majoribio ya vitendo kama vile maonyesho ya maabara yanaweza kuhamasisha wanafunzi kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji.

**Kujali afya ya kisaikolojia:** Mazingira ya kujifunzia yanapaswa kuzingatia afya ya kiakili na kisaikolojia ya wanafunzi. Hii inajumuisha kuunda mazingira yenye mawasiliano chanya, kutoa msaada wa kisaikolojia inapohitajika, na kuondoa vitendo vya unyanyasaji au ubaguzi. Shule ikiwa na kitengo cha ushauri na unasihi inaweza kuwasaidia wanafunzi kisaikolojia. Mazingira yenye walimu wanaowahimiza na kuwapongeza wanafunzi kwa juhudini zao huchangia katika kuimarisha hali ya kujiamini na kujituma.



**Ufutiliaji na tathmini:** Ni muhimu kwa walimu na viongozi wa shule kufutilia na kutathmini mara kwa mara hali ya mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Ufutiliaji huu unasaidia kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa na kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kuwa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanakuwa na ufanisi. Shule inayofanya tathmini ya mara kwa mara ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia, hali ya miundombinu na hali ya ujifunzaji inaweza kugundua hitilafu na kuchukua hatua za kurekebisha hali hiyo.



### Kazi ya kufanya 1.3

Wakati wa mafunzo ya ualimu kwa vitendo umepewa jukumu la kuchunguza namna walimu wanavyozingatia kanuni na taratibu za mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Andika taarifa na weka kwenye mkoba wako wa kazi.



### Zoezi la 1.3

1. Tathmini namna utamaduni wa shule unavyoweza kujenga mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi na elimu maalumu.
2. Pendekeza mikakati inayoweza kuchukuliwa ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.
3. Kwa kutumia mifano fafanua namna maboresho ya miundombinu yanavyoweza kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji.

### Kuandaa na kutumia mazingira katika ufundishaji na ujifunzaji

Kuandaa na kutumia mazingira ni mchakato muhimu unaoathiri moja kwa moja ubora wa ufundishaji na ujifunzaji. Mazingira haya yanaweza kuwa halisi, ya kijamii, kitaaluma, au kifedha, ambapo kila moja lina nafasi muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Wakati wa kuandaa na kutumia mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo:

**Usalama wa wanafunzi:** Mazingira ya kufundishia yanapaswa kuwa salama kwa wanafunzi wote. Hii inajumuisha kuhakikisha kuwa miundombinu ya shule.



kama vile madarasa, maeneo ya michezo, na vyoo, ni salama na inakidhi viwango vinavyostahili. Mfano, madarasa yanapaswa kuwa na milango na madirisha yanayoweza kutumika wakati wa dharura. Vile vile, vifaa vya kuzimia moto na kutolea huduma ya kwanza vinapaswa kupatikana kwa urahisi.

**Uwepo wa vifaa vya kutosha:** Vifaa vya kufundishia kama vitabu, vifaa vya maabara, kompyuta, na teknolojia nyingine zinapaswa kupatikana kwa walimu na wanafunzi. Vifaa hivi vinapaswa kuwa katika hali nzuri na vinavyokidhi mahitaji ya wanafunzi wote, ikiwemo wale wenye mahitaji maalumu.

**Ujumuishaji wa wanafunzi:** Wakati wa kuandaa na kutumia mazingira ya kufundishia, ni muhimu kuzingatia mahitaji ya wanafunzi wote wakiwemo wenye ulemavu au changamoto za kujifunza. Hii inajumuisha vifaa maalumu vya kujifunzia na mbinu za ufundishaji zinazowezesha wanafunzi kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji. Mfano, kuweka vibao vya maelekezo vinavyoweza kuguswa au kutumia lugha ya ishara kwa wanafunzi wenye changamoto ya usiku.

**Tofauti za kiutamaduni na kijamii:** Ni muhimu kuzingatia tofauti za kitamaduni na kijamii za wanafunzi wakati wa **kuandaa** na kutumia mazingira ya kujifunzia. Mazingira yanapaswa kuakisi na kuheshimu tamaduni mbalimbali za wanafunzi ili kuawezesha kujifunza kwa ufanisi zaidi. Kwa mfano, kutumia mifano ya kitamaduni katika masomo au kuzingatia sherehe za kitamaduni wakati wa kupanga ratiba ya masomo.



#### Kazi ya kufanya 1.4

1. Kwa kutumia vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni andaa wasilisho kuhusu namna ya kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa elimu ya awali, msingi na elimu maalumu. Fanya wasilisho hili kwa wanachuo wenzako chini ya uangalizi wa mkufunzi.
2. Wakati wa mafunzo kwa vitendo umepangiwa kufundisha darasa la sita somo la Historia ya Tanzania na maadili. Tathmini hali ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji shulenii, kisha andika taarifa na weka kwenye mkoba wako wa kazi.



## Zoezi la 1.4

1. Eleza namna usalama na ustawi ni kanuni muhimu katika kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.
2. Fafanua namna teknolojia inavyoweza kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu.
3. Bainisha namna uhamasishaji wa ushiriki wa wanafunzi katika elimu ya awali, msingi na elimu maalumu unavyoweza kuimarisha ujifunzaji kwa vitendo.

## Zoezi la marudio

1. Fafanua namna utakavyoweza kuboresha maandalizi yako ya ufundishaji kwa kuzingatia mahitaji ya ujifunzaji katika darasa la elimu ya msingi.
2. Kwa kutumia mifano fafanua namna mazingira halisi, ya kijamii, kitaaluma, na kifedha yanavyoathiri ufundishaji na ujifunzaji.
3. Eleza umuhimu wa kanuni za kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji zinavyoweza kuboresha mazingira ya kujifunzia.
4. Ainisha faida na changamoto za matumizi ya teknolojia katika mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.
5. Eleza kwa mifano mikakati inayoweza kuchukuliwa ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.
6. Fafanua umuhimu wa usuutiliaji wa mara kwa mara wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia.
7. Tathmini umuhimu wa rasilimali katika mazingira ya kufundishia na kujifunzia.
8. Eleza namna ambavyo kujali afya ya kisaikolojia ya wanafunzi kunaweza kuboresha ufanisi wa ujifunzaji.





Sura ya  
Pili

## Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji

### Utanugulizi

Ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji unaweza kufikiwa na kuwa shirikishi kwa kuchagua na kutumia mbinu mbalimbali za kuwezesha ujifunzaji wa mwanafunzi. Katika sura hii, utachambua mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia maana, umuhimu, hatua na mambo ya kuzingatia. Aidha, utajifunza kubaini faida na changamoto za matumizi ya mbinu hizo na namna ya kuzitanua katika muktagha wa ufundishaji na ujifunzaji. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuaridhia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji ili kujenga umahiri uliokusudiwa kwa elimu ya awali, msingi na elimu maalumu.



Fikri

Ufundishaji na ujifunzaji bila kutumia mbinu sahihi

### Dhana ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni jumla ya vilendo vinavyobuniwa na mwalimu ili kutendwa na mtoto au mwanafunzi darasani au nje ya darasa kwa lengo la kukuza maarifa, stadi na mwelekeo. Mbinu bora na anuai ni zile zinazomwesha mtoto au mwanafunzi kujifunza kwa ufanisi, hivyo kupelekea kufikiwa kwa malengo ya mtaala katika ngazi husika ya elimu. Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazosisitiza kutumika ni zile zinazomfanya mtoto au mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji ikiwa pamoja na kumwezesha kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyando rasmi mbalimbali. Kwa kuzingatia mtaala wa ujenzi wa umahiri, ni muhimu kutumia mbinu zinazolenga kujenga maarifa, stadi na mwelekeo hasa katika kukuza Stadi za Karne ya 21. Stadi hizi zinajumuisha uwezo wa kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo. Mbinu anuai na mahususi zinawenza kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya awali, msingi na elimu maalumu ili



kumwezesha kujenga umahiri uliokusudiwa. Baadhi ya mbinu hizo ni pamoja na onesho mbinu, kualika mgeni, ujifunzaji kwa vitendo, majoribio, bungua bongo, majadiliano ya vikundi, mazoezi na marudio, ugunduzi, michezo, nyimbo, hadithi, igizo dhima na kisa mafunzo. Aidha, mbinu nyingine ni matembezi ya galari, ziara za mafunzo, changanya kete, fikiri-jozisha-shirikisha, uchunguzi, mashairi ya watoto, ngonjera, maswali na majibu na kazimradi.



#### Kazi ya kufanya 2.1

Soma maandiko mbalimbali katika maktaba ya chuo au vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni, chambua dhana ya mwanafunzi kama kitovu cha ujifunzaji inavyozingatiwa wakati wa kuchagua mbinu za kufundishia .

#### **Uchambuzi wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji**

Unyumbu na ubunifu wa mwalimu ni muhimu katika kuchagua mbinu zinazoendana na shughuli mahusi za ujifunzaji, mazingira halisi ya darasa na mahitaji ya kila mtoto au mwanafunzi, upatikanaji wa vifaa na hali halisi ya darasa. Ufutao ni ufanuzi wa baadhi ya mbinu mahususi za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia maana, umuhimu, matumizi, hatua, changamoto na namna ya kukabiliana na changamoto hizo katika ufundishaji na ujifunzaji:

#### **Ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia michezo**

Michezo ni mbinu inayotumika katika ujifunzaji na ufundishaji kwa kuhusisha mijongeo ya mwili, matumizi ya misuli midogo na mikubwa na unyumbu wa mwili na akili au fahamu. Michezo humsaidia mtoto au mwanafunzi kutumia zaidi ya mlango mmoja wa fahamu na inawezesha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa. Vilevile, michezo huburudisha, inakuza ushirikiano, huchochea ubunifu, kufikiriki kimantiki na kurahisisha ujifunzaji na ufundishaji. Michezo huimarisha kumbukumbu, husaidia kuibua na kuendeleza vipaji, hujenga mahusiano na kuwa na stadi za kutatua migogoro, kujimiani na ustahimilivu.



### Matumizi ya mbinu ya ujifunzaji kwa michezo

Katika shughuli za ujifunzaji na ufundishaji, michezo hutumika kwa kuzingatia umahiri mahususi unaokusudiwa kujengwa, miundombinu iliyopo, mahitaji ya kila mtoto, mazingira, hali ya hewa, upatikanaji wa visaa na usalama katika eneo husika la ujifunzaji. Eneo la kufanya michezo linaweza kuandaliwa ndani au nje ya darasa kwa kuzingatia upatikanaji wa nafasi ya kutosha na shughuli husika kwa watoto/wanafunzi wote kushiriki.

Hivyo, matumizi ya mbinu ya michezo yanawezesha shughuli iliokusudiwa kufikiwa kikamilifu. Kwa mfano mwalimu anaweza kutumia michezo wa kadi za namba kama mbinu ya kujenga stadi za kuhesabu au dhana ya namba ili kukuza stadi ya fikra tunduizi na kutatua changamoto. Kielelezo 2.1 kinaonesha ujifunzaji kwa kutumia michezo wa kadi za namba.



**Kielelezo 2. 1: Ujifunzaji kwa kutumia michezo wa kadi za namba**

### Hatua za kufuata

Mwalimu anapotaka kutumia mbinu ya michezo ni vyema kufuata hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- (a) Kutambulisha michezo husika;



- (b) Kuainisha vifaa vitakavyotumika kwenye mchezo;
- (c) Kubainisha kanuni na taratibu za mchezo ;
- (d) Kuonesha namna mchezo unavyochezwa;
- (e) Kusimamia na kufuutilia kila hata ya mchezo ili kuhamasisha, kuboresha na kuelekeza na kuhakikisha unafanyika kama ilivyopangwa;
- (f) Kupima na kutathmini umahiri uliojengwa kuititia mchezo; na
- (g) Kutoa mrejesho na maboresho kwa watoto kuhusu mchezo uliochezwa.

#### **Changamoto ya kutumia mbinu ya michezo**

Matumizi ya mbinu ya ujifunzaji na ufundishaji kwa michezo yanaweza yakakuzwa na uchaguzi wa mchezo unaoendana na muda wa vipindi uliopangwa pamoja na upatikanaji wa baadhi ya vifaa vya kutosha ambavyo vinaweza kuwa changamoto kutokana na mazingira na shughuli ilokusudiwa kufanyika.



#### Kazi ya kufanya 2.2

Angalia video mbalimbali kutoka katika vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni zinazoonesha namna michezo inavyoweza kutumika kujenga umahiri katika muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji. Andika dondoo na hifadhi katika mkoba wako wa kazi.



#### Zoezi la 2.1


1. Chagua michezo mitatu unayoifahamu, kisha eleza namna itakavyotumika katika ujifunzaji na ufundishaji katika darasa la awali, msingi na elimu maalumu.
2. Bainisha changamoto ya muda wa vipindi, ukosefu wa vifaa na idadi ya wanafunzi darasani katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia michezo katika elimu ya awali, msingi na elimu maalumu.





### Mbinu ya kualika mgeni

Mbinu hii huhusisha kualika mgeni mwenye utaalamu na ujuzi kuhusu mada au hoja inayofundishwa. Mwalimu anapotaka kutumia mbinu hii ni vyema aombe kibali cha kumwalika mgeni kwa mamlaka husika pale inapobidi na ampatie taarifa mgeni anayekusudia kumwalika na kumjulisha juu ya shughuli anayokuja kutolea usafanuzi ili kumpatia nafasi ya kuijandaa. Kisha, mwalimu afanye tathmini ya mahitaji ya kuwecesha ufanisi wa mafunzo hayo, yakiwemo mahitaji ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu. Mgeni anapaswa kupewa taarifa mapema ili aweze kuijandaa kikamilifu. Kielelezo 2.2 kinaonesha mgeni mwalikwa akitoa mada kuhusu magonjwa ya kuambukiza binadamu.



**Kielelezo 2.2:** Mgeni mwalikwa akifundisha magonjwa ya kuambukiza binadamu

### Faida ya mbinu ya kualika mgeni

Kualika mgeni darasani ni mbinu yenye ufanisi wa kuongeza uelewa na hamasa kwa wanafunzi. Zipo baadhi ya faida zitokanazo na mbinu hii:

- Mgeni huweza kufafanua kwa kina masuala ambayo hayapo vitabuni;
- Wanafunzi hujifunza kwa furaha na kwa uhuru zaidi kuliko wakiwa na mwalimu wao; na
- Hujenga tabia ya usikivu kwa wanafunzi.



### *Changamoto za mbinu ya kualika mgeni*

Ingawa mbinu ya kualika mgeni ina faida nyingi, pia ina baadhi ya mapungufu ambayo yanapaswa kuzingatiwa:

- Wanafunzi wa umri mdogo au madarasa ya chini wanaweza kushindwa kuchukua nukuu za mada inayotolewa;
- Ushirikishwaji wa wanafunzi unaweza kuwa mdogo sana hasa iwapo mgeni hana ujuzi wa mbinu bora za mawasiliano;
- Mada au hoja inaweza kuwasilishwa kwa muda mrefu ikiwa mgeni atatoa maelezo na ufanuzi wa kina; na
- Wanafunzi wanaweza kupuuza kinachofundishwa ikiwa mada inayotolewa na namna inavyowasilishwa haina mantiki au mtiririko unofaa.



#### Kazi ya kufanya 2.3

Soma machapisho mbalimbali yanayohusu matumizi ya mbinu ya kualika mgeni katika ufundishaji na ujifunzaji. Andika nukuu na ziweke katika mkoba wa kazi.



#### Zoezi la 2.2

- Eleza namna ya kuboresha matumizi ya mbinu ya kualika mgeni.
- Bainisha namna unavyoweza kupanga na kuratibu matumizi ya mbinu ya kualika mgeni katika ufundishaji na ujifunzaji.

### **Mbinu ya oneshombinu**

Katika mbinu hii, mwalimu na wanafunzi hutumia vitendo kuonesha jinsi ya kufanya jambo fulani. Kwanza, mwalimu huanza kwa kuonesha hatua za utekelezaji. Pili, mwalimu na wanafunzi hufanya vitendo pamoja. Hatimaye, wanafunzi hurudia vitendo hivyo wenye. Mbinu hii inajumuisha maelezo ya ana kwa ana pamoja na matumizi ya zana, na maswali na majibu yanayomwezesha mwanafunzi kujifunza stadi mpya. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwaelekeza wanafunzi kwa vitendo kuhusu tabia za tindikali na nyongo hatua kwa hatua.



Kisha, mwalimu na wanafunzi watafanya vitendo pamoja na hatimaye mwalimu atawataka wanafunzi kuonesha jinsi ya kufanya jaribio linalohusu tabia za tindikali na nyongo kwa kufuata hatua alizozionyesha.

#### *Faida za mbinu ya oneshombinu*

Oneshombinu ni mbinu ya uwasilishaji inayofanywa kwa vitendo kuhusu dhana au shughuli ya ujifunzaji. Baadhi ya faida zake ni:

- Kusaidia kuelezea dhana, kanuni na misingi ambayo ingekuwa vigumu kwa wanafunzi kuelewa kwa kutumia maelezo pekee;
- Kusaidia kujenga tabia ya usikivu kwa wanafunzi-wanaoangalia na kuiga kinachotendeka;
- Kuwezesha wanafunzi kutumia milango yote ya fahamu kama vile kuona, kusikia, kugusa, hivyo kuelewa haraka na kuimarisha kukumbuka ya kudumu; na
- Kutoa fursa kwa wanafunzi kuona mfanano kabla ya wao kutakiwa kutenda.

#### *Changamoto za mbinu ya oneshombinu*

Pamoja na kuwa oneshombinu inaleta ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji, lakini ina baadhi ya changamoto ambazo zinahitaji kuzingatiwa. Baadhi ya changamoto hizo ni:

- Wakati mwingine kuhitaji muda mwangi kufanya maandalizi; na
- Sio mbinu bora ikiwa kuna idadi kubwa ya wanafunzi;



#### Kazi ya kufanya 2.4

Tazama video ya kielimu kutoka katika vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni inayomwonesha mwalimu akiwaongoza wanafunzi namna ya kufanya jaribio, kisha chambua kwa makini ili kuona namna mwalimu alivyotumia mbinu hii. Zingatia mambo yafuatayo:

- Maarifa, stadi na mwelekeo ulinaokusudiwa kuendelezwa;
- Ufasaha wa lugha;
- Matumizi ya vifaa na zana za kuwezesha ujifunzaji;





- (d) Ushirikishwaji wa wanafunzi;
- (e) Mtiririko wa shughuli za ujifunzaji; na
- (f) Matumizi ya motisha katika ujifunzaji.



Eleza na andaa mkakati wa kutumia oneshombini katika ufundishaji wa darasa kubwa. Weka kazi yako kwenye mkoba wa kazi kwa matumizi ya baadaye.

#### ***Mbinu ya maswali na majibu***

Mbinu ya maswali na majibu inahusu kufundisha somo kwa mahojiano. Katika mbinu hii, mwalimu huweza kuwa uliza wanafunzi maswali mbalimbali na wanafunzi wanawenza kumuuliza mwalimu au wanafunzi kuulizana maswali wao kwa wao. Mwalimu ahakikishe wanafunzi wengi wanashiriki kujibu maswali.

#### ***Faida ya mbinu ya maswali na majibu***

Mbinu ya maswali na majibu inaruhusu mwalimu na mwanafunzi kufanya mahojiano ya moja kwa moja kwa kuuliza maswali ya uchochezi wa dhana. Faida za kutumia mbinu hii ni:

- (a) Kuchochea wanafunzi kufuata somo kwa makini;
- (b) Wanafunzi hupata fursa ya kushiriki katika harakati za kujifunza;
- (c) Mwalimu hupata nafasi ya kupima ni kwa kiasi gani wanafunzi wanaelewa somo kutohana na majibu yao;
- (d) Husaidia kufikirisha wanafunzi na kujenga uelewa wa kina;
- (e) Mwalimu kubaini changamoto alizonazo kuitia maswali yake na ya wanafunzi;
- (f) Husaidia kuboresha na kurekebisha makosa;
- (g) Kumsaidia mwalimu kufundisha kulingana na kasi ya wanafunzi kuelewa; na
- (h) Kuvuta usikivu wa wanafunzi, hivyo kudumisha na kuimarisha nidhamu darasani.



### Changamoto za mbinu ya maswali na majibu

Mbinu hii ya maswali na majibu ina baadhi ya changamoto ambazo zinahitaji kuzingatiwa. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:

- (a) Mwalimu anaweza kutumia muda mrefu ili kukamilisha kufundisha mada fulani;
- (b) Mwalimu asipokuwa na ujuzi wa kutosha wa kuuliza maswali ambayo yanamwongoza mwanafunzi kujifunza, mbinu hii inaweza kupoteza mwelekeo wa somo; na
- (c) Wanafunzi kuwa tegemezi sana kwa mwalimu kwa majibu ya maswali yao.



#### Zoezi la 2.4

1. Eleza mikakati unayoweza kutumia ili kuhakikisha kila mwanafunzi anapata fursa sawa ya kujibu maswali.
2. Bainisha changamoto utakazokutana nazo na pendekeza hatua utakazochukua wakati unatumia mbinu ya maswali na majibu katika ufundishaji.

### Mbinu ya uchunguzi

Uchunguzi ni mbinu ya kujifunzia na kufundishia inayowapa wanafunzi fursa ya kufanya uchunguzi wa kitu fulani ili kupata majibu ya maswali aliyonayo kuhusu kitu hicho. Mbinu hii inahusisha matumizi ya zaidi ya mlango mmoja wa fahamu katika utafutaji wa maarifa au taarifa. Mbinu hii inatumika katika kutafuta majibu ya maswali, kuthibitisha nadharia, au kuelewa matukio. Wanafunzi wanaweza kuchunguza namna mazingira yanavyotunzwa.

### Umuhimu wa mbinu ya uchunguzi

Mbinu ya uchunguzi ni muhimu kwa sababu humsaidia mtoto kutumia zaidi ya mlango mmoja wa fahamu. Mbinu hii inamshughulisha mwanafunzi ndani na nje ya darasa kwa lengo la kukuza ubunifu, kufikiri kimantiki, kukuza stadi za mawasiliano na ushirikiano, kukuza kumbukumbu, kukuza udadisi na kuelewa mazingira yake ya uhalisia kufanya ugunduzi.





### Matumizi ya mbinu ya uchunguzi

Mchakato wa kutumia mbinu ya uchunguzi unarahisisha kufanya jaribio au uchunguzi ili kuthibitisha ukweli wa dhana husika. Uchunguzi huu unamwezesha mtoto kuelewa kwa urahisi kuliko maelezo yanayotolewa. Vilevile, mbinu ya uchunguzi inahisisha vitendo na humshirikisha mwanafunzi kujifunza kuititia vitendo hivyo. Katika kutumia mbinu hii, ni muhimu kuzingatia **umahiri unaokusudiwa kujengwa, mahitaji ya kila mwanafunzi, mazingira, upatikanaji wa vifaa na usalama wake.**

### Hatua za kufuata

Zifuatazo ni hatua za matumizi ya mbinu ya uchunguzi:

- (a) Kufanya uchunguzi wa shughuli iliyokusudiwa kabla ya kuwashirikisha wanafunzi;
- (b) Kuandaa vifaa na zana zinazohitajika wakati wakutumia mbinu ya uchunguzi;
- (c) Kuandaa maswali ya mwongozo, yanayoibua udadisi na yenye kuchochea utafutaji wa majibu;
- (d) Kuandaa shughuli ya uchunguzi ambayo ni rahisi na inayoelewka, shughuli ihusishe matumizi zaidi ya mlango mmoja wa fahamu;
- (e) Kushirikisha wanafunzi wote katika mchakato wa ujifunzaji;
- (f) Kuwaongoza watoto kuweka kumbukumbu za matokeo ya uchunguzi; na
- (g) Kuwaongoza wanafunzi kuwasilisha matokeo na kujadili kwa pamoja, kufanya tafakuri, kutoa mrejesho na maboresho.

### Changamoto za matumizi ya mbinu ya uchunguzi

Changamoto kubwa katika matumizi ya mbinu ya uchunguzi ni kuwa inahitaji usimamizi wa karibu ili kuhakikisha usalama wa kila mwanafunzi. Aidha, uchache wa vifaa na zana unaweza kuifanya mbinu hii isiwezeshe kufikia malengo ya ujifunzaji. Vilevile, mbinu hii inaweza kutumia muda mrefu mfano wanafunzi wakifanya uchunguzi nje ya darasa au muda mrefu katika maandalizi ya vifaa. Hivyo, kuwa mnyumbu na mbunifu katika kuitumia mbinu ya uchunguzi katika kufanikisha shughuli iliyokusudiwa, itasaidia kukabiliana na changamoto hizo.



## Kazi ya kufanya 2.5

Soma matini kutoka vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni na maktaba ya chuo kuhusu matumizi ya mbinu ya uchunguzi katika ujifunzaji na ufundishaji. Kisha andika mambo muhimu ulioyifunza na hifadhi katika mkoba wa kazi.



## Zoezi la 2.5

1. Umepanga kufundisha kwa kutumia mbinu ya uchunguzi wa vitu vinavyopatikana katika mazingira ya nje ya darasa. Bainisha mikakati utakayotumia ili kufanikisha shughuli hiyo.
2. Eleza namna mbinu ya uchunguzi inavyosaidia kukuza stadi za karne ya 21 kwa wanafunzi.

## Mbinu ya majadiliano katika vikundi

Majadiliano katika vikundi ni mbinu ya kufundishia na kujifunzia ambapo watoto/mwanafunzi hupewa nafasi ya kutoa mawazo aliyonayo wakiwa katika kikundi. Mbinu hii husaidia mwanafunzi kupata ujuzi mpya nje ya ule aliokuwa nao kabla ya majadiliano. Katika mbinu hii kiongozi wa majadiliano anaweza kuwa mwalimu au mtoto/mwanafunzi ye yeyote amba ye atapaswa kutoa fursa sawa kwa kila mshiriki kutoa mawazo yake. Majadiliano yanaweza kuwa katika vikundi vidogo au darasa zima na kufuatiwa na uwasilishaji. Ni muhimu kuzingatia kuwa mwishoni mwa uwasilishaji wa makundi, mwalimu tarajali anashauriwa kufanya hitimisho fupi la majadiliano ya darasani na kusitiza mambo muhimu yaliyojiteze katika mijadala. Kielelezo 2.3 kinaonesha majadiliano katika vikundi.



Kielelezo 2.3: Majadiliano katika vikundi

~~Faida ya mbinu ya majadiliano katika vikundi~~

Faida za kutumia mbinu ya majadiliano katika vikundi ni nyingi na zinaweza cuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Baadhi ya faida hizo ni:

- a) Wanafunzi **kujifunza** stadi za lugha za kuzungumza na kusikiliza;
- b) Ni **mbinu** inayowafanya wanafunzi waweze kufikiri kwa kina;
- c) Wanafunzi **wanajifunza** namna ya kupanga mawazo yao kimantiki;
- d) Wanafunzi **wanajengwa** hali ya kujimini kwa kuzungumza mbele za watu;
- e) Wanafunzi **hujifunza** kuhestimu mawazo ya watu wengine;
- f) Hukuza uwezo wa kujimini na kuvumiliana kwa washiriki;
- g) Hukuza ujuzi wa uongozi kwa washiriki;
- h) Njia inayofanya wanafunzi waelewe masuala yanayoikabili jamii; na
- i) Hukuza na kujenga moyo wa ushirikiano miongoni mwa wanafunzi.



### Changamoto za mbinu ya majadiliano katika vikundi

Pamoja na faida nyingi za mbinu ya majadiliano katika vikundi katika ufundishaji na ufundishaji, kuna changamoto ambazo zinapaswa kufahamika. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:

- (a) Maandalizi ya mtiririko wa majadiliano yanaweza athiri mafanikio ya mijadala;
- (b) Inahitaji nafasi kubwa kwa ajili ya vikundi vya darasani;
- (c) Majadiliano yanaweza kuwa hafifu au ya kiwango cha chini kutokana na mada inayojadiliwa;
- (d) Kama kiongozi wa kundi sio imara wanafunzi katika kundi wanaweza kutumia muda mrefu kwa kujadili mambo ambayo yako nje ya mada waliyopewa;
- (e) Kiongozi asipokuwa makini huenda suala jinalojadiliwa likapotoshwa kwa mabishano yasiyo na mwelekeo katika kikundi;
- (f) Endapo mwalimu atakuwa akitoa maelezo marefu wakati wa kazi za vikundi, basi ushiriki wa wanafunzi hufifishwa;
- (g) Baadhi ya wanafunzi kutoshiriki kikamilifu katika kutoa mawazo yao endapo mwalimu au kiongozi wa kundi hatozingatia kutoa fursa sawa kwa kila mwanafunzi; na
- (h) Inaweza ikachukua muda mrefu endapo mijadala haitasimamiwa vema na mwalimu.



#### Kazi ya kufanya 2.6

Soma vitibu na matini mbalimbali katika maktaba au vyanzo vingine rasmi vya taarifa mtandaoni kuhusu mbinu ya majadiliano ya vikundi ili kupata uelewa zaidi wa namna zinavyotumika katika mazingira tofauti.





Zoezi la 2.6

Eleza namna unavyoweza kutatua changamoto zinazotokana na mbinu ya majadiliano katika vikundi ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

### Mbinu ya kazimradi

Kazimradi ni mbinu ya kufundishia inayomshughulisha mwanafunzi na kumfundisha kwa vitendo. Mbinu hii inaweza kufanywa na mwanafunzi mmoja au kwa vikundi. Kazimradi inaweza kufanya kwa muda mrefu au hata muda mfupi kama vile kipindi kimoja cha darasani. Masomo mengi yanaweza kufundishwa kwa kutumia mbinu ya kazimradi. Kwa mfano katika Somo la Sayansi wanafunzi wanaweza kupewa kazimradi kuhusu kuchunguza mahitaji muhimu yanayohitajika ili mbegu iweze kuota.

### Faida ya mbinu ya kazimradi

Mbinu ya kazimradi ni njia ya kujifunza kwa vitendo na hutoa fursa kwa mwanafunzi kuunda ye ye binafsi kutokana na nadharia husika inavyojitekeza katika maisha halisi ya kila siku. Hivyo, mbinu hii inawaruhusu wanafunzi kutumia ujuzi wao katika mazingira halisi ya kazi. Njia hii, ina faida nyingi kwa wanafunzi, walimu, na hata jamii kwa ujumla. Baadhi ya faida hizo ni:

- (a) Wanafunzi huwa wanashiriki kikamilifu katika mchakato wa kujifunza;
- (b) Wanafunzi hufanya kazi kwa pamoja katika timu, na hivyo kujifunza jinsi ya kuwasiliana na kushirikiana na wengine;
- (c) Kukuza tabia ya kuhusisha mambo wajifunzayo na maisha ya kila siku;
- (d) Kukuza kujiamini na kujitegemea;
- (e) Huwapa wanafunzi nafasi ya kuwa wabunifu na kutatua matatizo kwa njia mbalimbali; na
- (f) Kazimradi inaweza kuunganisha shule na jamii kwa kuwataka wanafunzi kutatua matatizo yanayoikibili jamii.



**Namna ya kutumia mbinu ya kazi ya mradi**

Katika kutumia mbinu ya kazimradi ni muhimu kuzingatia hatua zifuatazo:

- (a) *Chagua mradi unaofaa:* mradi unapaswa kuhusiana na shughuli ya ujifunzaji na maisha halisi ya wanafunzi ili kuongeza hamasa yao. kwa mfano, kupanga safari ya shule na kuhesabu gharama, umbali, na muda; kubuni bustani ya shule na kuhesabu eneo, idadi ya mimea, na gharama za vifaa; kuandaa sherehe ya shule na kuhesabu idadi ya wageni, chakula, na vinywaji vitakavyotumika.
- (b) *Bainisha dhana lengwa ya kujifunza:* wakati wa kuandaa kazi mradi ni muhimu kutambua dhana ambazo wanafunzi watajifunza au kutumia wakati wa mradi. Mfano, stadi za kuhesabu au kujifunza matendo ya namba kama vile kujumlisha, kutoa, kuzidisha, na kugawanya au kupima na kuhesabu eneo, ujazo, na uzito au kusoma na kuunda grafu na chati ama kutumia pesa na kufanya mahesabu ya bajeti.
- (c) *Panga hatua za utekelezaji:* hakikisha unagawanya mradi katika hatua ndogo ndogo ili kurahisisha utekelezaji na ufuutiliaji wa maendeleo ya wanafunzi. Mfano, utafiti na ukusanyaji wa taarifa, uchambuzi wa taarifa, ubunifu na ujenzi wa mifano na maonesho au uwasilishaji wa matokeo kwa wanafunzi wengine au jamii.
- (d) *Toa msaada na mwongozo:* wasaidie watoto/wanafunzi wakati wa mradi kwa kuwapa rasilimali, vifaa, na ushauri wanapohitaji. hivyo hakikisha kuwa unaandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanayoruhusu ushirikiano na ubunifu. Toa maoni na kujibu maswali ya wanafunzi na kuwashimiza kufanya kazi kwa pamoja na kutatua matatizo kwa kutumia ujuzi wao.
- (e) *Tathmini na maoni:* tathmini uelewa wa wanafunzi wa dhana hizo na ujuzi wao wa kutatua changamoto kuititia mradi kwa kuangalia kazi ya wanafunzi, mawasilisho na ushiriki wao katika mradi au kutoa maoni ya kujenga ili kuwasaidia wanafunzi kuboresha uelewa wao na ujuzi wao na kupongeza mafanikio ya wanafunzi na kuwatia moyo kuendelea kujifunza.

**Changamoto ya mbinu ya kazimradi**

Pamoja na faida zinazotokana na kazi mradi, mbinu hii ina mapungufu ambayo





yanahitaji kuzingatiwa ili kuhakikisha utekelezaji wake unafanikiwa. Baadhi ya changamoto hizi ni pamoja na:

- (a) Kutekeleza kazimradi kunahitaji rasilimali nyingi kama vile fedha, vifaa na muda;
- (b) Mwalimu hana budi kufanya ushauri wakati wanafunzi wanapopata changamoto; na
- (c) Wakati mwingine wanaweza kukusanya na kutoa taarifa potofu endapo hawatopewa maelekezo ya kutosha.



#### Kazi ya kufanya 2.7

Tazama video ya kielimu kutoka mtandaoni zinazoonesha watoto/wanafunzi wakifanya kazimradi mbalimbali za ujifunzaji. Bainisha shughuli zinazofanyika na umuhimu wake katika ujifunzaji.



#### Zoezi la 2.7

Kazimradi ni mbinu muhimu ya kufundisha inayomshughulisha mwanafunzi na kumfundisha kwa vitendo. Buni namna kazimradi na uoneshe mkakati wa kuitekeleza katika mazingira ya chuo, kisha onesha namna ya kutathmini kazimradi katika muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji.

#### Mbinu ya majaribio

Ni mbinu mojawapo ya kufundishia na kujifunzia somo kwa vitendo. Mbinu hii inahusisha uchunguzi unaopelekea kuona matokeo yake. Jaribio linaweza kuwa la muda mfupi au mrefu kulingana na shughuli ya ujifunzaji. Mbinu hii ya majaribio inaweza kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji katika masomo mbalimbali mfano Sayansi, Jiografia na mazingira, Hisabati na Michezo. Mbinu ya majaribio inapotumika mwalimu anapaswa kuzingatia usalama na kuwasaidia





wanafunzi kuelewa dhana za msingi. Kwa mfano, katika somo la sayansi mbinu ya majaribio inaweza kutumika wakati wa ujifunzaji wa umahiri wa nguvu ya hewa, kuelea na kuzama, kumea na kukua kwa mbegu. Katika somo la Jiografia na mazingira mbinu hii inaweza kutumika katika jaribio la kutengeneza mvua ya bandia. Katika somo la Hisabati mbinu ya jaribio inaweza kutumika kufundisha dhana ya vipimo au upimaji wa nafasi kwa kutumia mazingira. Vile vile mbinu hii inaweza kutumika kujifunza dhana ya nafasi na uwezekano, upangaji wa maumbo na uchunguzi takwimu. Katika somo la Michezo mbinu ya jaribio inaweza kutumika kujifunza utamaduni wa chakula na mawasiliano ya kijamii.

#### Faida ya mbinu ya majaribio

Mbinu ya majaribio ni njia ya kisayansi inayotumiwa kufanya uchunguzi na kufikia matokeo yaliyotathminiwa kwa kina katika maeneo mbalimbali kama vile sayansi, elimu, na teknolojia. Faida za mbinu ya majaribio ni pamoja na:

- (a) Ni mbinu inayomshughulisha mwanafunzi ndani na nje ya darasa;
- (b) Matokeo yanayopatikana ni sahihi zaidi na yanaweza kurudiwa ili kuthibitisha uhalali wake;
- (c) Kusaidia kuthibitisha au kupinga nadharia au dhana na kupata uelewa wa kweli wa jinsi mambo yanavyofanya kazi;
- (d) Kutoa ufahamu wa kina kuhusu tabia, mchakato, au mfumo fulani kwa njia ambayo mbinu nyingine haziwezi kufanya;
- (e) Majaribio yanaweza kurudiwa na watafiti wengine kwa kutumia mbinu sawa, hivyo kutoa njia ya kuangalia uaminifu na usahihi wa matokeo;
- (f) Kutoa fursa ya kubuni na kujaribu suluhisho mpya kwa matatizo mbalimbali, hasa katika uhandisi na teknolojia; na
- (g) Aidha, mbinu hii inakuza stadi za mawasiliano kama itafanywa na wanafunzi katika vikundi.

#### Changamoto ya mbinu ya majaribio

Mbinu ya majaribio, ingawa ina faida nyingi, pia inachangamoto mbalimbali ambazo zinaweza kuathiri matokeo au utekelezaji wake. Changamoto hizi ni pamoja na:





- (a) Mbinu hii inahitaji muda mwingu katika kuandaa vifaa muafaka vyatia kufanya jaribio;
- (b) Inahitaji uangalizi mkubwa ili wanafunzi wasiumie;
- (c) Mbinu hii inaweza isifanikiwe iwapo vifaa havitaandalowi ipasavyo na hatua muhimu za uchunguzi kufuatwa;
- (d) Katika baadhi ya majaribio, hasa yale yanayohusisha viumbi hai, kuna changamoto za kimaadili kuhusu usalama, faragha, na ustawi wa washiriki; na
- (e) Mara nyingi majaribio hufanya katika mazingira yaliyodhibitiwa (maabara), ambayo yanaweza kuwa tofauti na hali halisi.



#### Kazi ya kufanya 2.8

Katika mafunzo ya ualimu kwa vitendo shulenii ongoza wanafunzi kwa kutumia mbinu ya jaribio kutohakana na shughuli ya ujifunzaji iliyobainishwa kwenye somo lako chaguzi.



#### Zoezi la 2.8

Eleza namna unavyoweza kupunguza changamoto zinazotokana na mbinu ya majaribio ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

#### Mbinu ya nyimbo

Nyimbo ni mbinu inayotumika zaidi kwa watoto katika darasa la awali, darasa la kwanza, na darasa la pili. Watoto hupata maarifa, stadi na mielekeo kuitia kuimba na kutenda. Mbinu hii inapotumika katika ujifunzaji na ufundishaji wa shughuli husika, huongeza ushiriki na uelewa wa umahiri husika kwa ufanisi.

#### Umuhimu wa kutumia mbinu ya nyimbo

Matumizi ya mbinu ya nyimbo ni muhimu katika ujifunzaji na ufundishaji wa watoto kwani zinashirikisha milango yao ya fahamu na husaidia katika ukuaji wa





kimwili, uratibu wa viungo vya mwili na uwezo wa kuzungumza. Vilevile, mbinu ya nyimbo inasaidia katika kuongeza uelewa na kukuza lugha, mawasiliano, stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, kutunza afya na mazingira, utamaduni na kufahamu jamii nyingine. Mbinu ya nyimbo ina umuhimu katika kufurahisha na kuburudisha, kukuza vipaji, kuvuta usikivu na umakini wakati wa kujifunza pamoja na kutunza kumbukumbu.

#### **Matumizi ya mbinu ya nyimbo**

Matumizi ya mbinu ya nyimbo hutumika kwa kuzingatia umahiri unaokusudiwa kujengwa, umri wa mtoto, mahitaji ya kila mtoto na mazingira. Mbinu hii inaweza kutumika katika mazingira ya ndani au nje ya darasa kulingana na shughuli iliyokususudiwa ili kutoa fursa kwa wanafunzi wote kushiriki. Matumizi ya mbinu ya nyimbo yanasaidia kujenga umakini na ujuzi wa kusikiliza kwani watoto wanapewa maelekezo na hatua za kuimba na kutenda wakati wa ujifunzaji.

#### **Hatua za kufuata**

Mbinu ya nyimbo hifuata hatua zifuatazo:

- (a) Kutambulisha wimbo;
- (b) Kuimba wimbo;
- (c) Kuimba na kuongoza watoto kuimba kwa pamoja;
- (d) Watoto kuimba wenywewe; na
- (e) Kufanya upimaji wa kile walichojifunza baada ya kumaliza kuimba na kutoa mrejesho.

#### **Changamoto za matumizi ya mbinu ya nyimbo**

- (a) Watoto wanaweza kuwa na uelewa tofauti kuhusu nyimbo kulingana na umri, lugha, na uzoefu wao. Nyimbo zinazotumia lugha ngumu au mitindo ya muziki isiyoleweka zinaweza kuwa changamoto kwa baadhi ya watoto.
- (b) Changamoto za upatikanaji wa nyimbo zinazoendana na shughuli na malengo ya kielimu. Nyimbo lazima zihusiane na umahiri uliokusudiwa, mara nyingine ni vigumu kutunga au kupata nyimbo zinazokidhi mahitaji ya shughuli.





- (c) Baadhi ya watoto hawapendi nyimbo. Hii inaweza kusababisha baadhi yuo kuhisi kutengwa au kutojihusisha na mbinu hiyo.
- (d) Kutumia nyimbo katika shughuli ya ujifunzajia na ufundishaji darasani, kunahitaji muda kwa kupanga, kuendesha, na kutathmini. Hii inaweza kuwa changamoto kufuata ratiba yenyе shughuli nyingi.
- (e) Kuunganisha nyimbo na maudhui ya kielimu inaweza kuwa changamoto pia, hasa kama nyimbo zinahitaji kupangwa kwa umakini ili kuhakikisha zinachangia kufanikisha malengo ya ujifunzaji.
- (f) Nyimbo zinapotumika kwa ajili ya ujifunzaji na ufundishaji, kuna uwezekano watoto kuelewa maudhui kwa njia istyo sahihi au kupotosha ujumbe uliokusudiwa wa nyimbo.
- (g) Ukosefu wa vifaa vya kutosha kunaweza kuathiri matumizi ya mbinu ya nyimbo kwani matumizi ya mbinu hii yanaweza kuhitaji vifaa vya kiufundi kama vile spika, vichezeshi vya muziki, au programu maalumu.



#### Kazi ya kufanya 2.9

Tunga wimbo unaoweza kutumika kujifunzia na kufundishia shughuli kwenye somo chaguzi katika elimu ya awali, msingi na elimu maalumu. Kisha weka katika mkoba wa kazi.



#### Zoezi la 2.9

1. Mbinu ya nyimbo hutumika zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wa watoto wa elimu ya awali. Bainisha mambo ya kuzingatia wakati unachagua nyimbo za kujifunzia na kufundishia.
2. Eleza kwa mifano zana na vifaa vinavyoweza kukusaidia katika matumizi ya mbinu ya nyimbo wakati wa shughuli za ujifunzaji na ufundishaji.





### Mbinu ya Kodály ya ishara za mikono

Hii ni njia ya kufundisha uimbaji na usomaji wa muziki iliyoundwa na Kodály. Mbinu hii inahusisha kufundisha muziki kwa kusikiliza na kuimba kwa kutumia ishara za mikono na silabi maalumu za muziki (solfa). Mbinu hii humsaidia mtoto au mwanafunzi kujifunza kuimba solfa (do re mi fa so la ti do) na kusoma muziki kwa njia ya ishara za mikono, hatua kwa hatua, huku akitumia nyimbo za michezo. Dhana kuu ni kwamba kila mtoto au mwanafunzi ana haki ya kujifunza muziki na kwamba muziki unapaswa kuwa sehemu ya maisha ya kila siku.

Mbinu hii inalenga kumfundisha mwanafunzi muziki kwa njia ya asili, kutumia nyimbo na michezo ya asili inayopatikana kwenye maisha yake ya kila siku. Mbinu hii inasisitiza, kuanza na kusikia kisha kuimba kabla ya kujifunza nadharia ngumu za muziki.

### Mambo ya kuzingatia unapotumia mbinu ya Kodály

- (a) *Kiwango cha uelewa wa mtoto/mwanafunzi:* Ni muhimu kufahamu kiwango cha uelewa wa muziki cha watoto/wanafunzi kabla ya kuanza. Hii inasaidia kupanga somo kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi.
- (b) *Kutumia nyimbo za asili zinazopatikana katika mazingira ya mwanafunzi:* Nyimbo zinazotumiwa zinapaswa kuwa sehemu ya utamaduni wa mwanafunzi. Hii inaongeza uelewa kwa wanafunzi kwani unamfundisha solfa kwa kutumia nyimbo ambazo anazifahamu.
- (c) *Kuzingatia utaratibu wa maendeleo na makuzi ya mtoto:* Mbinu ya Kodály inahusisha hatua za kimaendeleo na makuzi ya mtoto kwa kusisitiza, kuanza na mambo rahisi kuelekea magumu zaidi.
- (d) *Kuelewa solfa:* Watoto wanahitaji kufundishwa solfa ili waweze kuelewa mizani na sauti za muziki.
- (e) *Kutumia ishara za mikono:* Hii husaidia wanafunzi kuona na kuelewa tofauti za sauti na nafasi za noti katika mizani.
- (f) *Kutumia mazoezi ya vikundi:* Kujifunza kwa pamoja ni muhimu kwani kunawasaidia watoto kujifunza kushirikiana na kufanya kazi kwa umoja.

**Umuhimu wa mbinu ya Kodály katika ufundishaji na ujifunzaji wa muziki**

- (a) *Kujenga msingi thabiti wa muziki:* Mbinu ya Kodály inalenga kuanza na mambo ya msingi kama vile kuimba nyimbo rahisi na kutumia solfa. Hii inawasaidia watoto kujenga msingi thabiti wa ujuzi wa muziki ambao utaendelea kukua kadri wanafunzi wanavyoendelea na elimu yao ya muziki.
- (b) *Kukuza ujuzi wa kusikiliza na kutambua vipengele mbalimbali katika muziki:* Kupitia kusikiliza nyimbo na kuimba, wanafunzi wanajifunza kutambua sauti, mdundo, na melodia. Ujuzi huu wa kusikiliza na kutambua muziki ni msingi wa kujifunza kupiga ala za muziki na kuelewa muziki kwa undani zaidi.
- (c) *Kuimarisha uelewa wa muziki wa kinadharia:* Mbinu ya Kodály inawasaidia wanafunzi kuelewa muziki kwa njia ya kinadharia kupitia matumizi ya solfa na ishara za mikono. Hii inawawezesha watoto kuelewa mizani, vipimo vya sauti, na uhusiano kati ya noti mbalimbali, jambo ambalo ni muhimu kwa wanafunzi kujifunza kusoma na kuandika muziki.
- (d) *Kuzingatia utamaduni wa mtoto:* Kutumia nyimbo za asili kutoka kwenye mazingira ya mwanafunzi katika mbinu ya Kodály kunasaidia wanafunzi kuunganisha muziki na utamaduni wao wa asili. Hii inawasaidia kujenga uhusiano wa karibu na muziki, na kuongeza thamani na upendo wao kwa urithi wa utamaduni wao.
- (e) *Kujenga ushirikiano:* Mbinu ya Kodály inasisitiza kujifunza kwa vikundi ambapo wanafunzi wanajifunza kushirikiana na wenzao wakati wa kuimba au kucheza. Hii inawasaidia watoto kujifunza jinsi ya kufanya kazi kwa umoja, kusikilizana na kushirikiana, ambao ni ujuzi muhimu katika maisha yao yote.
- (f) *Kufurahia kujifunza muziki:* Kwa sababu mbinu hii inajumuisha michezo ya asili ya watoto, nyimbo, na mazoezi ya kupendeza, inafanya kujifunza muziki kuwa jambo la kufurahisha. Hii inawasaidia wanafunzi kukuza mapenzi ya muziki tangu wakiwa wadogo, na hivyo kuongeza uwezekano wa kuendelea na muziki katika maisha yao ya baadaye.





### Mambo muhimu ya kuzingatia

Mambo yafuatayo ni muhimu kuzingatiwa unapotumia mbinu ya ugunduzi unaoongozwa:

*Kuweka wazi malengo ya ufundishaji na ujifunzaji wa shughuli mahususi:* Andaa malengo ya mafunzo ili kukusaidia kufanikisha shughuli ya ufundishaji. Washirikishi wanafunzi wako wote ili wayaelewe malengo hayo na hivyo kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji.

*Kutoa mwongozo:* Mwongozo huu utahusisha aina ya kazi ya kufanya mathalani aina za mazoezi wanayopaswa kugundua na kuyaonesha, muda wa kufanya mazoezi hayo na namna ya uwasilishaji. Mfano, ikiwa utawapa kazi ya kubaini mazoezi ya msawazo, unaweza kuwapendekezea eneo ili upate nafasi ya kuwaafatilia na kuwasaidia.

*Kuhusu ugunduzi:* Ikiwa wanafunzi wanafanya mazoezi mathalani ya kujenga misili ya mwili basi wape uhuru wafanye wenyece huku ukiwapa usaidizi mdogo wa maboresho. Hii itasaidia kuona mazoezi mbalimbali waliyoyabaini na kuonesha kwa uwezo wao.

*Kutoa msaada katika usimamizi:* Wakati wanafanya mazoezi ni muhimu kuwapa usaidizi utakaosaidia kuhamasisha na kuboresha namna ya ufanyaji wa mazoezi hayo. Waongoze kurudia zaidi ya mara moja zoezi au mazoezi waliyoyagundua ili kuimarisha stadi za utendaji.

*Kutathmini ufanyakaji wa mazoezi:* Baada ya mazoezi, ongoza majadiliano na kufanya tafakuri ya mafunzo juu ya ugunduzi na nini wamejifunza zaidi. Hii itasaidia kuimarisha uelewa, kwa mfano, mazoezi ya viungo.

### Umuhimu wa mbinu ya ugunduzi

Mbinu ya ugunduzi ikitumika vizuri katika ufundishaji na ujifunzaji inaweza kuleta matokeo yafuatayo:

*Husaidia kukuza ugunduzi na utatuza wa changamoto mbalimbali:* Badala ya kuoneshwa aina za mazoezi na namna ya kufanya, wanafunzi wanajifunza wenyehe hivyo kukuza uwezo wao wa kiubunifu katika kufanya mazoezi mbalimbali.

*Inasaidia kukuza uhuru na motisha:* Wanafunzi wanapopewa fursa ya kugundua wao wenyehe, wanahisi kuwa na umiliki wa mchakato wa kujifunza hivyo kuongeza ari ya kufanya mazoezi kwa moyo.



*Kuimarisha maendeleo ya ujuzi:* Wanafunzi wanapofanya mazoezi wenyewe na kuhimizwa kuendelea kufanya kila mara husaidia kuimarisha viingo vyao na mwili kwa ujumla.

*Husaidia kukuza uelewa na kumbukumbu:* Kujifunza wenyewe kwa njia hii husaidia kuwa na uelewa wa kina na hivyo kuwa na kumbukumbu ya muda mrefu.



#### Kazi ya kufanya 2.II

Tembelea shule ya msingi jirani na chuo chako kisha chunguza namna ambavyo walimu wanatumia mbinu ya ugunduzi katika ufundishaji na ujifunzaji. Andika taarifa na weka kwenye mkoba wako wa kazi.



#### Zoezi la 2.10

1. Eleza namna utakavyoweza kutatua changamoto utakazokutana nazo wakati unatumia mbinu ya ugunduzi katika ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya awali, msingi na elimu maalumu.
2. Tathmini namna mbinu ya ugunduzi inavyotumika na wakufunzi wako katika kukujengea umahiri uliokusudiwa katika mazingira.

#### Mbinu ya fikiri-jozisha-shirikisha

Mbinu ya fikiri- jozisha- shirikisha ni njia ya kufundisha na kujifunza ambayo inampa mwanafunzi fursa ya kufikri binafsi kuhusu dhana fulani, kisha kuimarisha uelewa wake kwa kufanya mazoezi au shughuli, na hatimaye kuwashirikisha mawazo yake kwa wenzake mawazo yake. Mbinu hii inasisitiza ushiriki wa kila mwanafunzi katika mchakato wa ujifunzaji na inafaa sana katika darasa kubwa ambalo lina changamoto ya kuwaweka wanafunzi katika makundi madogo madogo.





### Umuhimu wa mbinu ya fikiri-jozisha-shirikisha katika kujifunzia na kufundishia

Mbinu hii hukuza uelewa kwa mwanafunzi anapopata fursa ya kufikiri yeye mwenyewe na uwezo wa kutafakari kuhusu maana au dhana mbalimbali. Mbinu hii pia hukuza uwezo wa kuwasiliana wakati wa kuwasilisha shughuli aliyopewa na kujadiliana na mwenzake katika jozi na kisha kushirikisha darasa zima. Vilevile, husaidia kufikiri kwa kina na kukuza uwezo wa kufikiri. Mchakato huu unasaidia mwanafunzi kuwa mdadisi, kuwa na uwezo wa kujiamini na kujisikia vizuri anaposhirikishwa.

### Matumizi ya mbinu ya fikiri-jozisha-shirikisha

Mbinu ya fikiri-jozisha-shirikisha huimarisha ushirikiano na kukuza maarifa. Mbinu hii inalenga kutoa uzoefu wa kina na kuimarisha uwezo wao wa kutumia maarifa kwa vitendo na kwa ushirikiano. Vilevile, matumizi ya mbinu hii yanazingatia kumfikirisha mwanafunzi katika kujenga umahiri uliokusudiwa. Kwa mfano, inamtaka kwanza afikiri binafsi, kisha wawasilishe na kujadiliana katika jozi na baadae kushirikisha darasa zima.

### Hatua za kufuata

Mbinu ya fikiri-jozisha-shirikisha inawezeshwa kwa hatua zifuatizo:

*Fikiri:* hatua hii huhusisha kumwongoza mwanafunzi kufikiri binafsi, kwa undani kuhusu dhanya au changamoto iliowasilishwa. Inahimizwa kuchunguza na kutafakari kwa kina kuhusu mada hiyo, na kufikiria mawazo mapya au mitazamo tofauti;

*Andika:* baada ya mtoto au mwanafunzi kutafakari kwa kina juu ya swali aliloulizwa na mwalimu, anaandika mawazo yake kabla ya kuanza kuwashirikisha wenzie. Hali hii husaidia kutosahau kile alichofikiri kabla ya kuanza kushirikisha wenzie katika jozi.

*Jozisha:* katika hatua hii, mwanafunzi hujozisha maarifa yake kwa kushirikishana katika jozi kutumia mbinu za kuimarisha, kama vile kufanya mazoezi, kujifunza kutokana na makosa, na kutumia mifano inayojumuisha vitendo ili kuimarisha kile alicho jisunza wakiwa wawili. Hii inahusisha kurudia na kuimarisha maarifa kwa njia ya vitendo au maswali; na





**Shirikisha:** katika hatua hii inahusisha kushirikiana na wengine katika kundi kubwa darasani ili kubadilishana mawazo, kuwasiliana kuhusu kile kilichofundishwa, na kujifunza kutoka kwa mitazamo ya wengine. Hii inaweza kufanyika kwa njia mazungumzo na majadiliano ya pamoja, kwa lengo la kupata mrejesho na kufanya maboresho.

#### *Changamoto za matumizi ya mbinu ya fikiri- Jozisha-shirikisha*

Ujifunzaji na ufundishaji kwa kutumia mbinu ya fikiri- jozisha-shirikisha katika darasa kubwa ni vigumu kusuutilia kila mwanafunzi kama ameshirikiana kikamilifu na wenzake. Hivyo, baadhi ya wanafunzi wanaweza kuwa na fursa ya kushirikisha mawazo yao, jambo linaloweza kupunguza ufanisi wa mbinu hii. Vilevile, kutumia mbinu hii inaweza kuchukua muda mwangi, hasa katika madarasa yenye shughuli nyingi. Wakati mwagine, kutoa nafasi kwa mwanafunzi kufikiria, kujadili na kushiriki ana kwa ana kunaweza kuchelewesha kusababisha kupoteza muda.



#### *Kazi ya kufanya 2.12*

Soma machapisho na rejea mbalimbali kutoka maktaba na vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni kuhusu namna ya kutumia mbinu ya fikiri-jozisha-shirikisha katika miktadha mbalimbali. Kisha andika mambo muhimu uliojifunza na weka katika mkoba wa kazi.



#### *Zoezi la 2.II*

Mbinu ya fikiri-jozisha-shirikisha inaweza kuwa bora zaidi kuliko mbinu nyingine za ujifunzaji na ufundishaji. Thibitisha kauli hii kwa mifano.

#### *Mbinu ya hadithi*

Hadithi ni mbinu ya asili katika ujifunzaji na ufundishaji darasani na hutumika na walimu katika kujenga umahiri kwa wanafunzi kuhusu jambo fulani. Mbinu hii inamvutia mwanafunzi na kuwezesha ujifunzaji wa tabia njema, mwenendo mwema, usikivu na kufikiri. Usimulizi wa hadithi hukuza ujifunzaji wa lugha hasa kuboresha msamati na kuwezesha uelewa kulingana na miktadha mbalimbali.



Aidha, mbinu ya hadithi katika madarasa ya awali, hutumia lugha rahisi, visa vichache, mambo mema kuwa ndiyo matarajio makuu, watoto kuwa wahusika wakuu, kuwa na msuko sahili, na hadhira kuwa wanafunzi wenye wewe. Mbinu ya hadithi inatumia dhana ya kufikirika ili kuwawutia watoto mfano, hadithi inayohusu wanyama kuwa katika eneo la shule na kujifunza kama wanafunzi wengine.

#### **Matumizi ya mbinu ya hadithi**

Katika kufanikisha ujifunzaji na ufundishaji wenye tija kwa mtoto/mwanafunzi, mbinu ya hadithi hutumika katika kukuza stadi nne za lugha ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Mbinu ya hadithi inahusisha masimilizi ambayo ni masupi na wahusika sio wengi katika hadithi. Matumizi ya lugha yanazingatia uwezo wa mtoto/mwanafunzi katika kuelewa lengo husika. Matumizi ya hadithi yanahusisha kutumia picha, vielelezo, zana au vifani vya zana, kufurahisha na kukuza kumbukumbu ya kudumu.

Uchaguzi wa hadithi katika ujifunzaji na ufundishaji unazingatia mambo kama vile hatua ya usomaji, umahiri unaokusudiwa kujengwa, msamati wezeshi kwa shughuli husika, stadi za kusoma kwa ufasaha na ufahamu. Mtoto au mwanafunzi anapewa fursa ya kujadili na kubashiri matukio muhimu, wahusika na tabia zao kwa kuhusianisha na maisha ya kila siku. Vilevile, huhusianisha na vitendo vya ujifunzaji mfano, maswali na majibu, kuhesabu vitu katika hadithi, kubuni kwa kuchora au kusimulia anavyoweza.

#### **Hatua za kuftuata**

Zifuatazo ni hatua za matumizi ya mbinu ya hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji:

##### **Kabla ya kusoma hadithi**

- (a) Kuchagua hadithi inayolenga umahiri na shughuli husika, kutumika katika ujifunzaji na ufundishaji;
- (b) Kuchagua msamati uliokusudia kujenga umahiri husika;
- (c) Kundaa vifaa vya kuwezesha ujifunzaji kama vile matini au hadithi simbuza, vitu halisi, kadi za picha, herufi au maneno, zana za kisasa kama radio, televisheni, filamu, vinasa sauti na zana nyingine za teknolojia ya kisasa;
- (d) Kusoma jina la hadithi;
- (e) Kueleza kuhusu picha zinazoonekana kwenye hadithi;





 **Zoezi la 2.12**

1. Eleza namna mbinu ya hadithi inavyoweza kujenga stadi za kusikiliza kwa wanafunzi.
2. Bainisha sifa za mbinu ya hadithi itakayowezesha watoto au wanafunzi kujenga umahiri katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji.
3. Bainisha changamoto na pendekeza namna mwalimu anavyoweza kuzitata wakati wa kutumia mbinu ya hadithi katika elimu ya awali.

**Mbinu ya matembezi ya galari**  
Matembezi ya galari ni mbinu ya kujifunza inayowapa wanafunzi fursa ya kuzunguka darasani au sehemu ya maonesho, kujifunza na kujadili kazi mbalimbali zilizowekwa kwenye ukuta au maeneo mengine. Mwalimu anaweza kuuliza baadhi ya maswali ya tathmini kwa kila kituo ili kurejesha baadhi ya wanafunzi wasioshiriki kikamilifu katika kikundi. Njia nyininge ya kuhakikisha wanafunzi wote wanashiriki kikamilifu, ni kugawa majukumu kwa wanafunzi katika kila kikundi. Majukumu hayo yanapaswa kuzungushwa kwa kila mwanafunzi wanapofika kituo kinachofuata.

Katika Sayansi, mbinu hii inaweza kutumiwa kwa njia mbalimbali kama vile vituo vya maonesho, vituo vya maswali na majibu, vituo vya majaribio, vituo vya uchunguzi wa data, vituo vya ufahamu na majadiliano. Hii, huwezesha wanafunzi kuwa na uzoefu wa kujifunza kwa kushirikiana na wenzao. Ni muhimu kuandaa vituo vizuri na kuhakikisha kila kituo kina vifaa vya kutosha ili wanafunzi waweze kujifunza kwa usanisi.

**Faida ya mbinu ya matembezi ya galari**  
Mbinu ya matembezi ya galari inatoa fursa ya kujifunza kwa majadiliano mionganini mwa wanafunzi, inakuza stadi za kijamii, na kuchochea mawazo ya kina, huku ikichangia katika uelewa wa kina wa dhana za Sayansi. Kwa kutumia mbinu hii, wanafunzi wanapata uzoefu wa moja kwa moja wa masomo na kuimarisha uwezo wao wa kutatua matatizo na kufanya maamuzi kwa kujitegemea. Baadhi ya faida za mbinu ya matembezi ya galari katika ufundishaji na ujifunzaji:

(a) Husaidia wanafunzi kukuza ujuzi wa ushirikiano na mawasiliano;

39





- (b) Huongeza uwezo wa wanafunzi wa kufikiria kwa kina na kufanya uchambuzi wa kisayansi;
- (c) Inawezesha walimu kuzingatia maeneo muhimu ya somo kwa kina, huku wanafunzi wakipata mtazamo bora wa dhana zinazohusiana na mada kuu;
- (d) Huongeza uwezo wa kutatua matatizo kwa kutumia maarifa na mbinu walizojfunza; na
- (e) Hujenga uwezo wa kujitathmini kuhusu uelewa wao na kuboresha maeneo yanayohitaji msaada.

#### **Changamoto za mbinu ya matembezi ya galari**

Ingawa mbinu ya matembezi ya galari huleta manufaa mengi, kuna changamoto zinazoweza kujitokeza kutoptana na utumiaji wa mbinu hii. Baadhi ya changamoto hizi ni kama vile:

- (a) Baadhi ya wanafunzi ambao hupendelea kujifunza kibinafsi kukataa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa maarifa;
- (b) Baadhi ya wanafunzi katika kikundi kutoshiriki kikamilifu na kuwategemea wanafunzi wenzao kakamilisha shughuli ya ujifunzaji waliopewa; na
- (c) Kuongezeka kwa kelele kama usimamizi wa darasa ni duni hupelekeea kushuka kwa umakini wa kujifunza kwa wanafunzi walioko kwenye matembezi ya galari.



#### Kazi ya kufanya 2.14

Soma kwa kina matini kutoka mtandaoni kuhusu namna ya kutumia mbinu ya matembezi ya galari katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa elimu msingi na maalumu.

#### **Mbinu ya kisa mafunzo**

Mbinu ya kisa mafunzo ni mbinu ya kufundishia ambayo hutumia hadithi au visa halisi (au viliviyotungwa) ili kusaidia wanafunzi kujifunza kwa kuchambua na kutatua matatizo yanayoibuka kutoptana na visa hivyo. Katika Somo la Sayansi, mbinu hii inaweza kuwa na manufaa makubwa kwa kusaidia wanafunzi kuelewa dhana mbalimbali kwa njia ya kiutendaji na kuhusisha dhana hizo na hali halisi za maisha.





### *Faida za mbinu ya kisa mafunzo*

Mbinu ya kisa ina faida mbalimbali zinazopelekea mwanafunzi kupata umahiri uliokusudiwa. Kwa kutumia mbinu hii, wanafunzi wanapata uwezo wa kufikiri kuhusu uelewa wao juu ya matatizo na changamoto zinazopatikana katika maisha yao ya kila siku. Kama kisa kikiandaliwa vizuri kinaweza kuhamasisha fikra tunduizi, na stadi za utatuizi wa matatizo yaliyopo katika mazingira yanayowazunguka wanafunzi. Baadhi ya faida za mbinu ya kisa mafunzo ni kama vile:

- (a) Wanafunzi hupata nafasi ya kutumia maarifa yao ya kisayansi kwa njia ya hadithi, visa halisi au viliviyotungwa, na kujifunza jinsi ya kuyatumia katika hali halisi;
- (b) Huweka dhana za kisayansi katika muktadha halisi, hivyo wanafunzi wanaweza kuelewa vyema jinsi dhana hizo zinavyofanya kazi katika maisha ya kila siku;
- (c) Wanafunzi kujenga uwezo wa kuchambua matatizo, kufanya maamuzi, na kutoa mapendekezo ya suluhisho, ambayo ni ujuzi muhimu katika masomo yao;
- (d) Ni kichocheo cha majadiliano ya kazi za vikundi, hivyo kuhamasisha ushirikiano na maoni tofauti; na
- (e) Husaidia wanafunzi kuelewa athari za kijamii na kimaadili na namna ya kufanya maamuzi yenye uwajibikaji.

### *Changamoto za mbinu ya kisa mafunzo katika Sayansi*

Pamoja na faida zitokanazo na mbinu ya kisa mafunzo, kuna vikwazo vinavyoweza kupelekea ufanisi wa mbinu hii kushuka. Baadhi ya changamoto zinazotokana na kisa mafunzo ni:

- (a) Visa vinavyohusisha dhana ngumu na zinazohitaji uchambuzi wa kina huweza kuchukua muda mwingi;
- (b) Kisa kinaweza kuwa kigumu kueleweka au kuchambuliwa, hasa kwa wanafunzi ambao hawana uelewa wa kutosha katika mada inayohusika;
- (c) Ni changamoto kuhakikisha wanafunzi wote wanashiriki kikamilifu katika mijadala na majadiliano;
- (d) Kufanya tathmini kwa usahihi wa kisa mafunzo unaweza kuwa changamoto, hasa katika kutathmini uwezo wa mwanafunzi kutatua matatizo na kufanya maamuzi; na



- (c) Ni vigumu kutumia matokeo yaliyopatikana kwenye kisa mafunzo kimoja kwenda kisa mafunzo kingine.



#### Kazi ya kufanya 2.15

1. Tembelea shule ya msingi iliyo jirani na chuo chako, chunguza namna walimu wanavyotumia mbinu ya kisa mafunzo katika ufundishaji na ujifunzaji. Andika taarifa kuhusu ubora na changamoto za matumizi ya mbinu hiyo na weka kwenye mkoba wako wa kazi.
2. Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa chambua mbinu nyingine za ufundishaji na ujifunzaji ambazo hazijatajwa katika sura hii.

#### Zoezi la marudio

1. Mwabuke ni mwalimu katika shule ya Msingi Mawenzi, anataka kutumia mbinu ya kisa mafunzo kuwezesha ujifunzaji katika darasa lake. Pendekeza hatua za msingi atakazoweza kuzifuata katika mchakato wa kutumia mbinu hiyo.
2. Tofautisha mbinu ya matembezi ya galari na mbinu ya changanyakete.
3. Eleza nafasi ya mwalimu na mwanafunzi katika kutumia mbinu ya igizo dhima kujenga umahiri uliokusudiwa katika muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji.
4. Mbinu ya Bungua Bongo haiwezi kutumika yenye na ikajikamilisha bila uwepo wa mbinu ya maswali na majibu katika ufundishaji na ujifunzaji. Thibitisha hoja hii kwa mifano.
5. Eleza namna mbinu ya mazoezi na marudio inavyoweza kutumika kujenga umahiri katika darasa jumuishi.
6. Mbinu ya majadiliano katika vikundi huwasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa kujieleza na kujiamini. Eleza namna wanafunzi wanavyoweza kujenga stadi za kuwasiliana kupitia mbinu hiyo.
7. Wanafunzi anaweza kukuza stadi mbalimbali za karne ya 21 kupitia mbinu ya ziara na kazimradi. Fafanua namna stadi hizo zinavyoweza kujengwa kwa wanafunzi kupitia mbinu hizo.

### Utangulizi

Zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ni muhimu katika kukuza umahiri uliokusudiwa kwa wanafunzi. Kati sura hii, utajifunza juu ya utengenezaji, ujifadhi na uundaji wa zana na vifaa vitakavyokusaidia katika ufundishaji na ujifunzaji. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kushirikiana na wanafunzi kutengeneza, ujifadhi na kuandaa zana za ufundishaji na ujifunzaji kulingana na mahitaji ya wanafunzi wote.



### Fikiri

Maandalizi na matumizi ya zana katika ufundishaji

### Zana na vifaa vya ujifunzaji

Zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ni nyenzo zinazotumiwa na walimu na wanafunzi ili kuwezesha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Katika mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, zana na vifaa huchukua nafasi kubwa katika kuboresha ufanisi wa mchakato wa ujifunzaji. Zana hizi ni pamoja na vifaa saidizi na rasilimali zinazowezesha walimu na wanafunzi kufanikisha ujenzi wa umahiri katika somo. Mifano ya zana za kufundishia na kujifunzia ni kama vile; vitabu vya kiada, vitabu vya ziada, ramani, michoro, picha, chati na vitu halisi kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinaongeza ushiriki wa wanafunzi katika ujifunzaji. Mifano ya vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji ni kama vile kompyuta, tabuleti, vifaa vya uchunguzi, majaribio ya kisayansi na programu za kufundishia.

Katika mazingira ya shule za elimu ya awali, msingi, na elimu maalumu, zana na vifaa vinaleta mabadiliko chanya ya ufundishaji na ujifunzaji kama zitatumwa kwa usahihi na mwalimu na wanafunzi. Zipo aina mbili za zana zinazoweza kutumika katika kufundishia na kujifunzia ambazo ni zana za asilia na zana za kisasa. Zana hizo zimegawanyika katika makundi matatu ambayo ni, zana maono, masikizi na masikizi-maono. Upatikanaji wa zana hizo unategemea kubuni, kufaragua na kutengeneza.

**Kazi ya kufanya 3.1**

Kwa kutumia maktaba ya chuoni kwako na vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni gawanya zana na vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji katika makundi makuu matatu. Kisha, weka kwenye mkoba wako wa kazi.

**Zoezi la 3.1**

1. Tofautisha zana za kufundishia na kujifunzia zinazohitajika kwa elimu ya awali, ya msingi, na elimu maalumu.
2. Pendekaze zana shirikishi zinazofaa kufundishia katika darasa jumuishi kwa wanafunzi wa shule ya msingi.
3. Eleza namna umahiri mahususikwenye muhtasari wa somo unavyozingatiwa katika kuchagua zana na vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji.

**Utengenezaji wa zana za kufundishia na kujifunzia**

Utengenezaji wa zana za kufundishia unahusisha michakato ya kubuni, kutengeneza, na kutathmini zana za ufundishaji na ujifunzaji ili kupata maarifa, ujuzi na mwelekeo kwa njia ya kueleweka na kuvutia. Ni muhimu kuzingatia ubora, urahisi wa matumizi kwa walimu na wanafunzi na uwezo wa kubadilika kulingana na mahitaji ya somo. Utengenezaji unahusisha hatua zifuatavyo:

**Hatua ya kwanza:** Kutambua mahitaji ya wanafunzi kwa kipitia, mazingira ya darasa husika, tathmini ya uwezo wao, changamoto zao na umahiri mkuu na mahususi wa somo.

**Hatua ya pilli:** Kubuni zana za ufundishaji na ujifunzaji kunahusisha uundaji wa nyenzo ambazo zitasaidia kufundisha na kujifunza kwa kuzingatia mahitaji mbalimbali ya wanafunzi. Katika uundaji wa zana za kufundishia unawenza kufanyika kwa kuzingatia rasilimali zinazopatikana kwa urahisi katika mazingira ya ujifunzaji kwa kufaragua makunzi kulingana na ujenzi wa umahiri.

**Hatua ya tatu:** Katika utengenezaji wa zana za ufundishaji, ni muhimu kuzingatia mahitaji ya wanafunzi, mazingira ya kujifunzia, na umahiri wa somo, huku zana zikiwa rafiki kwa mtumiaji na zinazochochea ushirikiano. Ubunifu na matumizi ya nyenzo zinazopatikana kwa urahisi huchangia kuongeza ufanisi wa zana hizo zinapotumika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.





**Hatua ya nne:** Kufanya majoribio ya zana katika mazingira halisi ya darasa ili kurekebisha kulingana na mrejesho kutoka kwa walimu na wanafunzi. Zana za kielektroniki zinahitaji uangalizi ili kuhakikisha usalama wa mtandao na urahisi wa matumizi, hivyo kuzifanya ziwe salama na rahisi kutumia.



### Kazi ya kufanya 3.2

Tathmini hali ya zana za kufundishia na kujifunzia katika mazingira ya shule ya msingi jirani na chuo chako na baini zana zinazohitaji matengenezo. Kisha, tengeneza mpango wa uhifadhi bora kama vile kupanga sehemu salama za kuhifadhi, kuweka ratiba ya ukaguzi ikiwemo hatua za kusafisha na kuhifadhi zana hizo baada ya matumizi.



### Zoezi la 3.2

- Wewe ni mwalimu wa darasa la nne na unatakiwa kufanya ukaguzi wa zana na vifaa vyote vya kufundishia na kujifunzia viilivypo darasani kwako. Kwa kutumia vigezo vya uundaaji wa zana, ainisha zana zinazohitajika kulingana na mahitaji ya wanafunzi wako.
- Unafundisha somo la Jiografia na Mazingira katika umahiri mahususi wa kuandaa zana ya ramani ya Tanzania. Eleza hatua utakazofuata kutengeneza zana itakayokidhi mahitaji ya wanafunzi katika darasa jumuishi.
- Eleza mpango wako wa uhifadhi wa zana kwa mwalimu mwenzako na namna mpango huu utakavyokuongezea ufanisi katika matumizi ya zana na kuhakikisha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji.

### Uhifadhi wa zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia

Ni muhimu kutunza zana kwa kuzihifadhi sehemu ambako ni salama ili zisiharibike. Zana huhifadhiwa kwa kufuata utaratibu unaokubalika kama vile kuhifadhi kwa kufuata aina ya malighafi zilizotumika kutengeneza, kwa kufuata wepesi au uzito wa zana yenye na utaratibu mwingine mzuri. Utunzaji zana unapunguza gharama ya muda na fedha katika kuzitengeneza au kununua upya. Yafuatayo ni baadhi ya mambo muhimu ya kuzingatia katika uhifadhi wa zana:



**Ubora wa zana:** Zana zinazotengenezwa, zinazobuniwa na kufaragua zinapaswa kuwa na ubora na zinadumu kwa muda mrefu.

**Mazingira sahihi:** Zana zinapaswa kuhifadhiwa kwenye sehemu maalumu ikiwemo yenye unyevunyevu unaofaa, joto linalotakiwa, mbali na yumbi au vitu vinavyoweza kuziharibu.

**Matengenezo ya mara kwa mara:** Zana zinapaswa kusafishwa, kufungwa upya, au kubadilishwa vipuri mara tu inapobidi ili vifaa hivyo viwe katika hali nzuri ya matumizi vinapohitajika wakati wa ujifunzaji.

**Usalama wa zana:** Ni muhimu kuhakikisha zana zote zinatunzwa kwa usalama ili kuepuka ajali au majeraha kwa watumiaji. Zana hatari zinapaswa kuhifadhiwa kwenye maeneo maalumu na mbali na wanafunzi au watu ambao hawana ujuzi wa kuzitumia.

**Utunzaji wa kumbukumbu:** Unahusisha kuorodhesha zana zote zilizopo, tarehe ya ununuzi na hali yake ili kufuatilia matumizi na kufanya maamuzi kuhusu matengenezo au ununuzi wa zana mpya. Ufutiliaji unaweza kutumia teknolojia, mfano misimbo ya haraka ya majibu.

**Mafunzo kwa watumiaji:** Ni muhimu kufundisha watumiaji namna ya kuzitumia, kuzihifadhi, na kuzitunza vizuri zana za ufundishaji na ujifunzaji ili kuepuka uharibifu.



### Kazi ya kufanya 3.3

1. Tembelea maeneo tofauti katika chuo au ofisi ambapo zana za kufundishia na kujifunzia zinahifadhiwa. Tathmini hali ya uhifadhi wa zana hizo ukizingatia usafi, utaratibu wa kuweka zana, na usalama kisha weka taarifa yako kwenye mkoba wa kazi.
2. Andaa mpango wa uhifadhi wa zana za kufundishia na kujifunzia katika somo la Sanaa na Michezo kwa wanafunzi wa Darasa la Tatu. Kisha, tengeneza orodha inayojumuisha namna ya kufuatilia na kuhakiki hali ya zana mara kwa mara.





## Zoezi la 3.3

1. Kama mwalimu, utachukua tahadhari gani ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi wanapotumia zana na vifaa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji? Bainisha zana na vifaa hivyo.
2. Fikiria uko katika mazingira ya shule au chuo ambapo kuna ubaba wa nafasi ya kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia. Eleza hatua unazoweza kuchukua ili kuhakikisha zana zinahifadhiwa kwa njia inayofaa bila kuathiri ubora wake.
3. Baininisha njia ambazo zinaweza kutumika kuwczesha walimu wenzako shulenii kuhusu mbinu za kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi na elimu maalumu.

**Uandaaji wa kivunge cha zana**

Kivunge cha zana ni kifaa au nyenzo inayotumika kuhifadhia zana (angalia Kielelezo 3.1). Kwa kawaida, zipo baadhi ya zana ambazo ni rahisi kuharibika, zina gharama kubwa na ni hatari kwa maisha ya binadamu kwa mfano, vimiminika vya kemikali. Kwa mazingira haya, mwalimu anatakiwa kuhifadhi zana hizo katika mazingira yatakayopelekea kuvitumia tena baadaye bila kuleta madhara kwa watuamajji.

Kivunge cha zana ni muhimu kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji. Chombo hiki kinaweza kufanya mchakato wa kufundishia na kujifunza kuwa salama, endelevu, wa gharama nafuu na unaozingatia mahitaji maalumu ya wanafunzi kama ifuatavyo:

- (a) Kulinda zana dhidi ya ucharibifu wakati wa matumizi ya ufundishaji na ujifunzaji na kubaki katika hali nzuri kwa muda mrefu.
- (b) Usalama kwa watumiaji wa zana za kufundishia na kujifunzia ni muhimu ili kupunguza hatari ya ajali au madhara kwa walimu na wanafunzi.
- (c) Matumizi endelevu ya zana za kufundishia na kujifunzia yanachangia kupunguza na kudhibiti hitaji la kununua vifaa vingine mara kwa mara.
- (d) Kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia kunatoa njia bora ya kulinda uwekezaji ambao shule imeufanya katika vifaa na zana.
- (e) Upatikanaji wa zana za kufundishia na kujifunzia zilizopangwa vizuri unawezesha kupata urahisi na ucharaka pale zinapohitajika kutumiwa.





Kielelezo 3.1: Kivunge cha zana



#### Kazi ya kufanya 3.4

1. Fanya utafiti katika shule iliyopo karibu na chuo chako kuangalia namna walimu walivyotengeneza vivunge vya kuhifadhiwa zana zao. Kisha, andaa taarifa na weka kwenye mkoba wako wa kazi.
2. Tengeneza kivunge cha zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira yanayokuzunguka.



#### Zoezi la 3.4

1. Kama mwaliimu eleza hatua utakazopaswa kuchukua kuhakikisha kivunge cha zana kinasaidia ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji tofauti ya ujifunzaji.
2. Tumia mifano ya zana na vifaa vya kufundishia vinavyotumika katika somo la Sayansi na fahamu namna unavyoweza kuboresha zana na vifaa hivyo kwa kutumia mbinu za utengenezaji.

**Zoezi la marudio**

1. Eleza dhana ya zana za kufundishia na kujifunzia na toa mifano ya zana ambazo zinaweza kutumika katika mazingira ya shule.
2. Eleza kwa mifano vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa kuchagua zana za kufundishia na kujifunzia katika mazingira ya elimu ya awali, msingi na elimu maalumu.
3. Bainisha hatua nne za utengenezaji wa zana za kufundishia na eleza umuhimu wa kila hatua katika kuhakikisha ubora wa zana hizo.
4. Eleza tofauti ya utengenezaji wa zana za kufundishia kwa matumizi ya kawaida na zana za kufundishia zinazozingatia mahitaji maalumu ya wanafunzi.
5. Chambua hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha uhifadhi wa zana za kufundishia na kujifunzia katika mazingira ya shule.
6. Bainisha changamoto zinazoweza kutokea katika uhifadhi wa zana za kufundishia na kujifunzia na pendekeza namna ya kuzitatu.
7. Fanya tathmini ya zana za kufundishia na kujifunzia zinazoweza kutumika katika elimu ya awali, msingi na elimu maalumu na eleza faida zake katika kuboresha ushiriki wa wanafunzi.
8. Bainisha mikakati unayoweweza kutumia ili kuhakikisha zana na vifaa vya kufundishia vinavyotengenezwa vinachangia kwa ufanisi katika mikakati ya kitaaluma shulenji.
9. Eleza zana utakazotumia katika kuandaa somo kwa watoto na wanafunzi wenyе umri na uwezo tofauti wa ujifunzaji wa elimu ya awali, msingi na wenyе mahitaji maalumu.
10. Eleza namna utavyohakikisha zana kama vile chati au picha zinakuwa na manufaa kwa wanafunzi wote darasani.
11. Chagua programu au kifaa cha kidijitali unachoweza kutumia na eleza namna kitakavyowasadid awanafunzi wenyе mahitaji maalumu ya ujifunzaji.
12. Eleza namna utakavyotengeneza zana za maono kwa ajili ya kuwezesha kujifunza herufi na namba. Onesha mifano ya namna utakavyozitumia katika kuboresho ujifunzaji kwa watoto wa elimu ya awali.
13. Eleza namna utakavyotumia zana za sauti kama ngoma na kinanda katika kuboresha ujifunzaji wa somo la muziki.
14. Fafanua namna unavyotumia chati za picha kuwasaidia wanafunzi wa Darasa la Pili kuelewa dhana ya Hisabati.



## Darasa salama, changamshi na jumuishi

### Utangulizi

*Darasa salama, changamshi na jumuishi linahakikisha mazingira bora ya kujifunza kwa wanafunzi wote. Linazingatia usalama wa kimwili na kisaikolojia ili kuhamasisha ushiriki wa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao. Katika sura hii utajifunza dhana ya darasa salama, changamshi na jumuishi, upangaji wa darasa kwa kuzingatia mazingira na mahitaji ya wanafunzi, upangaji wa zana katika kona za ujifunzaji kulingana na mahitaji ya wanafunzi na uchocheaji wa utayari na ushiriki wa wanafunzi katika ujifunzaji. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuandaa darasa salama, changamshi na jumuishi kulingana na mazingira na mahitaji ya kila mwanafunzi.*



Fikiri

Darasa salama, changamshi, na jumuishi katika ufundishaji na ujifunzaji

### Dhana ya darasa salama

Darasa salama ni chumba au mazingira yoyote anapo jifunzia mwanafunzi akiwa huru, mwenye amani, utulivu na afya nzuri pasipokuwa na shaka ya jambo lolote ambalo linawenza kumfanya asijifunze kwa umakini na ufasaha. Katika darasa salama walimu wanahakikisha kuwa wanafunzi hawakabiliwi na vitisho, unyanyasaji, au ubaguzi wa aina yoyote. Darasa linatakiwa kuwa na nidhamu, heshima na uelewano baina ya wanafunzi na mwalimu. Vilevile, linatakiwa kuzingatia usalama wa wanafunzi kimwili, kiakili, kihisia na kijamii. Kielelezo 4.1 kinaonesha ufundishaji na ujifunzaji katika darasa salama.



Kielelezo 4.1: Ufundishaji na ujifunzaji katika darasa salama

#### Ifa za darasa salama

Ji mwanafunzi aweze kujifunza kwa usalama akiwa darasani, ni muhimu juhakikisha kuwa darasa lina heshima na uelewano mzuri baina ya wanafunzi a walimu. Mazungumzo ya staha na yenye kuzingatia heshima katika mchakato a ufundishaji na ujifunzaji yanapaswa kupewa kipaumbele. Ni muhimu kujali ahitaji ya kihisia, kimwili, kiakili na kijamii ya mwanafunzi ili kuhakikisha iwa anajifunza katika mazingira bora.

Ilevile, ni lazima kufuata kanuni na taratibu zilizokubaliwa na darasa. Hii asaidia kudumisha nidhamu na utaratibu darasani. Ushirikiano baina ya anafunzi na walimu huchangia usalama wa darasa. Ushirikiano huu unaleta fanisi katika kufikia umahiri wa ujifunzaji.

Iotisha inapaswa kuzingatiwa ili kuhamasisha ujifunzaji. Walimu wanapaswa iwa na mikakati ya kuwatia moyo wanafunzi kushiriki kikamilifu katika asomo yao. Pia, ni muhimu kushirikisha wadau mbalimbali kama vile wazazi i walezi na viongozi ili kuhakikisha kuwa mazingira ya darasa yanabakia kuwa ilama na yanayojali maendeleo ya mwanafunzi kwa ujumla.



### Kazi ya kufanya 4.1

Fanya uchunguzi katika shule ya jirani na chuo chako kisha bainisha kama walimu wanazingatia kufundisha darasa salama, changamshi na jumuishi. Ibua changamoto zilizojitokeza na toa mapendekezo yako. Andika taarifa, kisha weka kwenye mkoba wako wa kazi.

#### Faida ya darasa salama

Darasa salama lina faida nyingi zinazochangia ufanisi wa ujifunzaji kwa wanafunzi. Kwanza, linaborcsa mafanikio ya ujifunzaji kwa kuwa wanafunzi wanakuwa na mazingira bora ya ujifunzaji. Hali hii inawawezesha kukuza ujasiri na kujiamini, wanafunzi wanakuwa na fursa ya kuuliza maswali na kushiriki katika ujifunzaji bila hofu.

Vilevile, darasa salama hujenga uhusiano dhabiti baina ya wanafunzi na mwalmi, hali inayofanya ujifunzaji kuwa na tija. Aldha, linawasaidia wanafunzi kukabiliana na changamoto mbalimbali za ujifunzaji wao kwa ufanisi, kwa kuwa wanajisikia kuwa huru wakati wote.

Mbali na hivyo, darasa salama linachangia katika kujenga nidhamu na uwajibikaji kwa mwanafunzi na mwalmi. Nidhamu inachochewa na hali ya kuheshimiana na kuthaminiana inayojengwa katika darasa. Hii hupelekea wanafunzi kuwa na tabia njema na kuwajibika zaidi katika ujifunzaji wao. Vilevile, darasa salama huibua fikra tunduizi na ubunifu mionganoni mwa wanafunzi. Wanafunzi wanapokuwa katika mazingira yasiyo na hofu, wanapata nafasi ya kufikiria kwa kina na kutoa mawazo mapya, hali inayochangia katika ubunifu na maendeleo ya kitaaluma.

Kwa upande mwingine, darasa lisilosalama linawenza kuathiri kiwango cha ujifunzaji wa wanafunzi. Mazingira yasiyosalama huongeza wasiwasi na woga mionganoni mwa wanafunzi, hivyo kuathiri uwezo wao wa kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji wao. Kukosekana kwa amani na utulivu wakati wa ufundishaji na ujifunzaji kunachangia kupunguza ufanisi katika ujifunzaji. Wakati mwingine wanafunzi wanaweza kuhisi kutengwa, hali inayozorotesha ujifunzaji.

Vilevile, darasa lisilosalama linachochea mazingira ya kutokujiamini kwa wanafunzi, hivyo kuwafanya kushindwa kujieleza au kushiriki kikamilifu katika shughuli za ujifunzaji. Athari hizi zinawenza kusababisha changamoto za kisaikolojia kwa wanafunzi na kupelekea kushuka kwa nidhamu. Kwa ujumla, ni muhimu kwa walimu kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira salama ili kujenga jamii yenye watu wanaothaminiana, kuheshimiana, na walio tayari kwa changamoto za maisha ya baadaye.





## Kazi ya kufanya 4.2

Tembelea shule ya msingi jirani na chuo chako na fuatilia hali ya usalama wa darasa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kisha, andika taarifa kuhusiana na hali ya usalama, mafanikio na changamoto ulizoziona na toa mapendekezo kwa mwalimu ili kuboresha usalama wa darasa.



## Zoezi la 4.1

1. Katika Shule ya Msingi Ukombozi, kuna ukosefu wa motisha kwa wanafunzi, matumizi duni ya lugha ya mawasiliano, na uchafu wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Kama mwalimu turajili:
  - (a) Eleza ni changamoto zipo zinazoweza kumkabili mwanafunzi anayesomea katika darasa hilo.
  - (b) Tathmini athari zinazoweza kumkumba mwalimu anayefundisha katika darasa hilo.
2. Kama Afisa Elimu Kata, umepokea taarifa kwamba darasa la mwalimu Twiga lina changamoto za usalama wa wanafunzi wanaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji kwa vitendo. Eleza mambo muhimu ambayo ungemshauri mwalimu azingatie ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi wake anapofundisha darasani.

## Darasa changamshi

Darasa changamshi ni mazingira ya kujifunzia ambapo wanafunzi wote wanaajishughulisha kwa ari na nguvu ili kuelewa somo kwa ufanisi bila kujali tofauti zao za kijinsia, kiakili, kihisia, kimaumbile, kimazingira na kiuchumi. Linaweza kuwa ni darasa lililosheheni zana mbalimbali kama picha za kuchorwa, picha za kubandikwa, mbegu za nafaka mbalimbali, vitambaa na majani ya mimea. Vilevile, linaweza kutumia mbinu za kuvutia ikiwemo matembezi ya galari, majadiliano ya vikundi na onesho mbinu ili kuchangamsha na kuleta ufanisi katika ujifunzaji na kuwezesha ujifunzaji wa wanafunzi. Uchangamshi unaweza kuonekana namna wanafunzi wanavyojibu maswali, wanavyojadili na kushiriki katika shughuli mbalimbali darasani.





### Sifa za darasa changamshi

Darasa changamshi ni darasa linalofuata kanuni na taratibu zilizokubaliwa na walimu na wanafunzi. Kanuni hizi husaidia kudumisha nidhamu na kuleta ushirikiano wa hali ya juu katika masomo. Aidha, darasa hili linahakikisha mazingira yake hayana hatari yoyote kwa wanafunzi na walimu, hali ambayo inachangia kuleta utulivu na usalama wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

Vilevile, darasa changamshi lina mpangilio mzuri unaohamasisha ufundishaji na ujifunzaji. Mpangilio huu unajumuisha upangaji wa madawati, meza, nà vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa namna inayowezesha walimu na wanafunzi kushirikiana kwa urahisi. Darasa hili linaangazia ujifunzaji unaozingatia mazingira tofauti, yakiwemo ya nje na ndani ya darasa, ili kutoa fursa kwa wanafunzi kujifunza kwa njia zinazobadilika kulingana na umahiri husika.

Matumizi ya kona za ujifunzaji katika darasa changamshi ni muhimu. Kona hizi zinapaswa kupangiliwa kwa ustadi na kujumuisha vifaa au zana zilizotengenezwa kutoka katika mazingira yanayowazunguka wanafunzi. Hii inawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kuhusisha mazingira yao katika ujifunzaji wao.

Kuta za darasa changamshi ni zile zinazoongea na jumuishi, zikiwa na machapisho, picha, michoro, na chati mbalimbali zilizobandikwa au kunininginizwa. Kuta hizi zinawezesha kujenga umahiri uliokusudia katika ufundishaji na ujifunzaji. Darasa changamshi linazingatia utoaji wa motisha kwa wanafunzi kulingana na mahitaji yao ya ujifunzaji, hali inayosaidia kuongeza ari na hamasa ya kujifunza.

### Faida za darasa changamshi

Darasa changamshi lina umuhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi, walimu, na shule kwa ujumla. Darasa changamshi huongeza ushiriki wa wanafunzi na kupunguza utoro shulen. Ushiriki huu wa wanafunzi hutokana na mazingira rafiki yanayowavutia na kuwafanya wajisikie sehemu ya ujifunzaji.

Pili, darasa changamshi hufanya ufundishaji na ujifunzaji kuwa rahisi kwa walimu na wanafunzi. Mazingira yenye mpangilio mzuri na vifaa vinavyohitajika husaidia wanafunzi kuelewa kwa urahisi na kumrahisishia mwalmu kufundisha kikamilifu. Hali hii inachangia kufanikisha malengo ya ujifunzaji kwa urahisi.

Aidha, darasa changamshi huchangia katika kuhamasisha elimu jumuishi ambayo husaidia kuondoa ubaguzi kati ya wanafunzi. Elimu jumuishi inawahuisha wanafunzi wote bila kujali tofauti zao, na kuwajengea stadi muhimu kama vile ubunifu, fikra tunduizi, mawasiliano, ushirikiano, uvumbuzi, udadisi, na kujiamini. Stadi hizi ni muhimu kwa maendeleo ya mwanafunzi, kitaaluma, kijamii na kihisia.





Vilevile, darasa changamshi huwapa wanafunzi hamasa na ari ya kujifunza. Wanafunzi wanapokuwa na ari ya kujifunza, wanajituma zaidi, jambo ambalo linaimarisha ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji. Hali hii pia inachangia kuimarisha kumbukumbu na uelewa wao, kwani wanafunzi wanakuwa na nia ya kweli ya kuelewa na sio tu kujifunza kwa ajili ya kufaulu mitihani.

Darasa changamshi hurahisisha upimaji na tathmini ya wanafunzi. Walimu wanawenza kutathmini uelewa wa wanafunzi kwa urahisi kutokana na ushiriki wao darasani. Hii husaidia kubaini maeneo ambayo mwanafunzi anahitaji msaada zaidi na hivyo kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Darasa changamshi humjengea mwanafunzi hali ya uzalendo kwa kuwa hulipenda, hulithamini, hulitunza na kulinda darasa lao. Hali hii huchangia kuwaandaa wanafunzi kuwa raia wema na wenye uwajibikaji katika jamii.

Kwa upande mwingine, darasa lisilo changamshi linaweza kuwa na madhara kwani hupunguza ushirikiano kati ya mwalimu na mwanafunzi, jambo linaloweza kuathiri ufundishaji na ujifunzaji. Vile vile linapunguza ari na hamasa ya mwanafunzi kujifunza, na hivyo kusababisha kushuka kwa kiwango cha nidhamu ya wanafunzi. Aidha, darasa lisilo changamshi huchangia kupungua kwa maarifa, ujuzi, na mwelekeo wa kitaaluma, kihisia na kijamii kwa wanafunzi, jambo ambalo linaweza kuathiri maisha yao ya baadaye.



#### Kazi ya kufanya 4.3

Chagua mbinu tano za kufundishia zinazochangamsha darasa kisha, jaza jedwali lifuatalo kuhusu mbinu ulizochagua:

Mbinu	Sifa za mbinu	Faida za mbinu	Mapungufu ya mbinu
Aina ya mbinu	Orodhesha sifa kuu ya mbinu hiyo	Eleza faida za kutumia mbinu hiyo	Taja madhara yanayoweza kutokea endapo mbinu hiyo haikutumika vyema

Baada ya kujaza jedwali, fanya tathmini ya namna mbinu hizo zinavyoweza kutumika kwa ufanisi katika kuchangamsha wanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Andika taarifa ikijumuisha hitimisho lako kuhusu mbinu hizo na weka taarifa yako kwenye mkoba wa kazi.





 **Zoezi la 4.2**

1. Wakati wa mafunzo kwa vitendo shulenii umegundua wanafunzi hawashiriki kikamilifu katika shughuli za ujifunzaji. Pendekesa mbinu utakazozitumia ili kuwezesha wanafunzi wako kushiriki kwa uchangamfu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
2. Eleza mbinu unazoweza kutumia ili kuwawezesha wanafunzi kukuza stadi za karne ya ishirini na moja kupitia ujifunzaji katika darasa salama na changamshi.

**Darasa jumuishi**

Darasa jumuishi ni darasa ambalo mwalimu na watoto au wanafunzi wenye mahitaji tofauti ya ujifunzaji wanashirikiana katika shughuli mbalimbali ili kujenga mazingira ambayo kila mtoto au mwanafunzi anajisikia salama, anapewa fursa ya kutoa maoni na kueleza matatizo yake. Mwalimu ni vyema kulifahamu darasa lake kwa idadi, tabia na mitindo yao ya ujifunzaji ili aweze kuwasaidia watoto au wanafunzi wake. Kielelezo 4.2 kinaonesha mfano darasa jumuishi.



**Kielelezo 4.2: Mfano wa darasa jumuishi**

56





### Sifa za darasa jumuishi

Ili watoto au wanafunzi wapate fursa sawa ya kujifunza, ni muhimu kuzingatia mahitaji yao na mazingira stahiki ya ujifunzaji. Hii inahusisha kuwapa mazingira yanayochoea ujifunzaji na kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika mchakato wa kujifunza. Ushiriki huu unaweza kufanikishwa kwa kutoa fursa kwa wanafunzi kushirikiana, kuuliza maswali, na kushiriki katika majadiliano, huku wakihimizwa kuwa wabunifu na kujitegemea katika ujifunzaji.

Wazazi au walezi wanapaswa kushiriki katika maendeleo ya watoto au wanafunzi kitaaluma, kiafya, kiimani na kihisia. Ushirikiano kati ya walimu na wazazi unasaidia kubaini changamoto zinazoweza kuathiri maendeleo ya watoto na kutafuta namna ya kuzitatua. Aidha, kuwepo kwa mikakati mizuri ya upimaji ni muhimu kwa kufanya utambuzi wa mapema wa mahitaji ya kila mwanafunzi. Hii inasaidia kuandaa mikakati maalumu ya kumsaidia mwanafunzi kufikia malengo katika ujifunzaji wake.

Vifaa au zana za kujifunzia na kufundishia vinavyolingana na mahitaji ya wanafunzi vinapaswa kupatikana kwa wingi. Hii inajumuisha vitabu, teknolojia, na vifaa vingine vya kufundishia ambavyo vinasaidia kuimarisha ujifunzaji. Kwa kuzingatia tofauti za ujifunzaji, kama vile kuona, kusikia, na kutenda, walimu wanapaswa kutumia mbinu zinazoendana na mitindo hiyo ili kuhakikisha kila mwanafunzi anapata fursa ya kujifunza.

Usawa wa kijinsia na ujumuishi ni masuala muhimu ya kuzingatiwa katika ufundishaji na ujifunzaji. Walimu wanapaswa kuhakikisha kuwa hakuna mwanafunzi anayebaguliwa kwa misingi ya kijinsia, rangi, au hali ya kimwili. Ujumuishi unamaanisha kutoa fursa sawa kwa watoto wote, ikiwemo wale wenye mahitaji maalumu, ili waweze kufikia uwezo katika ujifunzaji.

### Faida ya kuwa na darasa jumuishi

Darasa jumuishi ni dhana inayothamini na kuheshimu tofauti za wanafunzi kwa kuzingatia uwezo, mahitaji, na jinsia, huku ikitambua kwamba kila mwanafunzi ana uwezo wa kujifunza na kufanikiwa. Mojawapo ya faida ya darasa jumuishi ni kukuza uelewa na kukubalika kwa hali tofauti za watoto na wanafunzi. Kupitia mfumo huu, wanafunzi wanajifunza kuchukuliana na kuthamini tofauti zao za ujifunzaji. Hali hii inachangia kujenga jamii yenye mshikamano na heshima kwa kila mmoja.



Vilevile, darasa jumuishi linachangia katika kujenga ustawi wa kijamii baina ya wanafunzi, walimu, wazazi na wadau wengine wa elimu. Wanafunzi wote wakihusishwa na kuheshimiwa katika darasa, wana uwezo wa kujifunza na kujenga uhusiano mzuri. Hali hii inawasaidia kuwa na mitazamo chanya kuhusu wenzao, na pia inachangia kupunguza unyanyapaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Aidha, darasa jumuishi linawawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalumu kujitegemea katika ujifunzaji. Kwa kuwa wanapata fursa sawa ya kujifunza pamoja na wenzao, wanafunzi hawa wanajifunza stadi muhimu za maisha ambazo zinawasaidia kujenga hali ya kujiamini. Kujitegemea huku kunawapa fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za jamii na hatimaye kuchangia maendeleo yao binafsi na ya kijamii.

Walimu nao wananaufaika kuititia darasa jumuishi kwa kuimarisha maarifa, ujuzi, na umahiri wao. Kufundisha darasa lenye utofauti kunahitaji walimu kuwa wabunifu na kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji ambazo zinaweza kuwasaidia wanafunzi wote kujifunza kwa ufanisi. Hali hii inawawezesha walimu kuwa na uelewa mpana wa mahitaji ya wanafunzi na hivyo kuongeza uwezo wao wa kufundisha kwa ufanisi.

Mbali na hayo, darasa jumuishi linaondoa unyanyapaa dhidi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kutoa fursa sawa ya kujifunza. Unyanyapaa mara nyingi hutokana na kutengwa au kupuuuzwa kwa wanafunzi fulani, lakini kwa kuhusisha wanafunzi wote, darasa jumuishi linaweka mazingira ya usawa ambapo kila mwanafunzi anajihisi kuthaminiwa na kushirikishwa kikamilifu katika mchakato wa kujifunza.

Faida nyingine ya darasa jumuishi ni kuongeza maendeleo ya kiakili kwa wanafunzi. Wanafunzi wanapokuwa katika mazingira yanayoheshimu na kuthamini tofauti zao, wanakuwa na motisha zaidi ya kujifunza na hivyo kuongeza uwezo wao wa kuelewa na kutumia maarifa wanayopata darasani. Hii inachangia katika maendeleo ya kiakili na kitaaluma kwa wanafunzi wote, bila kujali tofauti zao.

Hata hivyo, kutozingatia ujumuishi katika darasa kunaweza kuwa na madhara. Kwa mfano, kubaguliwa na kutengwa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, kushuka kwa kiwango cha maendeleo ya kitaaluma, kujengeta kwa hofu na kutoaminiana baina ya wanafunzi. Vilevile, kutozingatia ujumuishi kunapelekeea kukosekana ubunifu kwa wanafunzi na walimu na huchangia kuongezeka kwa utoro wa wanafunzi. Hivyo, ni muhimu ufundishaji na ujifunzaji katika darasa jumuishi uzingatia kanuni za usawa na ujumuishi.



**Kazi ya kufanya 4.4**

Catika darasa unalofundisha wakati wa mafunzo kwa vitendo, umebaini baadhi a wanafunzi wanashiriki kwa ari katika ujifunzaji wakati wengine wanashindwa. Uumia vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni kuibua mbinu zitakazohamasisha wanafunzi wote kujumuika na kujifunza kwa ufanisi. Andaa taarifa kisha weka wenye mkoba wako wa kazi.

**Zoezi la 4.3**

- Afisa Elimu wa Mkoa ametembelea darasa unalofundisha somo la Hisabati ili kutathmini namna elimu jumuishi inayotekelizwa. Katika ziara hiyo, amekuomba kutoa maoni yako kuhusu faida na changamoto za kufundisha darasa jumuishi. Toa maoni yako
- Eleza namna utakavyomshauri mwalimu anayefundisha darasa lenye wanafunzi wenyewe changamoto ya uoni katika darasa jumuishi.
- Mwalimu Tukwa ana darasa lenye wanafunzi 25 wakiwemo wawili wenyewe changamoto ya kusikia. Pendekenza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji atakazotumia kuhakikisha wanafunzi wote wanapata fursa sawa ya kujifunza.

**Pangaji wa darasa kwa kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi**

Ili kuhakikisha darasa linakuwa salama, changamshi na jumuishi ni muhimu uzingatia mpangilio wa darasa. Upangaji wa darasa unahusisha mambo nbalimbali kama vile kuandaa nafasi, vifaa na shughuli za darasani ili kuhakikisha mazingira ya ujifunzaji yanakuwa bora. Mpangilio mzuri wa darasa unahitaji uzingatia mazingira halisi na mahitaji ya kila mwanafunzi ili kuleta chachu ya fundishaji na ujifunzaji wenyewe tija na kuvutia. Kwa mfano, kukaa katika duara, usu duara na umbo la 'U' kulingana na shughuli ya ujifunzaji. Kielelezo 4.3 inaonesha mfano wa mpangilio wa darasa jumuishi.



Kielelezo 4.3: Mpangilio wa darasa jumuishi



#### Kazi ya kufanya 4.5

Tembelea maktaba ya chuo ni kwako na tafuta taarifa zinazozungumzia namna ya kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanayochochea ujifunzaji kwa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi na maalumu. Andaa taarifa kisha weka kwenye mkoba wa kazi



#### Zoezi la 4.4

1. Fikiria unafundisha Somo la Sayansi Darasa la Nne na unatamani kuwapanga wanafunzi wako kwa kuzingatia mahitaji, utofauti na uelewa wa kila mwanafunzi katika ujifunzaji. Toa maoni yako kuhusu mambo muhimu utakayoyazingatia ili kukidhi mahitaji na mazingira halisi ya kila mwanafunzi.
2. Eleza namna unavyofanya tathmini ya mpangilio wa darasa ili kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
3. Fafanua namna mpangilio wa darasa unavyochangia kudhibiti tabia za wanafunzi na kuimarisha nidhamu ya darasa wakati wa ujifunzaji.



### Mambo ya kuzingatia katika kupanga darasa

Katika kupanga darasa, ni muhimu mwalimu kuzingatia mambo yafuatayo ili kuhakikisha darasa linabaki kuwa salama, jumuishi na changamshi katika ufundishaji na ujifunzaji.

**Kutambua afua stahiki za kila mwanafunzi:** Fanya tathmini ya kina ya mahitaji ya kila mwanafunzi kwa kuzingatia mambo yafuatayo: uwezo wa kitaaluma, hali ya kiuchumi, lugha, mahitaji maalumu, jinsia, na hali ya kijamii na kihisia. Ikkibidi, wasiliana na wazazi au walezi ili kuelewa vizuri mazingira ya nyumbani ya mwanafunzi na namna yanavyoathiri ujifunzaji wake.

**Kuweka umahiri mahususi:** Weka umahiri wa ujifunzaji unaozingatia mahitaji na uwezo wa kila mwanafunzi. Kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu, andaa mpango wa maendeleo binafsi unaojumuisha malengo, mikakati, na njia za kutathmini maendeleo yake.

**Kubuni mazingira ya kujifunzia:** Andaa mazingira ya darasa yanayowasaidia wanafunzi kujisikia salama. Hii inaweza kujumuisha mipangilio ya viti, zana za kujifunzia, na vifaa vya teknolojia. Tumia mbinu mbalimbali za ufundishaji kama vile kazi za vikundi, mafunzo ya vitendo, na matumizi ya teknolojia ili kukidhi mitindo tofauti ya ujifunzaji.

**Kuwezesha ushiriki wa kila mwanafunzi:** Hakikisha kila mwanafunzi anapata fursa ya kushiriki kikamilifu dasanasi. Tumia mbinu za kuchochea ushiriki kama vile majadiliano ya wazi, maswali ya kufikirisha, na kazi za vikundi na fuatilia maendeleo ya kila mwanafunzi.

**Kujenga mahusiano imara:** Jenga mahusiano imara na wanafunzi ili wajisikie huru kushirikisha matatizo yao na kupata msaada. Vilevile, weka ushirikiano mzuri na familia za wanafunzi ili kuhakikisha msaada unaotolewa nyumbani unalingana na ule wa shulenii.

**Kupima na kutathmini maendeleo:** Fanya tathmini endelevu kama vile kutoa kazi za nyumbani, mazoezi, na majoribio ya vitendo ili kufuutilia maendeleo ya wanafunzi. Tathmini na boresha mipango ya ufundishaji na ujifunzaji kulingana na matokeo.

**Kuboresha ufundishaji:** Hakikisha unajifunza mara kwa mara kuhusu mbinu bora za kufundisha na mbinu za kusaidia wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu. Pokea maoni kutoka kwa wanafunzi, wazazi, na walimu wenzako kuhusu mbinu za kufundisha na fanya maboresho inapobidi.





## Kazi ya kufanya 4.6

Tembelea shule ya msingi iliyopo jirani na chuo chako na fanya tathimini ya mpangilio wa madarasa. Andika taarifa ya namna ulivyotekeleza zoezi hilo na weka kwenye mkoba wako wa kazi.



## Zoezi la 4.5

1. Wewe ni mwalimu unayeanza kufundisha katika shule mpya. Darasa lako linaonekana kuwa na mpangilio wa kawaida lakini unahisi kuna mambo ambayo yanaweza kuboreshwa ili kuongeza ufanisi wa ujifunzaji. Kwa kutumia maelezo haya, eleza umuhimu wa kufundisha katika darasa lenye mpangilio mzuri.
2. Unakutana na changamoto ya kufundisha katika darasa ambalo madawati yamepangwa vibaya, vifaa vya kufundishia havipatikani kwa urahisi na wanafunzi wameingiwa na wasiwasi. Eleza mambo yanayopaswa kufanyika kutatatau changamoto hizo.

## Upangaji wa zana za kufundishia na kujifunzia

Upangaji wa zana ni mchakato wa kuchagua, kuandaa, na kupanga zana zinazofaa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji maalumu na uwezo wa wanafunzi. Upangaji wa zana unahitaji hatua mbalimbali kama vile: kutambua mahitaji ya wanafunzi, kuchagua zana zinazofaa, kuandaa mpangilio wa matumizi ya zana, na kuhakikisha zana hizo zinapatikana na zinatumika ipasavyo. Hatua hizi zimeelezewa kama ifuatavyo:

**Kutambua mahitaji ya wanafunzi;** Ni vema mwalimu kubaini maeneo ambayo wanafunzi wanahitaji msaada zaidi na aina ya mbinu zitakazofaa kulingana na mahitaji ya ujifunzaji. Kwa mfano mwanafunzi mwenye changamoto ya uoni au kusikia atahitaji vifaa saidizi ili kuwesheza ujifunzaji wake.

**Kuchagua zana zinazofaa;** Mwalimu anapaswa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi ili kuchagua zana zinazoendana na mahitaji yao kwa mfano ikiwa mwalimu anafundisha somo la Sayansi umahiri wa dhana ya uchunguzi wa kisayansi anaweza kutumia vitu halisi mfano viumbe hai, mazingira na vifaa vya kisayansi.





**Kuandaa mpangilio wa matumizi ya zana;** Mwalimu anapaswa kuamua ni wakati gani unaofaa kutumia aina fulani ya zana kwa kuzingatia umahiri unaojengwa kwa wanafunzi. Kwa mfano mwalimu anaweza kuandaaa mpangilio wa ujifunzaji kwa kuonesha video au picha zinazohusisha maudhui muhimu katika ujifunzaji wa sayansi kwa kutumia projecta.

**Kuhakikisha zana hizo zinapatikana na zinatumika ipasavyo;** Mwalimu anahitaji kuchunguza kwa makini kama zana zinazohitajika zinapatikana kwa urahisi na zinafanya kazi vizuri. Kwa mfano atatakiwa kujua kama kompyuta zote zitakazotumika kuwezesha ujifunzaji zimeunganishwa na programu za ujifunzaji zinazohitajika zimewekwa na kutoa maelekezo ya namna ya kutumia vifaa hivyo kwa ufanisi.



#### Kazi ya kufanya 4.7

1. Wakati wa mafunzo kwa vitendo shulenii umepangiwa kufundisha somo la Kiswahili katika Darasa la Nne, Chagua umahiri mahususi na panga zana za kufundishia zinazofaa na uandae mpangilio wa namna zana hizi zitakavyotumika darasani ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wote.
2. Tathmini zana na vifaa vya kufundishia vilivyopo chuongi kwako kwa kuzingatia ushirikishwaji wa wanafunzi wote katika ujifunzaji kisha, andika taarifa na weka kwenye mkoba wako wa kazi.



#### Zoezi la 4.6

Eleza-namna unavyoweza kupanga zana za kufundishia na kujifunzia ili kuhakikisha zinachangamsha, zinashirikisha na zinazingatia mahitaji ya wanafunzi wenye mitindo tofauti ya ujifunzaji.





### Kona za ujifunzaji

Katika darasa la Elimu ya Awali unatakiwa kuwa na kona za ujifunzaji ambazo ni maeneo yaliyowekwa, vifaa/zana mbalimbali za kujifunzia ambazo watoto wanaweza kuzitumia wakati wa ujifunzaji darasani au kwa muda wao wenywewe. Baadhi ya kona hizo ni kona ya Afya na Mazingira, Stadi za Awali za kihisabati, kisayansi na TEHAMA, Stadi za Awali za Maisha, Lugha na Mawasiliano, Utamaduni, Elimu ya Imani, Sanaa na Michezo. Baadhi ya kona za kujifunzia ni kama zifuatazo:

**Kona ya utamaduni, elimu ya imani, sanaa na michezo:** Kama ramani za tamaduni na kihistoria, vipeperushi, picha na video zinazowasilisha hadithi, mila na desturi za makabila mbalimbali, mipira, mikoko na vifaa vya michezo vinavyotumiwa katika michezo ya darasani. Vilevile ina vitabu vya hadithi na vitabu vya maadili ya dini mbalimbali, vifaa vya kuchora, kielelezo cha sanaa, kazi za vitendo kama vile kuchonga na uundaji kwa mikono.


**Kona ya lugha na mawasiliano:** Kama vile vitabu vya picha, kadi za maneno, santuri yenye nyimbo, vikaragosi vya maongezi, mchoro wa hadithi, rekodi za hadithi, ubao wa alfabeti, michezo ya maneno kama vile kibao fumbo, vitabu vya hadithi, kazi za misamiati, programu za kujifunza lugha na hotuba mbalimbali.

**Kona ya stadi za awali za maisha:** Kama vile mabango yenye tafsiri ya stadi mbalimbali za maisha, vyombo vya kuchezea (midoli, magari ya plastiki, vikaragosi, vifaa vya jikoni), vifaa vya elekroniki vinavyotoa sauti, vitabu vya picha, picha zinazoonesha shughuli za kila siku, vipande vya mbao, brashi, karatasi na kamba za kuruka.

**Kona ya afya na mazingira:** Kona hii inakuwa na vifaa vya usafi (sabuni, miswaki, taulo na maji safi), michoro na picha za mzunguko wa maji, picha za vyanzo vya maji, michoro ya uchafuzi wa mazingira, vikaragosi vya afya vinavyoolezea dhana za afya kama vile kula vyakula vya lishe, umuhimu wa chanjo na kukaa katika mazingira safi, bango la chakula bora, vifaa vya michezo kama kamba za mvutano, filamu fupi zinazohusu afya na mazingira.

**Kona ya stadi za awali za kihisabati, kisayansi na TEHAMA:** Ina vifaa vya kuhesabu (mawe madogo, maharagwe, au sarafu), vipande vya maumbo (duara, mraba, pembe tatu na mstatili), kadi za namba, darubini, miwani ya kuangalia wadudu, vifaa vya kukusanya mimea na wadudu, vifaa vya majaribio rahisi (vikombe, plastiki, nyavu, maji, chupa ndogo, siki, soda na puto) kompyuta ya toi au tabuleti ya watoto na vifaa vya kielektroniki vya kuchezea. Kielelezo 4.4 kinaonesha baadhi ya kona za ujifunzaji.



**Kielelezo 4.4: Baadhi ya kona za ujifunzaji****Kazi ya kufanya 4.8**

Andaa kona yenyne zana za kufundishia na vifaa vya majoribio katika umahiri wa kutumia stadi za awali za kihisabati, kisayansi na TEHAMA kisha uwafundishe wanafunzi namna ya kutumia zana hizo kwa usalama na uwasimamie wanapofanya majoribio. Andika taarifa na weka kwenye mkoba wako wa kazi.

**Zoezi la 4.7**

1. Mwalimu Jane ameandaa kona ya ujifunzaji kwa ajili ya Somo la Lugha na Mawasiliano ameweka vitabu vya hadithi, picha za maneno na zana za kuandika. Baada ya wiki moja amegundua kuwa baadhi ya wanafunzi wanapendelea kukaa katika kona hiyo zaidi ya muda uliopangwa wakisoma vitabu vya hadithi na kuchora picha. Eleza sababu zinazowafanya wanafunzi wavutiwe na kona hiyo.
2. Katika darasa la awali mwalimu ameandaa kona ya zana za kugusa kwa ajili ya somo la Sayansi ambapo wanafunzi wanaweza kushika na kuchunguza vitu kama mawe, mchanga, udongo, majani na vitu vingine halisi. Wakati wa kipindi, mwanafunzi mmoja anapoteza ari ya kujifunza na kuanza kuchenza mbali na wenzake. Eleza hatua utakazochukua kumsaidia mwanafunzi huyu arudi kwenye shughuli za kona na kushiriki kikamilifu katika somo.



## Zoezi la marudio

1. Eleza sifa ambazo darasa salama, changamshi, na jumuishi linapaswa kuwa nazo.
2. Fafunua dhana ya mpangilio wa darasa na kona za ujifunzaji.
3. Eleza madhara yanayoweza kutokea endapo mwalimu hatazingatia mazingira halisi na mahitaji ya kila mwanafunzi wakati wa kupanga darasa.
4. Kwa kutumia umahiri ulioupata kwenye somo la Falsafa ya Elimu na Maadili ya ualimu, toa mapendekezo ya kuboresha stadi za mwalimu katika kuandaa darasa salama, changamshi, na jumuishi.
5. Utekelezaji wa elimu jumuishi unakumbana na changamoto nchini Tanzania. Eleza changamoto hizo kwa kutumia mifano halisi.
6. Shuleni kwako, kuna darasa lenye kona za kujifunzia ambazo zinaendana na dhana ya elimu jumuishi. Eleza namna kona hizo zinavyosaidia katika mchakato wa ujifunzaji.



Sura ya  
Tano

## Usimamizi wa darasa wakati ufundishaji na ujifunzaji

### Utangulizi

*Usimamizi wa darasa ni kipengele muhimu katika kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ujifunzaji. Usimamizi mzuri wa darasa huwezesha walimu kudhibiti nidhamu na kuhamasisha ushirikiano mionganini mwa wanafunzi. Katika sura hii utajifunza dhana ya usimamizi wa darasa, mahitaji ya ujifunzaji kwa kila mwanafunzi, ushiriki wa mwanafunzi katika ujfundishaji na ujifunzaji. Vilevile, utajifunza kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa, mbinu na zana jumuishi na changamshi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kumudu mbinu za usimamizi wa darasa katika ujfundishaji na ujifunzaji.*



Fikiri

### Darasa bila usimamizi

#### Dhama ya usimamizi wa darasa

Usimamizi wa darasa ni kipengele cha msingi katika mchakato wa ujfundishaji na ujifunzaji kwa kuwa unahusisha mikakati inayotumiwa na walimu ili kuhakikisha kuwa shugbuli za ujifunzaji zinaendelea bila usumbufu na kwa ufanisi. Mchakato huu unalenga kuunda mazingira yanayosaidia maendeleo ya kitaaluma, kihisia na kijamii ya wanafunzi darasani.

Usimamizi wa darasa unahusisha mikakati na mbinu mbalimbali ambazo walimu wanatumia ili kuimarisha nidhamu, kuhamasisha ushiriki wa wanafunzi katika ujifunzaji, kupima maarifa na kuleta usawa katika mazingira ya ujifunzaji. Usimamizi huu unahitaji mwalimu kuwa na umahiri wa kuchanganua hali ya darasa, kutambua mahitaji ya ujifunzaji, na kuchukua hatua za makusudi ili kuzuia na kushughulikia changamoto zinazoweza kuathiri mchakato wa ujifunzaji.





## Kazi ya kufanya 5.1

- Kwa kutumia programu andishi, tayarisha taarifa fupi juu ya dhana ya usimamizi wa darasa ikieleza maana, umuhimu, na namna inavyohusiana na ufanisi wa kujifunza. Weka taarifa hii kwenye mkoba wako kazi.
- Fanya utafiti kwa kutembelea shule iliyopo jirani na chuo chako na chunguza namna dhana ya usimamizi wa darasa inavyotekelizwa. Kisha andika taarifa na weka kwenye mkoba wako wa kazi.



## Zoezi la 5.1

- Eleza namna unavyoweza kuunda mazingira ya darasani yanayochoea ushiriki wa wanafunzi katika masomo ukizingatia mbinu na mikakati ya usimamizi wa darasa kwa ngazi ya elimu ya awali, msingi, na elimu maalumu.
- Tathmini umuhimu wa kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi katika elimu ya awali, msingi, na elimu maalumu wakati wa kusimamia darasa na eleza mwalimu unavyoweza kufanikisha ujifunzaji.
- (a) Pendekeza mbinu za kudhibiti changamoto zinazoweza kujitokeza darasani wakati wa utekelezaji wa usimamizi wa darasa katika elimu ya awali, msingi, na elimu maalumu.  
(b) Fafanua namna mbinu hizo zinavyoweza kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji.

## Mahitaji ya kila mwanafunzi

Kila mwanafunzi ana mahitaji maalumu ya ujifunzaji ambayo yanapaswa kuzingatiwa ili kuhakikisha mchakato wa kujifunza unafanikiwa. Mwalimu anapaswa kutumia mbinu za ufundishaji na usimamizi wa darasa zinazokidhi mahitaji haya kwa njia inayojenga mazingira bora ya kujifunzia. Mambo ya kuzingatia katika kubainisha mahitaji ya usimamizi wa darasa ni kama ifuatavyo:

- Kutathmini ujuzi na uelewa wa kila mwanafunzi ili kupanga mbinu za ufundishaji kulingana na viwango vyao vya uelewa.
- Kupanga mazingira ya darasa kwa kuzingatia ustawi wa kimwili na kisaikoloja wa kila mwanafunzi ili kuhakikisha wanafunzi wote wanapata mazingira mazuri ya kujifunzia.





- (c) Kujenga mazingira rafiki na yenyе ushirikiano, msaada wa kihisia na uelewa wa kutoa msaada kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalumu ya ufundishaji na ujifunzaji.
- (d) Kurekebisha mbinu za ufundishaji kulingana na mahitaji ya wanafunzi wote ili kuhakikisha kuwa mbinu zinaendana na mahitaji yao ya ujifunzaji.
- (e) Kufuatilia maendeleo ya wanafunzi kwa ukaribu na kutoa mrejesho wa uboreshaji.



## Kazi ya kufanya 5.2

1. Tafiti na andika taarifa kuhusu mbinu bora za tathmini ya uelewa wa wanafunzi katika shule ya jirani na chuo chako kwa kuzingatia stadi za karne ya 21. Kisha weka kwenye mkoba wako wa kazi.
2. Andika mpango kuhusu namna unavyoweza kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ili kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo darasani kupata fursa sawa ya kujifunza.



## Zoezi la 5.2

1. Eleza hatua muhimu zinazoweza kuchukuliwa na mwalimu ili kuhakikisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu anapata fursa ya kujifunza.
2. Bainisha mbinu zinazoweza kutumika ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenyе mitindo tofauti ya ujifunzaji.
3. (a) Eleza namna mwalimu anavyoweza kupanga shughuli kwa mwanafunzi mmoja mmoja darasani ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenyе mitindo tofauti ya ujifunzaji.  
(b) Kwa kutumia mifano halisi, bainisha shughuli zinazoweza kufanya na mwanafunzi mmoja mmoja ili kuhakikisha anapata msaada stahiki katika ufundishaji na ujifunzaji.
4. Bainisha mbinu za usimamizi wa darasa ambazo zinaweza kutumika kuwezesha wanafunzi wenyе mahitaji maalumu kuboresha ushirikiano na hali ya kujifunza darasani.



### Ushiriki wa mwanafunzi katika ujifunzaji

Ushiriki wa mwanafunzi katika ujifunzaji unarejelea kiwango ambacho mwanafunzi anahusishwa kikamilifu katika mchakato wa kujifunza, ikijumuisha utayari wa kushiriki, kuuliza maswali, na kufanya maamuzi kuhusu ujifunzaji wao. Ushiriki huu ni muhimu kwa mwanafunzi katika mazingira ya kujifunzia ili kupata matokeo chanya ya ufundishaji na ujifunzaji. Kuzingatia na kuhamasisha ushiriki wa mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji ni hatua muhimu katika kuhakikisha mafanikio bora ya ufundishaji na ujifunzaji.



#### Kazi ya kufanya 5.3

1. Kwa kutumia video au programu maalumu za kielimu eleza namna teknolojia inavyoweza kuhamasisha ushiriki wa wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika umahiri mahususi utakaouchagua.
2. Tembelea darasa katika shule ya msingi iliyoko karibu na chuo chako kisha chunguza ufundishaji na ujifunzaji na andika taarifa kuhusu ushiriki wa wanafunzi wakati wa ujifunzaji. Weka taarifa kwenye mkoba wako wa kazi.

### Kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa

Kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa ni muhimu kwa walimu ili kuhakikisha kuwa mazingira ya darasani yanakuwa na tija katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Usimamizi mzuri wa darasa huwezesha kujenga nidhamu, kudumisha utulivu, na kumsaidia kila mwanafunzi kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji. Kanuni na taratibu zilizo wazi, husaidia darasa kuwa na mwenendo mzuri, jambo ambalo linaweza kuboresha matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji.



#### Kazi ya kufanya 5.4

1. Tumia kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa kuandaa somo la dakika 40 na kulifundisha Darasa la Tano katika shule ya msingi iliyopo jirani na chuo chako. Kisha andika taarifa kuhusu nidhamu na ushiriki wa wanafunzi wakati wa ujifunzaji, na weka taarifa kwenye mkoba wako wa kazi.
2. Tumia maktaba na vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni kutafuta na kueleza umuhimu wa kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Andika taarifa, na weka kwenye mkoba wako wa kazi kwa ajili ya marejeleo.





Zoezi la

5.3

1. Katika Shule ya Msingi Jumuiya, mwanafunzi mwenye changamoto ya uoni alijunga na darasa la kawaida. Eleza hatua ambazo mwalimu atachukua ili kuhakikisha mwanafunzi huyu anashiriki ipasavyo katika shughuli za ujifunzaji darasani.
2. Ibuu changamoto zinazoweza kumkabili mwalimu katika kuzingatia kaapuni na taratibu za usimamizi wa darasa.
3. Bainishaa mbinu ambazo mwalimu anaweza kutumia **kuhamasisha** ushiriki wa watoto wa elimu ya awali kwa kuzingatia mahitaji yao ya ujifunzaji.

### Mbinu na zana shirkishi, jumuishi na changamshi

Mbinu na zana shirkishi, jumuishi, na changamshi ni muhimu katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Mbinu shirkishi, kama kazi za vikundi na mijadala, huongeza ushiriki wa wanafunzi na kuboresha ushirikiano katika ujifunzaji. Zana jumuishi, kama michoro na programu za kielektroniki, zinaendana na mitindo mbalimbali ya kujifunza, huku mbinu changamshi, kama michezo ya kufundishia darasani, zinaongeza motisha na umakini katika ujifunzaji. Kutumia mbinu na zana hizi kwa ufanisi husaidia walimu kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yenye tija.

Matumizi ya mbiyu na zana shirkishi, jumuishi, na changamshi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji huimarisha ufanisi wa elimu kwa njia zifuatazo:

**Mbinu shirkishi** kama vile kazi za vikundi na mijadala, zinasaidia wanafunzi **kushirikiana** na kubadilishana mawazo, hivyo kuimarisha ushirikishwaji na uelewa wa kina.

**Mbinu jumuishi** zinazotumia michoro na zana za kielektroniki, zinasaidia kufanya mbinu za ufundishaji zikidhi mahitaji mbalimbali ya wanafunzi na kuimarisha mazingira ya kujifunzia.

**Mbinu changamshi** kama michezo ya kielimu na shughuli zinazohusisha ushirikiano katika ujifunzaji, huongeza motisha na umakini wa wanafunzi. Kutumia mbinu na zana kwa ufanisi, walimu wanawea kuwavutia, kuwaburudisha, kuwashirikisha na kuwamotisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.



**Zoezi la marudio**

1. Mwalimu Asha anakabiliana na changamoto zinazohusiana na usimamizi anapofundisha darasa jumuishi. Bainisha changamoto hizo na fafanua namna anavyoweza kuzitatua ili kufanikisha ujifunzaji.
2. Bainisha vipengele muhimu vinavyounda usimamizi wa darasa. Eleza namna mwalimu anapaswa kuviiimarisha.
3. Eleza umuhimu wa mwalimu kuelewa na kujali mahitaji ya **kila wananfunzi** darasani wakati wa ufundishaji na ujifunzaji
4. Bainisha faida za kuhamasisha ushiriki wa wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
5. Fafanua umuhimu wa mwalimu kuweka na kutekeleza kanuni na taratibu za darasani kwa ufanisi.
6. Eleza namna kanuni na taratibu za darasani zinavyochangia katika kujenga mazingira salama na yenyе nidhamu kwa wanafunzi.
7. Bainisha mambo ambayo mwalimu anapaswa kuyazingatia wakati wa kuunda taratibu za usimamizi wa darasa kwa ufanisi.



**Sura ya Sita**

## Teknolojia na vifaa saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji

**Utangulizi**

Matumizi ya teknolojia, na vifaa saidizi kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri yanaweza kuboresha uelewa na ujuzi wa wanafunzi kwa kuwapatia, maarifa, stadi na mwelekeo. Katika sura hii utajifunza teknolojia na vifaa saidizi, sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji katika darasa kubwa. Vile vile, utajifunza mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji.

**Fikiri**

Matumizi ya teknolojia na vifaa saidizi vyta ufundishaji na ujifunzaji

**Teknolojia na vifaa saidizi**

Katika kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji matumizi ya teknolojia na vifaa saidizi ni nyenzo muhimu za kuzingatia katika ujenzi wa umahiri. Teknolojia inawezesha walimu kuandaa na kufundisha kwa usanisi kwa kutumia vifaa kama projekta na programu za mtandaoni ambazo hurahisisha shughuli za ufundishaji na ujifunzaji. Vifaa saidizi vinaweza kutumika kuwezesha ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kupata fursa sawa ya ujifunzaji. Baadhi ya vifaa saidizi kama vile vifaa vya kusikia, kompyuta zenyet programu maalumu, kibodi ya Braille, kibao henamu, kibao na kitobozi, rula ya kusomea na mifumo ya ufuutilaji kwa macho na vifaa saidizi vingine kulingana na mahitaji maalumu ya wanafunzi.

**Kazi ya kufanya 6.1**

Kwa kutumia vyanzo rasmi vya taarifa cleza namna teknolojia na vifaa saidizi vinawezesha katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Andaa taarifa hiyo na weka kwenye mkoba wako wa kazi.

73





## Zoezi la 6.1

1. Fafanua namna simu janja, tabuleti, projekta na kompyuta vinaweza kutumika kama nyenzo za kujifunzia kwa wanafunzi ndani na nje ya darasa.
2. Bainisha changamoto zinazoweza kutokea wakati vifaa nya teknolojia vinapotumika darasani na pendekeza hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kuhakikisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unafanikiwa.
3. Bainisha vifaa saidizi ambavyo vinawezesha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
4. Eleza namna teknolojia inavyoweza kuunganishwa na mbinu za ufundishaji za jadi ili kuboresha uzoefu katika ujifunzaji.
5. Mwalimu Zuri anafundisha darasa lenye wanafunzi wa elimu ya awali, elimu msingi na wenye mahitaji maalumu. Tathmini teknolojia na vifaa saidizi atakavyotumia kulingana na walengwa na namna zitakavyoweza kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

## Sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji

Mbinu ya sanaa na michezo ni njia za kufundisha zinazotumia ubunifu na shughuli za kimwili ili kuwasaidia wanafunzi kukua kiakili, kijamii na kihisia. Kupitia sanaa mwanafunzi hujifunza kueleza mawazo yake na kuboresha ustadi wa mikono wakati wa michezo na huwfundisha ushirikiano na ujasiri. Kwa pamoja mbinu hizi hufanya ujifunzaji kuwa wa furaha na kuwawezesha wanafunzi kushirikiana vizuri na wenzao katika ufundishaji na ujifunzaji.



## Kazi ya kufanya 6.2

1. Andaa hadithi fupi inayohusu chakula na lishe kisha ongoza wanafunzi katika shule ya msingi jirani na chuo chako na kwa kutumia hadithi hii uliza maswali yafuatayo:
  - (a) Nini umejifunza kutockana na hadithi hii?
  - (b) Taja faida za vyakula vilivyotajwa kwenye hadithi hii.



2. Andaa kazi ya ujifunzaji inayohusisha sanaa na michezo katika kukuza ujenzi wa umahiri kwa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi na elimu maalumu. Kisha weka kwenye mkoba wako wa kazi.
3. Andaa somo la kufundisha kwa kipindi cha dakika 20 kwa ajili ya kuwasilisha umahiri mahususi katika darasa la elimu awali au dakika 40 kwa elimu msingi katika somo chaguzi.

### Zoezi la 6.2

1. Umepelekwa kwenye mafunzo ya ualimu kwa vitendo kufundisha darasa la awali. Umepanga kutumia igizo ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanashiriki na wanachangamka bila kujali tofauti zao za ujifunzaji.
  - (a) Eleza mikakati utakayoitumia ili kuhakikisha wanafunzi wanashiriki kikamilifu na wanajifunza kwa usawa kupitia igizo hilo.
  - (b) Taja faida za kutumia igizo katika ufundishaji wako.
2. Eleza namna michoro na picha za watoto zinavyohusiana na shughuli wanazopenda nyumbani na eleza zinavyoweza kumsaidia mwalimu kuelewa mahitaji ya wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji.
3. Bainisha aina za michezo ambazo zinawezesha ujenzi wa umahiri wa lugha kwa wanafunzi katika elimu ya awali, msingi na elimu maalumu.

### Ufundishaji na ujifunzaji katika darasa kubwa na jumuishi

Darasa kubwa na jumuishi linaundwa na idadi ya wanafunzi wenye mahitaji tofauti ya ujifunzaji. Katika madarasa makubwa, walimu wanatakiwa kutumia mbinu shirkishi ili kuwezesha wanafunzi wote kupata fursa ya kujifunza kwa ufanisi na usawa. Ujumuishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika madarasa ya kawaida unahitaji matumizi ya vifaa saidizi, teknolojia, na mbinu zinazozingatia mahitaji ya wanafunzi.



**Kazi ya kufanya 6.3**

1. Andaa na fundisha kipindi cha mfano kwa dakika 20 kwa watoto wa elimu ya awali na dakika 40 kwa wanafunzi wa elimu ya msingi katika shule iliyopo karibu na chuo chako. Kisha andika taarifa ya namna somo ilivyofanyika ukiibua mafanikio na maeneo ya uboreshaji.
2. Andaa na fundisha kipindi cha dakika 20 au 40 katika darasa jumuishi kuhusu umahiri mahususi utakaouchagua chini ya uangalizi wa mkufunzi. Bainisha mbinu utakazotumia katika somo na onesha namna zitakavyowezesha kuwafikia watoto wenye mahitaji maalumu darasani.
3. (a) Kwa kuzingatia mbinu na zana za kufundishia na kujifunzia; andaa na fundisha kipindi cha dakika 20 au 40 kwa wanafunzi wa elimu ya awali au msingi chini ya uangalizi wa mwaliimu mzoefu katika shule iliyopo karibu na chuo chako.  
(b) Andika taarifa ya tathimini ya somo na mrejesho uliopewa na mwaliimu mzoefu kisha weka taarifa yako kwenye mkoba wa kazi.
4. Buni mpango wa somo unaojumuisha matumizi ya teknolojia na vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Katika mpango huo eleza namna utakavyotumia michezo na sanaa ili kuongeza ushirikiano katika ujifunzaji. Weka mpango huo kwenye mkoba wako wa kazi.

**Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji**

Masuala mtambuka yanajumuisha mambo mbalimbali kama tamaduni, usawa wa kijinsia, matumizi ya teknolojia na vifaa saidizi, mazingira, afya, mabadiliko ya tabia nchi, ujumuishi katika elimu, ulinzi na usalama na elimu ya fedha. Matumizi ya TEHAMA, mbinu za ufundishaji, zana na vifaa hutumika kuwasilisha masuala mtambuka wakati wa ujifunzaji hivyo kuwawezesha wanafunzi kujenga uelewa wa kina na uwezo wa kukabiliana na changamoto za dunia ya sasa.

**Kazi ya kufanya 6.4**

1. (a) Chagua umahiri mahususi kutoka katika muhtasari wa somo lako chaguzi, andaa na fundisha kipindi cha dakika 20 kwa wanafunzi wa elimu ya awali au dakika 40 kwa wanafunzi wa elimu ya msingi katika shule ya jirani na chuo chako.



- (b) Bainisha namna ulivyoweza kuchopeka masuala mtambuka wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.
- (c) Andika taarifa ya mambo muhimu yaliyozingatiwa wakati wa kuchopeka masuaka hayo mtambuka.
- (d) Fafanua changamoto ulizokutana nazo katika kuchopeka masuala mtambuka katika somo lako.
2. Kwa kutumia maktaba ya chuongi kwako na vyanzo rasmi nya taarifa mtandaoni, andaa wasilisho la dakika 20 kuhusu namna mahitaji ya mwanafunzi yanavyoathiri uchaguzi wa zana za kufundishia na kujifunzia. Weka kwenye mkoba wako wa kazi.



## Zoezi la 6.3

- Unafundisha somo la Historia ya Tanzania na Maadili Darasa la Tatu, wakati wa kujadili haki za binadamu mwanafunzi mmoja anatoa hoja kwamba kazi za nyumbani ni za wanawake tu. Fafanua namna utakavyomsaidia mwanafunzi huyo kujenga mwelekeo chanya juu ya usawa wakijinsia.
- Katika shule moja, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wanafunzi wa kike kubusu ukosefu wa vifaa na unyanyapaa wanaokumbana nao wakati wa hedhi. Shule imeanzisha kampeni ya kuellimisha wanafunzi wote kuhusu maswala ya afya ya uzazi na usawa wa kijinsia. Eleza namna kampeni hii inaweza kusaidia kuboresha ujifunzaji kwa wanafunzi wa kike.
- Kama Mdhibiti Ubora wa shule, katika shule unazokagua umekutana na changamoto ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu kutopata msaada wa kutosha katika ufundishaji na ujifunzaji. Eleza hatua utakazochukua ili kuhakikisha upatikanaji wa elimu jumuishi kwa wanafunzi wote.





### Zoezi la marudio |||

1. Eleza namna teknolojia inavyoweza kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika darasa kubwa na jumuishi.
2. Bainisha namna mwali mu anavyoweza kutathimini ufanisi wa teknolojia na vifaa saidizi vya ufundishaji na ujifunzaji.
3. Tumia maktaba iliyopo chuoni kwako na vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni fafanua dhana ya darasa kubwa na jumuishi.
4. Chambua changamoto mwali mu anazowenza kukutana nazo wakati wa kufundisha darasa jumuishi.
5. Eleza namna ambavyo sanaa na michezo inaweza kuboresha mahusiano katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
6. Pendekeza mikakati inayoweza kutumika kuhakikisha kuwa mbinu za ufundishaji zinazingatia darasa jumuishi.
7. Unaufundisha somo la Sayansi katika elimu ya msingi ambapo kuna umahiri kuhusu afya ya uzazi. Mwanafunzi mmoja anaonekana kuwa na aibu na kuomba majadiliano nje ya darasa. Toa mapendekezo yako juu ya namna utakavyomsaidia mwanafunzi huyo
8. Eleza mikakati unayoweza kutumia ili kuhakikisha shughuli za michezo na sanaa zinahusisha masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji.
9. Bainisha faida za kutumia nyimbo, ngonjera, na mashairi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.



Sura ya  
Saba

## Ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa

### Utangulizi

*Ujifunzaji nje ya darasa huongeza ujuzi wa kitaaluma na kuchangia maendeleo ya ukuaji wa wanafunzi kiakili, kimwili, kihisia na kijamii. Vile vile huwasaidia wanafunzi kujenga uhusiano thabiti kati ya nadharia walizojifunza darasani na mazingira halisi wanayokutana nayo kila siku. Katika sura hii utajifunza dhama ya ujifunzaji nje ya darasa, mambo ya kuzingatia wakati wa kupanga shughuli za kufanya nje ya darasa na kutathmini utekelezaji wa ujifunzaji nje ya darasa. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kubuni na kusimamia shughuli za ujifunzaji nje ya darasa.*



### Fikiri

Shughuli za ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa

### Dhama ya ujifunzaji nje ya darasa

Shughuli za ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa ni mbinu zinazohusisha wanafunzi kujifunza kwa vitendo katika mazingira halisi. Shughuli hizi zinaweza kufanya kama maeneo kama vile kwenye bustani, maeneo ya kihistoria, warsha za vitendo, shughuli za kijamii, viwandani, maeneo ya sanaa, au hata katikajamii kwa ujumla. Lengo la shughuli hizi ni kuwajengea wanafunzi uzoefu wa moja kwa moja na wa vitendo.



### Kazi ya kufanya 7.1

- Wakati wa mafunzo kwa vitendo umepewa jukumu la kuandaa mkakati wa usimamizi wa shughuli za ujifunzaji nje ya darasa kwa muhula wa kwanza. Tekelceza shughuli hii na weka taarifa kwenye mkoba wako wa kazi.





2. Katika shule uliyoenda kufanya mafunzo ya ualimu kwa vitendo, umepewa jukumu la kushirikiana na mwalimu wa taaluma kuandaa ratiba ya ufundishaji na ujifunzaji.
- Eleza namna utavyojumuisha shughuli za ujifunzaji nje ya darasa katika ratiba hiyo.
  - Bainisha changamoto unazoweza kukutana nazo katika kujumuisha shughuli hizo kwenye ratiba ya shule.

Andika taarifa na weka kwenye mkoba wako wa kazi.



### Zoezi la 7.1

- Bainisha faida ambazo mwanafunzi anaweza kupata kwa kujihusisha na ujifunzaji nje ya darasa.
- Eleza namna mwalimu anavyoweza kutumia teknolojia kuboresha shughuli za ujifunzaji nje ya darasa.
  - Toa mifano ya teknolojia zinazoweza kutumika katikka kusimamia shughuli za nje ya darasa na uoneshe namna zinavyoweza kuongeza ufanisi wa ujifunzaji.
- Eleza namna mwalimu anavyoweza kubaini mahitaji ya wanafunzi kabla ya kupanga shughuli za ujifunzaji nje ya darasa.
- Endapo kutakuwa na upungufu wa muda kwa ajili ya kutekeleza shughuli za ujifunzaji nje ya darasa, mwalimu anaweza kutumia mbinu gani kuhakikisha kuwa shughuli za nje ya darasa zinafanyika kwa ufanisi bila kuathiri muda wa masomo ya darasani?

### Mambo ya kuzingatia wakati wa kupanga shughuli za ujifunzaji nje ya darasa

Mwalimu anapaswa kuzingatia mambo ya muhimu kabla ya kupanga shughuli za nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa shughuli hizo zinafanyika kwa wakati na kwa ufanisi. Mambo muhimu ya kuzingatia ni kama ifuatavyo:





**Umahiri wa ujifunzaji:** Kabla ya kupanga shughuli, ni muhimu kuelewa umahiri mahususi wa ujifunzaji unaotarajiwa kwa mwanafunzi. Shughuli za ujifunzaji nje ya darasa zinapaswa kuendana na mapendekezo yaliyopo kwenye muhtasari wa somo ili kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa, stadi na mwelekeo unaotarajiwa.

**Usalama wa wanafunzi:** Mwalimu anapaswa kuhakikisha mazingira ya ujifunzaji ni salama kwa kila mwanafunzi na kwamba kuwe na mipango madhubuti ya kusimamia wanafunzi, kama vile kuhakikisha kuna vifaa vya huduma ya kwanza na idadi ya kutosha ya walimu au wasimamizi.

**Rasilimali na vifaa:** Mwalimu anapaswa kuhakikisha kwamba kuna rasilimali na vifaa vya kutosha kwa ajili ya shughuli za ujifunzaji nje ya darasa. Hii inaweza kujumuisha vifaa vya kufundishia, chakula, maji, na usafiri wa kwenda na kurudi.

**Muda na ratiba:** Mwalimu anapaswa kupanga ratiba inayoendana na muda wa kujifunza. Shughuli haipaswi kuchukua muda mrefu na kusababisha mwingiliano wa ratiba ya masomo mengine au wanafunzi kuchoka.

**Mahitaji maalumu ya wanafunzi:** Mwalimu azingatie mahitaji maalumu ya wanafunzi, kama vile wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu au wenyewe magonjwa yanayohitaji uangalizi maalumu. Mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anaweza kushiriki kikamilifu katika shughuli zilizopangwa.

**Mazingira ya kujifunzia:** Mwalimu anapaswa kuchagua mazingira yanayofaa kulingana na umahiri na shughuli za ujifunzaji nje ya darasa. Kama umahiri mahususi ni kujifunza kuhusu mazingira, shughuli ifanyike katika mazingira halisi. Baadhi ya maeneo ambayo ujifunzaji nje ya darasa unaweza kufanyika ni kama vile; msituni, mtoni, bwawani, viwanjani, shambani, mabandani, mbuga za manyama, sokoni, taasisi za kifedha, hospitali, mahakamani na bungeni.

**Ushirikishwaji wa wazazi na walezi:** Ni muhimu kuwajulisha wazazi au walezi kuhusu shughuli za ujifunzaji nje ya darasa na kupata ruhusa yao ikiwa ni muhimu. Mwalimu awaeleze wazazi na walezi faida za wanafunzi kujihusisha katika utekelejaji wa shughuli za ujifunzaji nje ya darasa na hatua za usalama zilizowekwa.

**Matayarisho ya kabla:** Fanya matayarisho ya kabla, kama vile kuwaandaa wanafunzi kuhusu kile wanachotarajia kujifunza, utaratibu wa kufuata, na namna ya kujihusisha katika shughuli za ujifunzaji. Mwalimu anashauriwa kufanya ziara ya awali ya eneo husika ili kutathmini mazingira ya kujifunzia kabla ya shughuli halisi.





**Matumizi ya fedha:** Mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa kuna bajeti ya kutosha kwa ajili ya shughuli na kuwa matumizi yanaendana na kiasi cha fedha kilichopangwa. Ikiwa shughuli inahitaji ghamama za ziada kutoka kwa wazazi au walezi, basi ni vema kuwajulisha mapema.

**Tathmini ya shughuli:** Baada ya shughuli za ujifunzaji, ni muhimu kutathmini ili kuja kama umahiri uliotarajiwa umefikiwa. Hii inaweza kufanya kwa kuwataka wanafunzi washiriki katika mijadala, kuandika taarifa na kushirikisha uzoefu wao. Kielelezo 7.1 kinaonesha baadhi ya shughuli za ujifunzaji nje ya darasa.



Kielelezo 7.1: Baadhi ya shughuli za ujifunzaji nje ya darasa



### Kazi ya kufanya 7.2

Umepangwa kuongoza kundi la wanafunzi watakaofanya ziara ya kimasomo kwenye shule ya jirani, andaa mpango kazi, ratiba na utaratibu ukionyesha namna ya kusimamia na kutekeleza ziara hiyo. Kisha weka kwenye mkoba wako wa kazi.



## Zoezi la 7.2

1. Eleza umuhimu wa ujifunzaji nje ya darasa na toa mifano ya shughuli hizo katika somo lako chaguzi.
2. Eleza namna utakavyowasimamia wanafunzi wako wakati wa ujifunzaji nje ya darasa.
3. Shule yako imefanya ziara ya mafunzo kwa wanafunzi wa darasa la Saba. Pendekeza hatua unazoweza kuchukua ili kuhakikisha wanafuzi wote wanashiriki kikamilifu katika ziara za kimasomo.

**Tathmini ya ujifunzaji nje ya darasa**

Ujifunzaji nje ya darasa unapaswa kufanyiwa upinaji na tathmini ili kutoa mapendekezo ya kuboresha utekelezaji wa shughuli za ujifunzaji na kuhakikisha zinaendelea kuwa na manufaa katika mchakato wa ujifunzaji. Tathmini hii inaweza kutumia mbinu mbalimbali kama vile, kufanya uchunguzi, majadiliano, utafiti, mkoba wa kazi, mawasilisho, michezo ya kujifunza, taarifa ya kimaandishi, picha na video, kutumia orodha hakiki na ulinganishi wa matokeo ya kabla na baada.

**Vidokezo vya kuzingatia katika kufanya tathmini ya ujifunzaji nje ya darasa**

Wakati wa ujifunzaji nje ya darasa kuna vidokezo vinapaswa kuzingatiwa katika kufanya tathmini ili kuhakikisha kuwa uzoefu wa wanafunzi ni wa kufaa na unafanyaika kwa usalama. Vidokezo hivyo ni kama ifuatavyo:

**Umahiri wa ujifunzaji:** Mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa umahiri wa ujifunzaji unaendana na shughuli ya ujifunzaji nje ya darasa. Mbinu ya tathmini inayotumika izingatie umahiri mahususi uliopangwa katika somo husika.

**Ubunifu:** Katika kufanya tathmini ya shughuli za ujifunzaji nje ya darasa mwalimu anapaswa kuweka mkazo kwenye mbinu za ujifunzaji zinazochochea ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, mawasiliano na ujifunzaji binafsi.

**Ushirikiano:** Tathmini inapaswa kuhakikisha kuwa shughuli inatoa nafasi kwa wanafunzi kushirikiana na kuzungumza na wenzao, walimu, au wataalamu wa nje ili kuimarisha uelewa.

**Mchakato wa utekelezaji:** Mwalimu anapaswa kuzingatia mpango na ratiba ya shule, shughuli halisi za ujifunzaji nje ya darasa na matumizi sahihi ya rasilimali za ujifunzaji.



**Matokeo na maendeleo:** Tathmini inapaswa kutoa mrejesho kama shughuli ya ujifunzaji nje ya darasa inachangia maendeleo ya kiakili, kijamii na kihisia kwa wanafunzi.

**Rasilimali na ufadhilli:** Ujifunzaji nje ya darasa unapaswa kuzingatia rasilimali zilizopo shulenii au katika mazingira yanayoizunguka shule kama vile vifaa vya kujifunzia, fedha na miundo mbinu. Ufadhilli unawenza kuwa wa kifedha au vifaa kwa kuwahusisha wazazi, walezi na wadau wengi.

**Usalama na ustawi:** Tathmini za ujifunzaji nje ya darasa unapaswa kuzingatia uchunguzi wa namna ambavyo shughuli zinawezesha ustawi na usalama wa wanafunzi.

**Mfano wa orodha hakiki ya kutathmini shughuli za ujifunzaji nje ya darasa**  
 Kwa kutumia orodha hii mwalimu anaweza kutathmini ubora na ufanisi wa shughuli za ujifunzaji zinazofanywa nje ya darasa kwa kuhakikisha kwamba zinaongeza thamani katika ujifunzaji wa mwanafunzi.

Na.	Vigezo vya kuangalia	Kiwango cha ushiriki wa mwanafunzi			
		A	B	C	D
1.	Ushiriki wa mwanafunzi	✓			
2.	Umahiri uliojengwa		✓		
3.	Ubunifu katika ujifunzaji				✓
4.	Ushirikiano katika kazi			✓	
5.	Tathmini ya ubora wa kazi		✓		
6.	Ulinganisho wa shughuli na umahiri		✓		
7.	Mazingira ya kujifunzia	✓			
8.	Mwitikio wa mwanafunzi katika kazi	✓			
9.	Msaada na mwongozo wa mwalimu		✓		
10.	Uendelevu na ushiriki wa mara kwa mara			✓	

A ..... Vizuri sana

B ..... Vizuri

C ..... Wastani

D ..... Dhaifu





## Kazi ya kufanya 7.3

1. Kwa kutumia maktaba na vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni andaa mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia na vifaa saidizi katika kutathmini ujifunzaji nje ya darasa. Eleza kwa kina mifano ya teknolojia na vifaa hivi na namna vinavyoweza kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa kisha weka taarifa kwenye mkoba wako wa kazi.
2. Tembelea shule jirani na chuo chako na fanya tathmini kwa-kuchunguza namna shughuli za nje ya darasa zinavyotekelawa na ushiriki wa wanafunzi katika shughuli hizo. Fanya majadiliano na walimu na wanafunzi ili kupata maoni yao kuhusu ufanisi na changamoto wanazopitia.
3. Andaa zana utakayotumia kufanya tathmini ya ujifunzaji katika somo la michezo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Eleza umuhimu wa kutumia zana hiyo katika kufanya thathmini ya ujifunzaji nje ya darasa.



## Zoezi la 7.3

1. Bainisha namna ya kufanya tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa.
2. Fafanua namna matumizi ya programu za kompyuta au michezo ya ujifunzaji vinaweza kusaidia katika kutathmini uwezo wa watoto nje ya mazingira ya darasani.

**Zoezi la marudio**

1. Eleza namna shughuli za ujifunzaji nje ya darasa zinavyoweza kuimarisha uelewa wa wanafunzi kuhusu umahiri mahususi.
2. Katika kutathmi ushiriki wa wanafunzi ni vigezo vipi vitatumika kupima ufanisi wa shughuli nje ya darasa?
3. Eleza namna mbinu zinazotumika katika shughuli za nje ya darasa zinaweza kubadilishwa ili kukabiliana na changamoto zilizojoitokeza na kuongeza ufanisi wa shughuli kwa wanafunzi wenye mitindo tofauti ya ujifunzaji.
4. Bainisha namna tathmini ya shughuli za nje ya darasa inaweza kuathiri maamuzi ya mipango ya baadaye ya shule.
5. Katika tathmini ya shughuli za nje ya darasa umegundua kwamba baadhi ya vifaa vya ujifunzaji viliviyotumika havikutosha na vilisababisha changamoto kwa wanafunzi. Tathmini athari za ukosefu wa vifaa hivi na pendekeza mpango wa kuboresha shughuli za ujifunzaji nje ya darasa.
6. Kwa kutumia TEHAMA, bainisha namna unavyoweza kufanya tathmini isiyo na upendeleo kwa wanafunzi wakati wa ujifunzaji nje ya darasa.
7. Kama mwalimu wa taaluma, umegundua kuwa baadhi ya walimu wanachelewa kufika kazini na kutofundisha vipindi kwa wakati. Pendekeza hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kuondokana na changamoto hiyo na kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.
8. Changanua zana utakazozitumia kufanya tathmini ya ziara ya kimasomo na onesha namna utakavyowashirikisha wanafunzi.



Sura ya  
Nane

## Upimaji, tathmini na utoaji mrejesho wa ufundishaji na ujifunzaji

### Utangulizi

Upimaji na tathmini ni mchakato muhimu kwa maendeleo ya kitaaluma na huchangia katika kufanya maamuzi sahihi kuhusu mabadiliko ya mbinu, zana, na shughuli za ufundishaji na ujifunzaji. Katika sura hii, utajifunza kutumia mbinu na zana za upimaji ikiwemo TEHAMA kutathmini, kufuatilia, kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji na kutumia taarifa za matokeo ya upimaji katika kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Umahiri utakaonjenga utakuwezesha kutumia matokeo ya upimaji katika kufanya maamuzi mbalimbali ya ufundishaji na ujifunzaji.



Fikiri

Upimaji, tathmini na mrejesho katika ufundishaji na ujifunzaji

### Kutumia mbinu na zana za upimaji katika ufundishaji na ujifunzaji

Kwa kutumia mbinu, zana na vifaa sahihi mwalimu anaweza kuboresha ushiriki wa wanafunzi, kurahisisha ulewa wa dhana ngumu na kuhakikisha kwamba ujifunzaji wa somo unabaki kuwa wa kuvutia na wenye manufaa. Mbinu zinazowezza kutumika katika upimaji na tathmini wakati wa ufundishaji na ujifunzaji zinaweza kuhusisha upimaji wa utendaji, kazi mradi, upimaji endelevu, jaribio la kiutambuzi, maswali ya mdomo, majaribio ya msingi na vigezo vya utendaji. Vilevile, zana na vifaa kama vitabu, majarida, vifaa vya maabara, ramani, viclelezo, programu za kielimu, michoro, kadi za kazi, vifaa vya kuchezea vya kielimu, vikaragosi, mabango ya elimu, simulizi za kidigitali na vifaa vya kielektroniki vinawezza kutumika katika kuboresha ujifunzaji. Mbinu, zana na vifaa hivi hutumika kwa kuzingatia umri na mahitaji ya wanafunzi ili kuboresha ushiriki na kukuza umahiri.





## Kazi ya kufanya 8.1

- Kwa kuzingatia aina za upimaji, baini changamoto zinazowakabili wanafunzi katika mchakato wa ujifunzaji. Andika taarifa kueleza namna utakavyotumia aina za upimaji kutambua changamoto za wanafunzi katika ujifunzaji na uoneshe mikakati itakayowezesha kufanya maboresho. Kisha weka taarifa hii kwenye mkoba wa kazi.
- Tumia vyanzo rasmi nya taarifa mtandaoni kuhusu **zana qa** vifaa vinavyoweza kutumika kufanya tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji. Weka taarifa hiyo kwenye mkoba wako wa kazi.
- Tembelea shule ya msingi iliyopo karibu na chuo chako na fanya uchunguzi wa namna walimu wa elimu ya awali wanavyofanya upimaji na tathmini ya maendeleo ya ufundishaji na ujifunzaji. Andaa taarifa na weka taarifa hiyo kwenye mkoba wako wa kazi.



## Zoezi la 8.1

- Bainisha njia za upimaji unazoweza kutumia ili kufutilia maendeleo ya kitaaluma, kijamii na kihisia katika ufundishaji na ujifunzaji.
- Chunguza namna mwalimu anavyotumia upimaji wa maendeleo na tathmini ya jumla katika somo la Historia ya Tanzania na Maadili na eleza matokeo yanayotarajiwa kutoka kwa kila aina ya upimaji.
- Katika shule ya msingi Kigurunyembe, mwalimu wa Darasa la Tatu A hutoa mitihani mwishoni mwa muhula bila kuwapa wanafunzi majoribio au tathmini za mara kwa mara wakati huo mwalimu wa Darasa la Tatu B hutumia majoribio ya mara kwa mara kufutilia maendeleo ya wanafunzi. Mwisho wa muhula, wanafunzi wa Darasa la Tatu B wanafanya vizuri zaidi katika mitihani. Eleza umuhimu wa kufanya upimaji endelevu katika ufundishaji kwa kutumia mifano hii.
- Bainisha mbinu zinazoweza kutumika kutathmini maendeleo ya mwanafunzi katika maeneo tofauti ya ujifunzaji.



**Ufutiliaji wa maendeleo ya ujifunzaji**

Kufutilia maendeleo ya ujifunzaji kwa wanafunzi ni mchakato wa mara kwa mara unaohitaji mbinu maalumu kulingana na mahitaji na uwezo wa kila mwanafunzi. Katika ufutiliaji wa ujifunzaji kuna makundi matatu; elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu maalumu. Kwenye kipengele hiki utajifunza namna ya kufutilia maendeleo ya ujifunzaji kwa makundi yafuatayo:

**Ufutiliaji wa maendeleo ya ujifunzaji kwa watoto wa elimu ya awali**

Ufutiliaji wa maendeleo ya watoto wa elimu ya awali ni mchakato muhimu wa kufutilia na kutathmini ukuaji wa watoto wadogo katika vipengele mbalimbali vya maendeleo yao kama vile lugha na mawasiliano, kijamii, kihisia, kiutambuzi na ukuaji wa kimwili. Mchakato huu unahusisha matumizi ya mbinu na zana mbalimbali za ujifunzaji kama vile uchunguzi wa mwalimu, michezo, mahojiano ya wazazi au walezi na rekodi za maendeleo ya ujifunzaji. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila mtoto anapata msaada unaohitajika katika makuzi na kuwawezesha walimu na wazazi kuelewa mahitaji ya watoto na kuandaa mazingira bora ya ujifunzaji.

**Ufutiliaji wa maendeleo ya ujifunzaji kwa wanafunzi wa elimu ya msingi**

Wanafunzi wa elimu ya msingi wanapitia mabadiliko ya utambuzi, kihisia na kimwili na wanapaswa kufutiliwa kwa njia zinazowiana na malengo ya kielimu ya ngazi hiyo. Mchakato huu unahusisha matumizi ya mbinu na zana mbalimbali za ujifunzaji kama vile majaribio ya mara kwa mara, kazi mradi, vikao vya wanafunzi, rekodi za maendeleo, michezo na mahojiano ya wazazi au walezi. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata msaada unaohitajika katika makuzi na maendeleo ya kitaaluma. Vilevile huwawezesha walimu na wazazi kuelewa mahitaji ya wanafunzi katika kuboresha mazingira ya ujifunzaji.

**Ufutiliaji wa maendeleo ya ujifunzaji kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu**

Wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu wanahitaji mbinu za kufutilia maendeleo zinazozingatia mahitaji yao, uwezo na malengo binafsi. Mchakato huu unahusisha matumizi ya mbinu na zana mbalimbali za ujifunzaji zinazozingatia mahitaji maalumu ya kila mwanafunzi. Hii ni pamoja na mpango wa elimu maalumu, uchunguzi wa mara kwa mara, tathmini ya kazi halisi, vikao na timu ya mpango wa elimu maalumu na rekodi za maendeleo ya kila siku. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu anapata msaada unaohitajika ili kukuza na kuendeleza uwezo wake wa kujifunza. Aidha, huwawezesha walimu na wazazi kuelewa mahitaji maalumu ya wanafunzi, hivyo kuboresha mazingira ya ujifunzaji yanayokidhi mahitaji hayo.





## Kazi ya kufanya 8.2

1. Wewe ni mkuu wa idara ya Somo la Sayansi katika Shule ya Msingi Nyerere. Walimu wako wanakupa taarifa za matookeo ya tathmini ya ujifunzaji wa wanafunzi. Katika taarifa hiyo, umegundua kuwa baadhi ya masomo yanakosa tathmini ya taarifa endelevu zinazomuhusu mwanafunzi binafsi. Tafiti na kisha pendekezo mfumo wa ufuatiliaji unaoweza kutumika kuboresha mbinu za tathmini.
2. Tembelea shule ya msingi iliyo karibu na chuo chako, chunguza namna walimu wanavyofuatilia maendeleo ya ujifunzaji kwa watoto wa elimu ya awali. Bainisha mbinu za ufuatiliaji wanazozitumia na zinasaidiaje kuboresha ujifunzaji. Andika taarifa ya uchunguzi huo na weka kwenye mkoba wako wa kazi.



## Zoezi la 8.2

1. Eleza namna mbinu za upimaji zinazojumuisha shughuli za vikundi au kazi mradi zinaweza kuboresha tathmini ya ujifunzaji.
2. Eleza namna tathmini ya mazoezi ya mwanafunzi mmoja mmoja, kazi za nyumbani na kazi mradi zinaweza kutumika kufuatilia maendeleo ya ujifunzaji kwa wanafunzi wa rika tofauti.
3. Bainisha viashiria vya maendeleo ya ujifunzaji ambavyo vinaweza kufuatiliwa kwa kutumia teknolojia na vifaa saidizi.
4. Pafanua hatua unazoweza kuchukua ili kuhakikisha ufuatiliaji wa maendeleo ya ujifunzaji unafanyika kwa njia ambayo ni sahihi na yenye usawa.

**Kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi**

Mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi ni mchakato muhimu wa kuhakikisha kuwa mwanafunzi anapata maeleo ya kina kuhusu maendeleo katika ujifunzaji. Mrejesho huu unajumuisha kutoa tathmini ya utendaji wa mwanafunzi, kubainisha maeneo aliyofanya vizuri na yanayohitaji maboresho, na kutoa mapendekezo ya namna ya kuimarisha umahiri. Kwa kutoa mrejesho



wa mara kwa mara na wa kina, walimu wanaweza kusaidia wanafunzi kuelewa maendeleo yao, kuongeza motisha, na kurekebisha mikakati ya kujifunzi ili kufikia malengo ya ujifunzaji. Kutoa mrejesho kwa wanafunzi wa umri na wenye mahitaji tofauti ya ujifunzaji kunahitaji mbinu maalumu zinazokidhi mahitaji yao ya kipekee kama inavyofafanuliwa katika schemu zinazofuata.

#### **Watoto wa elimu ya awali**

**Urahisi na uelewa:** Mrejesho unapaswa kuelewaka kirahisi na mtoto, Mwalimu anapaswa kutumia lugha inayoelewaka kwa mtoto na mifano ya picha ili kuwawezesha kuelewa. Kwa mfano, "*Umeweka rangi nzuri sana kwenye picha yako! Unaweza kuongeza baadhi ya samaki ili kuonesha baharini.*"

**Kufurahisha na kujenga:** Tumia mbinu za kujenga na zinazowahamasisha watoto kupokea mrejesho. Mrejesho unapaswa kuwa chanya na kuonesha mafanikio yao. Kwa mfano, "*Nimefurahi sana kuona namna ulivyofanya shughuli hii. Endelea kufanya vizuri zaidi!*"

**Matumizi ya msaada wa vifaa:** Tumia vifaa nya msaada kama vile alama za picha au mifano ya kielelezo ili **kuonesha** maeneo ya kuboresha kwa njia rahisi. Kwa mfano, *leta picha au mchoro wa mfano, modeli, chati, video kuonesha watoto namna ya kuandika herufi.*

#### **Wanafunzi wa elimu ya msingi**

**Maelezo ya kina:** Mwalimu katika elimu ya msingi anapaswa kutoa mrejesho wa kina na unaowezesha kujifunza. Eleza kwa undani ni wapi mwanafunzi amefanya vizuri na ni wapi anahitaji kuboresha. Kwa mfano, "*Umeeleza vizuri kuhusu ukuaji wa mimea, lakini unaweza kuboresha kwa kuchora picha ya mmea kuonesha hatua za ukuaji.*"

**Mikakati ya kuboresha:** Mwalimu apendekeze mikakati ya vitendo kwa ajili ya kuboresha ujifunzaji. Eleza namna ya kutumia mbinu maalumu au kurekebisha makosa. Kwa mfano, "*Jaribu kufanya mazoezi zaidi ya kuandika kwa kutumia muundo wa hati ili kuongeza ufanisi wa uandishi wako.*"

**Tumia matokeo ya kazi za zamani:** Linganisha maendeleo ya sasa na yale ya zamani ili kuonesha maendeleo na mahali ambapo mwanafunzi anahitaji kuzingatia zaidi. Kwa mfano, "*Rejea masahihisho ya kazi ya juma lililopita kisha fanya marudio*"





### Wanafunzi wenge mahitaji maalumu

**Mrejesho binafsi :** Mwalimu anapotoa mrejesho azingatie mahitaji maalumu ya kila mwanafunzi. Tumia mbinu na vifaa saidizi vinavyoendana na mitindo yao ya kujifunza. Kwa mfano, *mwanafunzi mwenye ugumu katika kusoma anaweza kutumia programu za sauti ili kusaidia kuelewa mrejesho.*

**Mifano ya vielelezo na msaada wa ziada:** Tumia mifano ya kielelezo na msaada wa ziada kama vile picha na mbinu za mikono ili kuonesha namna ya kuboresha. Kwa mfano, *"Hii ni namna ya kupanga mawazo yako kwa kutumia picha na maandiko. Jaribu kufuata mfano huu ili kuboresha kazi yako."*

**Ushirikiano na wazazi na wataalamu:** Mwalimu ashirikiane na wazazi, walezi na wataalamu wa elimu maalumu ili kuhakikisha kuwa mrejesho unazingatia mahitaji ya kila mwanafunzi na unatoa msaada wa ziada unaohitajika. Vikao vya mara kwa mara na kuandaa mipango ya kutoa msaada binafsi kwa wanafunzi inaweza kuboresha utoaji wa mrejesho.



#### Kazi ya kufanya 8.3

1. Kama mwalimu umegundua kuwa mwanafunzi wako anajifunza kwa haraka ukilinganisha na wenzake darasani. Eleza hatua ambazo unaweza kuchukua ili kuunda impango wa ujifunzaji utakaolingana na kiwango cha mwanafunzi huyu huku ukihakikisha anapata msaada anaouhitaji.
2. Mwanafunzi katika darasa la sita anachangamoto ya uziwi, lakini shule hajjachukua hatua yoyote ya kuhakikisha anapata vifaa maalumu vya kumsaidia katika ujifunzaji darasani. Pendekeza mikakati inayoweza kumsaidia mwanafunzi huyu ili kuboresha ujifunzaji wake.



#### Zoezi la 8.3

1. Fanya tathmini ya maendeleo ya ujifunzaji kwa mwanafunzi na eleza vigezo unavyotumia kuamua wakati mzuri wa kutoa mrejesho ili kuimarisha ujifunzaji.
2. Eleza namna unavyoweza kutumia teknolojia kama vile majukwaa ya elimu mtandaoni katika kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji wa wanafunzi. Kisha bainisha faida na changamoto za kutumia teknolojia katika kutoa mrejesho.





3. (a) Bainisha mbinu zinazoweza kutumika kwa watoto wa awali, wafunzi wa elimu ya msingi na maalumu kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji.
- (b) Eleza namna mbinu hizi zinavyoweza kuimarisha uelewa wa maendeleo yao ya ujifunzaji.

#### Kutumia taarifa za matokeo ya upimaji katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji

Matokeo ya upimaji ni taarifa muhimu katika kuboresha utendaji wa mwanafunzi na mwalimu kwa kutoa taarifa sahihi ambazo zinaweza kutumika kufanya mabadiliko ya kimuundo, kuboresha mbinu za kufundisha na kuongeza ufanisi wa ujifunzaji. Matokeo ya upimaji yanaweza kutumika kuboresha utendaji wa mwanafunzi na mwalimu. Shughuli ya utoaji wa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi inajumuisha hatua zifuzatazo; kwanza kukusanya na kuchambua matokeo ya upimaji kama kazi za nyumbani, mitihani, na tathmini za darasani ili kubaini maeneo waliofanya vizuri na ya kuboresha. Pili, kutoa mrejesho wa kibinasi kwa mwanafunzi kwa kutumia lugha ya wazi na ya kuhamasisha, huku ukieleza maeneo yenye mafanikio na yale yanayohitaji kuboreshwa. Tatu, kutoa mapendekezo ya vitendo vya kuboresha, pamoja na kuweka malengo na mpango wa kazi. Nne, kufutilia maendeleo ya mwanafunzi na kurekebisha mipango kama inavyohitajika, ili kuhakikisha mwanafunzi anapata msaada wa kutosha na anafikia malengo yake ya kujifunza.

#### Kuboresha utendaji wa mwanafunzi

Mwalimu anaweza kutumia mrejesho kuboresha utendaji wa mwanafunzi kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

**Kuelewa maeneo ya uhitaji:** Matokeo ya upimaji yanasaidia kubaini maeneo ambayo mwanafunzi anakumbana na changamoto, kwa mfano, ikiwa mwanafunzi anapata alama ndogo katika sehemu fulani ya somo, inaweza kuonesha uelewa mdogo au mahitaji maalumu. Tathmini hii inasaidia mwalimu kuelewa wapi mwanafunzi anahitaji msaada zaidi na inaweza kutumika kuweka malengo ya kibinasi kwa mwanafunzi. Malengo haya yanapaswa kuwa halisia na yanaweweza kupimika, kama vile kuongeza alama kwa asilimia fulani au kuboresha uandishi wa insha. Hivyo, kwa kuweka malengo haya, mwanafunzi anapata mwongozo wa namna ya kuboresha utendaji wake na hatua zinazohitajika kufikia malengo hayo.



**Kuboresha mikakati ya kujifunza:** Matokeo ya upimaji yanamwezesha mwanafunzi kupanga mikakati maalumu ya kujifunza ili kuboresha maeneo anayohitaji kuimashwa, kama vile kazi za ziada, mazoezi maalumu, au msaada wa ziada kutoka kwa mwalimu. Mikakati hii hutoa msaada wa moja kwa moja kwa mwanafunzi ili kuboresha maeneo yenye changamoto. Aidha, matokeo hayo yanaweza kubainisha aina ya msaada wa ziada unaohitajika, kama vile masomo ya ziada au ushauri wa kitaaluma. Kwa mfano, mwanafunzi anayepata changamoto katika Hisabati anaweza kuhitaji vipindi nya ziada au ushauri ili kuboresha uelewa wake katika eneo hilo.

**Kutoa Mrejesho wa uboreshaji:** Matokeo ya upimaji yanapotoa mrejesho wa mara kwa mara na wa kina, mwanafunzi anaweza kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Mrejesho huu wa moja kwa moja unacleza namna ya kuboresha uelewa na utendaji, hivyo kumwezesha mwanafunzi kujua maeneo ya kuzingatia na hatua za kuboresha. Aidha, mwanafunzi anapata ufahamu wa maendeleo yake katika maeneo aliyopimwa, jambo linalomsaidia kujitambua na kufanya marekebisho yanayohitajika. Kwa kujua matokeo, mwanafunzi anaweza kujua maendeleo yake na kuweka mikakati ya kuboresha maeneo yenye changamoto.

#### **Kuboresha utendaji wa mwalimu**

Mrejesho wa ufundishaji na ujifunzaji unamwezesha mwalimu kuboresha utendaji wake kama ifuatavyo:

**Kurekebisha mbinu za kufundishia:** Matokeo ya upimaji yanaweza kusaidia mwalimu kutathmini ufanisi wa mbinu za kufundishia kwa kuangalia changamoto zinazowakumba wanafunzi katika maeneo ya ujifunzaji. Ikiwa matokeo yanaoncsha kuwa wanafunzi wanapata ugumu katika eneo fulani, mwalimu anaweza kuititia mbinu zilizotumika na kubaini kama ziliikuwa bora au zinahitaji marekebisho. Kwa mfano, kama wanafunzi wanapata ugumu katika dhana za Hisabati, mwalimu anaweza kupima kama mbinu zilizotumika ziliikuwa na ufanisi au zinahitaji kubadilishwa. Kwa kutumia matokeo haya, mwalimu anaweza kuboresha mbinu za kufundisha kwa kupanga mikakati mipy, kubadilisha mbinu za ufundishaji, kutumia mbinu mipy, au kuongeza shughuli zinazosaidia wanafunzi kuelewa vizuri zaidi katika maeneo yanayohitaji msaada.

**Kutoa msaada wa kitaaluma:** Matokeo ya upimaji yanaweza kuonesha maeneo ambapo mwalimu anahitaji kuboresha umahiri wake, na hivyo kuweza kutafuta mafunzo au ushauri wa kitaaluma ili kuboresha mbinu zake za kufundishia. Aidha, matokeo haya yanaweza pia kuonesha maeneo ambayo mwalimu anahitaji msaada wa ziada kutoka kwa wenzake au wataalamu wengine ili kutoa mbadala



wa mbinu za kufundishia zinazoweza kutumika na kusaidia mwalimu kutatua changamoto zinazojitekeza.

**Kuboresha mikakati ya kufundisha:** Mwalimu anaweza kutumia matokeo ya upimaji kuboresha mipango ya mafunzo kwa kupanga vipindi nya ziada, kubadilisha mbinu za kufundisha, au kuongeza rasilimali za kujifunzia kulingana na mahitaji ya wanafunzi. Mpango huu unapaswa kuwa endelevu kwa kuzingatia matokeo ya upimaji ili kuhakikisha unakidhi mahitaji ya wanafunzi. Aidha, ni muhimu kwa mwalimu kufuatilia maendeleo ya wanafunzi mara kwa mara ili kutathmini ufanisi wa mikakati ya kufundisha. Matokeo ya upimaji yanaweza kutoa taarifa muhimu kuhusu namna mikakati hii inavyofanya kazi na kutoa marekebisho yanayohitajika. Kwa mfano, taarifa hihi zinaweza kusaidia kubadilisha mipango ya somo ili kuongeza ufanisi wa mbinu za kufundisha.



#### Kazi ya kufanya 8.4

Wakati wa mafunzo ya ualimu kwa vitendo shulenii, tumia matokeo ya upimaji kubaini changamoto za wanafunzi katika ujifunzaji. Tengeneza mkakati wa kuboresha ufundishaji kwa kurekebishaa mbinu zako na kutoa msaada kwa wanafunzi wa awali, msingi na wenye mahitaji maalumu. Tathminni athari za marekebisho hayo kwa kuchunguza maendeleo ya wanafunzi na fanya marekebisho zaidi kila inapohitajika.



#### Zoezi la 8.4

1. Saru mwanafunzi wa darasa la tatu alikuwa na changamoto ya kuhesabu wakati wa ujifunzaji kwenye somo la Hisabati. Eleza namna unavyoweza kutoa afua stahiki kulingana na maendeleo ya mwanafunzi ili kufikia malengo yake ya ujifunzaji.
2. Eleza namna unavyoweza kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji unaowezesha kuratibu afua stahiki kwa wanafunzi wenye uwezo tofauti katika ujifunzaji.
3. Bainisha mbinu za kuwezesha ushirikiano wa wanafunzi, walimu, na wazazi au walezi ili kuboresha mpango binafsi wa ujifunzaji.

## Zoezi la marudio

1. Bainisha mbinu za TEHAMA unazoweza kutumia kutathmini maendeleo ya mwanafunzi katika ujifunzaji.
2. Fafanua namna zana za upimaji kama vile majoribio na tathmini za kielektroniki, zinavyoweza kutumika katika kufuatilia maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi.
3. Eleza namna mrejesho unaotolewa kwa mwanafunzi unavyochoea ujifunzaji.
4. Fafanua namna matokeo ya tathmini za TEHAMA yanavyoweza kubaini maeneo yenye changamoto kwa wanafunzi na kuyafanyia kazi.
5. Fafanua namna taarifa za matokeo ya upimaji zinavyoboresha mbinu za ufundishaji na kufanikisha malengo ya kitaaluma kwa wanafunzi.
6. Bainisha mbinu za usuutiliaji wa maendeleo ya mwanafunzi unazotumia kupata picha halisi ya maendeleo yake katika nyanja zote za ujifunzaji.
7. Chambua faida za usuutiliaji wa maendeleo ya ujifunzaji mara kwa mara katika kuboresha mbinu za ufundishaji ili kuendana na mahitaji ya kila mwanafunzi.
8. Eleza hatua unazoweza kuchukua baada ya kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi na kugundua kuwa hayafikii viwango vilivyotarajiwu.
9. Eleza namna mwalimu anavyotumia taarifa za matokeo ya upimaji kupanga mikakati mipyä ya ufundishaji na ujifunzaji ili kuhakikisha maendeleo bora ya wanafunzi.
10. Fafanua namna matumizi ya teknolojia yanavyowezza kuboresha utoaji wa afua stahiki na mpango binaffsi wa ujifunzaji. Toa misano ya zana za teknolojia ambazo unaweza kutumia ili kuongeza usanisi wa mpango huo.

Sura ya  
Tisa

## Ushauri na unasihi katika ufundishaji na ujifunzaji

### Utangulizi

Ushauri na unasihi katika ufundishaji na ujifunzaji ni kipengele muhimu katika kuhakikisha mwanafunzi anapata taaluma bora na maendeleo ya kisaikoloja. Ushauri na unasihi ukitekelezwa kwa ufanisi unaweza kuchangia na kuimarisha maendeleo ya kitaaluma na kujenga mahusiano bora kati ya mwanafunzi na mwaliimu na kumuandaa mwanafunzi kwa maisha baada ya shule. Katika sura hii utajifunza mikakati ya kubaini wanafunzi wenye mahitaji ya ushauri na unasihi katika ufundishaji na ujifunzaji. Utaweza kujifunza mambo yanayohitaji ushauri na unasihi kwa wanafunzi katika mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji na kutoa huduma ya ushauri na unasihi kwa mwanafunzi. Vilevile Utajifunza utoaji wa ushauri na unasihi kwa watoto wa elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu maalumu. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia ushauri na unasihi katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.



Fikiri

Ushauri na unasihi katika ufundishaji na ujifunzaji

### Kubaini wanafunzi wenye mahitaji ya ushauri na unasihi

Ubainishaji wa mwanafunzi mwenye mahitaji ya ushauri na unasihi katika ufundishaji na ujifunzaji unaweza kufanywa kwa kuzingatia dalili kama vile mabadiliko ya ghafla, kushuka kwa ufanisi wa masomo, utoro au uchelewaji wa mara kwa mara, mwanafunzi kujitenga na wenzake, msongo wa mawazo, huzuni au kupoteza ari ya ujifunzaji. Mwalimu au walimu wanapaswa kuwa makini na dalili hizi na kuchukua hatua za mapema za kuwasaidia wanafunzi.





## Kazi ya kufanya 9.1

Tembelea shule ya msingi ilio jirani na chuo chako na chunguza mbinu zinazotumika na walimu kubaini wanafunzi wenye mahitaji ya ushauri na unasihi katika ufundishaji na ujifunzaji. Andika taarifa kisha weka kwenye mkoba wako wa kazi.

Baadhi ya mikakati maalumu ambayo mwalimu anaweza kuitumia kubaini wanafunzi wenye uhitaji wa ushauri na unasihi katika ufundishaji na ujifunzaji ni pamoja na:

**Kufuatilia mwenendo wa kitaaluma:** Mwalimu anaweza kufuatilia alama za mitihani na majoribio mbalimbali ili kubaini wanafunzi wenye alama za chini au walioonesha kushuka kwa ghafla katika utendaji wao. Mwalimu wa somo pia anaweza kufanya ufuatiliaji wa ufanisi wa kazi za darasani na za nyumbani.

**Kufuatilia mahudhurio:** Wanafunzi wanaokosa masomo na wanaochelewa mara kwa mara ni viashiria vya tatizo, hivyo mwalimu anapaswa kufuatilia tabia hiyo ili kugundua visababishi vyake na kupendekeza namna ya kutatua.

**Ushiriki darasani:** Wanafunzi ambao hawaonekani kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani kama vile kutochuchangia mijadala au kuwa wakimya kupita kiasi wanaweza kuwa wanapitia changamoto, hivyo wanahitaji kusaidiwa.

**Kutathmini tabla na nidhamu:** Mabadiliko ya ghafla ya tabia, kama vile kuwa mkimya sana, kuwa mkali au kuonesha hasira au huzuni ni ishara kwamba wanafunzi wanachangamoto na wanahitaji msaada. Wanafunzi wanaojihuisha na vitendo vya utovu wa nidhamu mara kwa mara wanahitaji msaada wa ushauri na unasihi.

**Kuangalia afya ya kiakili na kihisia:** Wanafunzi wanaonehesha dalili za msongo wa mawazo, wasiwas, au huzuni ni viashiria kwamba wanahitaji ushauri na unasihi. Vilevile, wanafunzi wanaopitia matatizo ya kifamilia kama vile talaka za wazazi, kutengwa na jamii, vifo, au matatizo ya kifedha wanaweza kuhitaji msaada wa ushauri na unasihi.

**Kuangalia mahusiano baina ya wanafunzi:** Mwalimu aangalie na kubaini wanafunzi wanaoneckana kutengwa, wasio na marafiki, wanaobaguliwa na





wenye mabadiliko ya ghafla katika uhusiano na wanafunzi wenzao, kama vile kuachana na marafiki wa karibu. Hii itasaidia kuwapatia msaada wa ushauri na unasihi kwa wakati.

**Uwasilishaji wa changamoto inayomkabili:** Wanafunzi wanaweza kujitokeza na kuomba msaada au kuelezea shida zao moja kwa moja kwa walimu au washauri wanaowaamini. Wanafunzi wenzao wanaweza kutoa taarifa au videokezo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji msaada ushauri na unasihi katika ujifunzaji.

**Ufuatiliaji wa mara kwa mara:** Vikao vya mara kwa mara kati ya walimu na wanafunzi vinaweza kusaidia kubaini matatizo yanayowakumba wanafunzi wao. Tathmini za mara kwa mara za kisaikolojia zinaweza kusaidia kugundua matatizo ya kiakili, kihisia na kijamii kwa wanafunzi na kutoa msaada stahiki.

**Kushirikiana na wazazi, walezi na wadau wengine:** Vikao vya mara kwa mara kati ya wazazi, walezi, walimu na wadau wengine vinawezesha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu matatizo ya wanafunzi ambayo yanaweza kuhitaji ushauri na unasihi. Mawasiliano kati ya wazazi, walezi na walimu yanaweza pia kusaidia kubaini matatizo yanayowakumba wanafunzi nyumbani na shulenii na hivyo kuweka mikakati ya kutoa msaada kulingana na mahitaji hayo.



### Kazi ya kufanya 9.2

Andaa dodoso kwa wanafunzi wa Darasa la Sita kuhusu hali yao ya kihisia na kitaaluma inayokwamisha mchakato wa ujifunzaji. Tumia dodoso hilo kukusanya taarifa kutoka katika shule ya msingi jirani na chuo chako kisha, changanua na andika taarifa kuhusu matokeo ya uchunguzi na weka kwenvye mkoba wako wa kazi.



### Zoezi la 9.1

1. Katika mgwanyo mpya wa vipindi shulenii kwako, umepangwa kufundisha darasa lenye watoto wenye mahitaji maalumu; eleza kwa kina namna za kuwabaini na kuwasaidia watoto wenye changamoto zifuatazo:

*Uoni hafifu; usonji; ufaulu duni; utoro; ulemavu wa viungo na mabadiliko ya kimaumbile au balehe.*





2. Wanafunzi wa darasa la awali wanahitaji mazingira tofauti na wanafunzi wa madarasa ya juu wakati wa ushauri na unasihi. Fafanua
3. Eleza namna mawasiliano kati ya wazazi, walezi na walimu yanaweza kusaidia kubaini wanafunzi wenye uhitaji wa ushauri na unasihi.

### Mambo yanayohitaji ushauri na unasihi kwa wanafunzi

Ushauri na unasihi kwa wanafunzi katika elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu maalumu ni muhimu katika kuhakikisha wanapatu msaada unaohitajika ili kukua vyema, kuboresha taaluma, na kujenga ustawi wa kifakili, kihisia, na kijamii. Mahitaji ya ushauri na unasihi yanatofautiana kulingana na umri, hatua ya maendeleo, na hali zao maalumu, kama vile changamoto za kijamii, kisaikolojia, au za kitaaluma. Kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, ushauri unalenga zaidi kusaidia kupata huduma zinazolingana na mahitaji yao. Ushauri na unasihi shuleni husaidia kujenga mazingira jumuishi yanayowezesha kila mwanafunzi kufanikiwa kitaaluma, kihisia na kijamii kwa kuzingatia umri na uwezo wa wanafunzi kama ifuatavyo:

#### Elimu ya awali

**Mabadiliko ya mazingira:** Watoto wanapoanza shule, wanakutana na mazingira mapya ambayo yanaweza kuwa magumu kwao. Ushauri unasaidia kuwaongoza kujenga ujasiri na kukabiliana na mabadiliko haya.

**Kujifunza stadi za kimsingi:** Watoto wa elimu ya awali wanahitaji msaada wa kuendeleza stadi za kijamii, kama vile kushirikiana na wenzao, kujali, mawasiliano, kusadiana, kujiari, kutunza vifaa na mazingira, na kufuata maelekezo.

**Nidhamu au tabia:** Mshauri wa unasihi husaidia katika kukuza tabia nzuri kwa watoto kama vile heshima, utii, kujali muda na kushughulikia hisia zao kwa njia inayofaa.

**Kutojitambua:** Katika hatua hii, watoto huanza kutambua tofauti zao na wengine. Ushauri unawasaidia kuelewa na kukubali tofauti hizi kwa kuimarisha kujiamini.

#### Elimu maalumu

**Kutojitambua na kujikubali:** Watoto wenye mahitaji maalumu mara nyingi wanahitaji msaada wa kipekee ili kujitambua na kujikubali. Unasihi unasaidia watoto hawa na familia zao kukabiliana na changamoto za kimaisha na kitaaluma.

**Mpango wa mafunzo ya kipekee:** Ushauri unahuishwa maendeleo ya mpango binafsi wa ujifunzaji ambao unaangazia mahitaji maalumu ya kila mwanafunzi na kufuutilia maendeleo yake kitaaluma na kimaisha.



**Kukuza ustadi wa kijamii:** Wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanahitaji msaada wa ziada katika kukuza stadi za kijamii na namna ya kuhusiana na wengine kwa usanisi.

**Msongo wa mawazo:** Unasihi unahitajika kusaidia wanafunzi kukabiliana na msongo wa mawazo unaoweza kutoptana na hali yao ya kipekee au changamoto za kijamii wanazokutana nazo.

#### Elimu kwa wanafunzi wa kawaida

**Masuala ya kitaaluma:** Wanafunzi katika elimu ya kawaida wanakabiliwa na mitihani, mahitaji ya masomo, na matarajio ya wazazi. Ushauri unasaadidhika katika kudhibiti shinikizo hili kwa kuwasaidia wanafunzi kupanga ratiba zao na kuweka malengo yanayoweza kufikiwa.

**Masuala ya kijamii:** Ushauri unahitajika kusaidia wanafunzi kushughulikia changamoto za kijamii kama vile urafiki, uonevu, kutengwa na unyanyapaa.

**Masuala ya familia:** Wanafunzi wanaweza kukumbana na changamoto nyumbani kama vile migogoro ya kifamilia au matatizo ya kiuchumi ambayo yanaweza kuathiri utendaji wao shulenii. Ushauri na nasihii husaidia katika kutatua masuala haya kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi.

**Kutojiamini na kutojitambua:** Ushauri unahitajika ili kuwasaidia wanafunzi kujenga kujiamini, kujitambua kihisia na kiuwezo katika mazingira ya ujifunzaji.



#### Kazi ya kufanya 9.3

1. Tembelea darasa la awali katika shule ya msingi iliyopo jirani na chuo chako na bainisha changamoto mbalimbali zinazowakabili wanafunzi katika ujifunzaji, na toa mapendekezo ya namna bora ya kutumia ushauri na unasihi katika kutatua changamoto hizo.
2. Katika mafunzo yako ya ualimu kwa vitendo, tumia mbinu ya uchunguzi kubaini mahitaji ya ushauri na unasihi kwa wanafunzi wako. Andaa taarifa, kisha weka kwenye mkoba wako wa kazi.
3. (a) Wakati wa mafunzo yako ya ualimu kwa vitendo, andaa mpango kazi na utumie kutoa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wenye changamoto za ujifunzaji.  
 (b) Andaa taarifa ya utekclezaji wa mpango huo, kisha weka kwenye mkoba wako wa kazi.





Zoezi la 9.2

1. Wewe ni mwalimu katika shule ya msingi na umeona mabadiliko ya ghafla ya kitabia kwa mwanafunzi wako wa Darasa la Nne ambaye hapo awali alikuwa mchangamfu na anayejiamini. Eleza namna utakavyomsaidia mwanafunzi huyo kuboresha ujifunzaji wake.
2. Eleza namna tathmini za mara kwa mara mara zinavyomwezesha mwalimu kumsaidia mwanafunzi mwenye tabia za kujitenga na kushindwa kufuata maelekezo darasani.
3. Bainisha mbinu uakazotumia kuwatambua wanafunzi wanaokumbana na changamoto za kifamilia na pendekeza mikakati unayoweza kutumia kuwasaidia.
4. Shule yako inamchanganyiko wa wanafunzi wa elimu awali, kawaida na wenge mahitaji maalumu. Katika uchunguzi wako umegundua kuwa wanafunzi wenge mahitaji maalumu wana changamoto katika kuhusiana na wenzao. Onesha namna utakavyowsaidia.

*Kutoa huduma ya ushauri na unasihi kwa mwanafunzi*

Utoaji wa huduma ya ushauri kwa mwanafunzi kuhusu masomo na maisha ya kazi ni wa muhimu katika kumsaidia kufikia malengo yake (angalia Kielelezo 9.1). Mwalimu atahakikisha anamsaidia mwanafunzi kubaini malengo yake, kupanga vizuri muda wa masomo na kutambua fursa za kitaaluma. Vilevile, atamwelimisha namna elimu inavyoweza kutumika katika ulimwengu wa kazi na kumpa mwongozo kuhusu usimamizi wa muda, kupambana na msongo wa mawazo na maadili ya kazi. Hii itamsaidia kuwa na mtazamo mzuri na uwezo wa kujipanga kwa ajili ya maisha ya baadaye. Utoaji wa huduma hii unategemeana na kundi la wanafunzi:

102





Kielelezo 9.1: Ushauri na unasihi

#### Utoaji wa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wa elimu ya awali

Huduma ya ushauri na unasihi kwa watoto wa elimu ya awali inapaswa kuwa rahisi, yenye kuvutia, na inayozingatia maendeleo ya kiakili, kihisia na kijamii. Watoto wa elimu ya awali wanaweza kufaidika na huduma ya ushauri na unasihi kwa kuhusisha wazazi, walezi na walimu ili kuwajengea mazingira salama ya kujifunza. Michezo na mazungumzo inaweza kutumika kuwafanya watoto wajiamini, wakuze uwezo wa kijamii na kihisia na kujenga tabia njema wakiwa shulenii na nyumbani.



#### Kazi ya kufanya 9.4

Andaa programu wezeshi ya mafunzo juu ya ushauri na unasihi kwa watoto wa elimu ya awali kwa ajili ya wazazi na wadau wengine wa elimu. Katika wasilisho lako, zingatia namna ya kubaini, mbinu, umuhimu na changamoto za kutoa ushauri na unasihi. Kisha weka kwenye mkoba wako wa kazi.

**Utoaji wa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wa elimu maalumu**

Ushauri na unasihi kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalumu lazima uzingatие mahitaji yao ya kipekee na kutoa msaada binafsi. Utoaji wa huduma hii, ni muhimu kuanza kwa kubaini mahitaji yao na mazingira wanayokutana nayo katika maisha ya kila siku. Hili ni jambo la muhimu katika kusaidia kujenga ushirikiano mzuri kati ya wazazi, walezi, walimu na wataalamu wa afya ili kutoa msaada stahiki. Msaada wa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalumu unajikita katika kuwajengea kujitambua, kujamini na kukuza stadi za kijamii.



Kazi ya kufanya 9.5

Tembelea maktaba na vyanzo rasmi vya taarifa mtandaoni kupata taarifa muhimu zitakazokuwezesha kuandaa mpango wa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalumu. Kisha, mshirikishe mkufunzi wako kwa majadilino, fanya maboresho na weka kwenye mkoba wako wa kazi.

**Utoaji wa ushauri na unašihi kwa wanafunzi wa elimu ya msingi**

Ushauri na unasihi kwa wanafunzi wa elimu ya msingi ni hatua muhimu ya kuwaongoza na kuwasaidi watoto katika ukuaji wao kiakili, kihisia, kimwili, na kijamii. Katika kipindi hiki wanafunzi wanakutana na changamoto zinazohusiana na masomo, uhusiano wa kijamii na mazingira ya kujifunzia. Kutoa ushauri na unasihi kunawawezesha watoto kushughulikia matatizo na kujijengea uwezo wa kujitambua na kufanya maamuzi yaliyo sahihi. Mwalimu anajukumu la kuhakikisha kwamba wanafunzi wanapata msaada wa kitaalamu ulio rafiki ambao unawaongoza katika maendeleo yao ya kielimu na kijamii. Mwalimu anapaswa kushirikisha wazazi na walezi katika mchakato wa ushauri na unasihi kwa kuwapa taarifa kuhusu maendeleo ya watoto wao na mbinu za kuwasaidia katika mazingira ya nyumbani.





## Kazi ya kufanya 9.6

1. Kwa kuzingatia kanuni za unasihi ulizojifunza, tembelea shule ya msingi jirani na chuo chako na baini changamoto zinazowakumba wanafunzi. Zigawanye changamoto hizi katika makundi kulingana na mahitaji na mazingira ya ujifunzaji. Andika namna utakavyoweza kuwasaidia walimu kutoa huduma ya ushauri na unasihi kwa wanafunzi wao.
2. Fanya utafiti kuhusu changamoto zinazojitekeza katika utoaji wa ushauri na unasihi kwa wanafunzi katika masuala ya kijamii, kimasomo, kimaadili, kimwili na kiakili. Baada ya utafiti andika taarifa inayojadili changamoto na toa mapendekezo ya namna ya kuzitatau kisha weka taarifa kwenye mkoba wako wa kazi.
3. Andaa mafunzo maalumu kwa ajili ya kuwaelekeza wanachuo wenzako namna ya kutoa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wa darasa la sita juu ya mabadiliko ya kimwili wanayopitia na namna ya kuyapokea. Fanya wasilisho na andika taarifa kuhusu mafunzo hayo na weka kwenye mkoba wako wa kazi.



## Zoezi la 9.3

1. Eleza namna ushauri na unasihi unaweza kusaidia watoto wa elimu ya awali kuimarisha uwezo wao wa kujifunza.
2. Angela anachangamoto kubwa katika kufanya kazi za vikundi, mara nyingi anahisi qibu. Kama mshauri, bainisha namna utakavyotoa ushauri na unasihi ili kumsaidia kuboresha uhusiano wake na wenzake katika ujifunzaji.
3. Juma ana malengo ya kuwa mhandisi lakini anapata changamoto katika ujifunzaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati. Kama mwalimu, safanua namna ushauri na unasihi utasaidia kuboresha umahiri wake katika masomo hayo na kutimiza malengo yake.
4. Katika darasa lako kuna mwanafunzi mwenye hasira na mara nyingi anakuwa na migogoro na walimu na wanafunzi wenzake. Kama mshauri, eleza mbinu unazoweza kutumia kumsaidia aweze kujifunza na kudhibiti hisia zake.
5. Mwanafunzi wa Darasa la Tatu anapata ugumu katika kupanga muda wake kati ya masomo, michezo na majukumu ya nyumbani. Kama mwalimu, eleza namna utakavyomsaidia mwanafunzi huyu kumudu ratiba yake.



### Zoezi la marudio |||

1. Eleza hatua utakazochukua ili kubaini mahitaji maalumu ya ushauri na unasihi kwa mwanafunzi katika mazingira ya shule.
2. Walimu na wazazi wanashindwa kutofautisha kati ya ushauri na unasihi. Wewe kama mtaalamu, toa usafanuzi kwa kutumia mazingira ya ujifunzaji.
3. Eleza namna utoaji wa ushauri na unasihi unawezesha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
4. Chambua hatua unazoweza kuchukua ili kumsaidia mwanafunzi anayepitia changamoto za kijamii kama vile migogoro na marafiki au kutengwa.
5. Kama mwalimu, bainisha changamoto unazoweza kukutana nazo wakati wa kutoa ushauri na unasihi kwa wanafunzi.
6. Eleza msaada unaowenza kutolewa na jamii ya shule ili kuboresha utoaji wa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
7. Umeandaa mpango kazi wa wiki wa kutoa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wako. Lakini kutokana na wingi wa majukumu shulenii unashindwa kutekeleza kwa ufanisi mpango huo. Eleza namna utakavyotumia teknolojia kutekeleza mpango huo.
8. Eleza namna utakavyoshirikiana na wanafunzi wenye mahitaji maalumu ili kubaini na kutatua changamoto wanazokutana nazo katika ufundishaji na ujifunzaji.
9. Bainisha juhudini za pamoja za wanafunzi, walimu, na wazazi zinazoweza kuchukuliwa ili kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanapata fursa sawa katika ujifunzaji.



**Faharasa**

<i>Changamshi</i>	vitendo vinavyoleta furaha na kuburudisha katika mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji
<i>Hisia</i>	hali ya ndani ya kiakili inayojitokeza kutokana na matukio mbalimbali
<i>Jumuishi</i>	hali ya kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi katika ujifunzaji
<i>Kivunge</i>	jumla ya zana zinazofunganywa pamoja na kwenye begi au boksi na kutumiwa kwa lengo maalumu
<i>Kona za ujifunzaji</i>	mpangilio wa zana au vifaa vya kujifunzia darasani kwa kuzingatia umahiri au somo
<i>Kufaragua</i>	hali ya kutumia vitu vinavyopatikana katika mazingira kusidia vitu visivyopatikana
<i>Makunzi</i>	vitu vinavyoweza kutumika kutengeneza zana za ufundishaji na ujifunzaji
<i>Motisha</i>	hali ya kuhamasisha mtu kufanya jambo fulani kwa shauku, bidii na nia dhabiti
<i>Mjongo</i>	hali ya ujifunzaji inayohusisha kuhama kutoka sehemu moja ya darasa kwenda nyingine
<i>Msimbo</i>	kuweka alama za utambuzi wakati wa kuhifadhi zana za kufundishia na kujifunzia
<i>Msongo</i>	hali ya uchovu au wasiwasi inayompata mtu baada ya kutingwa na mambo mengi akilini mwake
<i>Mtambuka</i>	mambo yanayohusu watu wote au pande zote





<b>Teknolojia</b>	matumizi ya maarifa ya kisayansi kwa ajili ya kubuni, kuunda, kuwasilisha na michakato inayosaidia kutatua changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji
<b>Unasihi</b>	msaada wa kitaalamu unatolewa juu ya tatizo fulani
<b>Usonji</b>	hali ya neva inayoahiri namna mwanafunzi anavyowasiliana, kufikiria na kushirikiana na wengine katika mazingira ya ujifunzaji
<b>Vifaa saidizi</b>	vifaa vya ufundishaji vinavyowezesha ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu
<b>Vipuri</b>	vifaa vya ziada vinavyoweza kutumika kwa ajili ya matengenezo au kurekebisha sehemu zilizoharibika
<b>Zana maono</b>	zana za ufundishaji zinazowezesha ujifunzaji kwa kuona
<b>Zana masikizi</b>	zana za ufundishaji zinazowezesha ujifunzaji kwa kušikiliza
<b>Zana mguso</b>	zana za ufundishaji zinazowezesha ujifunzaji kwa kugusa au kupapasa



**Bibliografia**

- American School Counselor Association. (2019). *The ASCA national model: A framework for school counseling programs* (4th ed.). Author.
- Arends, R. I. (2014). *Learning to Teach* (10th ed.). New York: McGraw-Hill Education.
- Black, P. & Wiliam, D. (1998). *Inside the black box: Raising standards through classroom assessment*. Phi Delta Kappan, 80(2), 139–148.
- Brown, A. & Green, T. D. (2022). *The essentials of instructional design: Connecting fundamental principles with process and practice* (4th ed.). Routledge.
- Children in Cross Fire. (2024). *Mwongozo wa Mwezeshaji Mafunzo ya Walimu Elimu ya Awali*. Dar es Salaam Tanzania.
- Chonjo, I. K. (2019). *Mbinu za Ufundishaji na Upinaji katika Elimu ya Sekondari Tanzania*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Cook, A. M. & Polgar, J. M. (2015). *Assistive Technologies: Principles and Practice* (4th ed.). St. Louis, MO: Mosby.
- Eggen, P. & Kauchak, D. (2013). *Educational Psychology: Windows on Classrooms* (9th ed.). Upper Saddle River, NJ: Pearson.
- Friend, M. & Cook, L. (2017). *Interactions: Collaboration skills for school professionals* (8<sup>th</sup> ed.). Pearson.
- Fuchs, D., & Fuchs, L. S. (2006). *Introduction to response to intervention: What, why, and how*. Teaching Exceptional Children, 39(1), 14–20.
- Johnson, R. T. (2020). *Effective classroom management and student guidance*. Routledge.
- Jones, C. S. (2018). *Workshop on effective group counseling techniques*. National Institute for Education.





Joyce, B., Weil, M., & Calhoun, E. (2015). *Models of Teaching (9th ed.)*. Boston: Pearson.

Kafyulilo, A. C., Fisser, P., & Voogt, J. (2016). Supporting teachers' collaboration in design teams to develop technological pedagogical content knowledge: A case of science teachers in Tanzania. *Journal of Education and Practice*, 7(7), 89-102.

Kapinga, O. S. (2017). *Changamoto za kufundisha madarasa yenyeye idadi kubwa ya wanafunzi katika shule za msingi Tanzania*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Komba, W. L. M., & Mwandanji, M. (2015). *Reflections on the implementation of competence-based curriculum in Tanzanian secondary schools*. Journal of Education and Learning, 4(2), 73-80. <https://doi.org/10.5539/jel.v4n2p73>

Msuya, O. E. (2016). *Integrating information and communication technology in English language teaching: A case study of selected secondary schools in Tanzania*. Journal of Education, Humanities and Sciences, 5(2), 1-15.

Mwita, J. R., & Mbwambo, A. H. (2018). *Psychological counselling in Tanzanian schools*, Theory and Practice, Mkuki na Nyota Publisher.

NECTA. (2023). *Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa Katika Mtihani wa Ualimu Daraja A (GATCE)*.

Nyabanya, M. O. (2014). *Mbinu za kufundisha katika madarasa yenyeye idadi kubwa ya wanafunzi: Kesi ya shule za msingi mkoa wa Mwanza*. Chuo Kikuu cha Dodoma.

Reiser, R. A., & Dempsey, J. V. (Eds.). (2017). *Trends and issues in instructional design and technology* (4th ed.). Pearson.

Salend, S. J. (2016). *Creating inclusive classrooms: Effective and reflective practices* (9th ed.). Pearson.

Schwab, K. (2016). *The Fourth Industrial Revolution*. New York: Crown Business.



Smith, J. A., & Brown, L. M. (2021). *Educational counseling and guidance: A practical approach*. Oxford University Press.

Taasisi ya Elimu ya Tanzania. (2016). *Mwongozo wa Walimu wa Shule za Msingi: Sayansi na Teknolojia*. Dar es Salaam: TIE.

Taasisi ya Elimu ya Tanzania. (2016). *Mwongozo wa Mitaala ya Elimu ya Sekondari*. Dar es Salaam: TIE.

Taasisi ya Elimu ya Tanzania. (2016). *Mwongozo wa Walimu wa Shule za Sekondari: Jiografia*. Dar es Salaam: TIE.

Taatgen, N. A., & Anderson, J. R. (2008). *The Past, Present, and Future of Cognitive Architectures*. Topics in Cognitive Science, 1(1), 15-35.

Tanzania Institute of Education. (2016). *Mwongozo wa Mwalimu kwa Shule za Msingi*. TIE, Dar es Salaam.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2005). *Mwongozo wa Maandalizi na Matumizi ya zana za kufundishia na kujifunza elimu ya awali na ya msingi Tanzania*.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2005). *Mwongozo wa Mwezeshaji Elimu ya Ualimu, Ufaraguzi wa Zana na Upimaji wa Elimu ya Awali na Msingi*.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2015). *Mtaala wa Elimu ya Msingi Darsa la I – VII*. Dar es Salaam Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2016). *Mwongozo wa Mwalimu wa Kufundishia Elimu ya Msingi*. Dar es Salaam Tanzania.

UNESCO. (2017). *Education for sustainable development goals: Learning objectives*. Author.

UNICEF. (2019). *Gender-responsive pedagogy: A teacher's handbook*.

White, K. E., & Smith, T. R. (2022). Exploring the impact of one-on-one counseling in educational settings. *Journal of Educational Psychology*, 114(3).



Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2020). *Mitaala ya Elimu ya Msingi na Sekondari: Muhtasari wa Upimaji na Tathmini*. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu.

Woolfolk, A. (2016). *Educational Psychology (13th ed.)*. Boston: Pearson.

World Health Organization. (2018). *Promoting health through schools: The WHO's global school health initiative*. World Health Organization.

WyEST .(2023). *Mtaala wa Elimu ya Awali*, Taasisi ya Elimu Tanzania

WyEST .(2023). *Muhtasari wa Somo la Mitaala na Ufundishaji Shahada ya Ualimu Elimu ya Msingi*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

WyEST. (2023). *Muhtasari wa Somo la Mitaala na Ufundishaji Shahada ya Ualimu Elimu ya Awali*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

WyEST. (2023). *Muhtasari wa Somo la Mitaala na Ufundishaji Shahada ya Ualimu Elimu Maalum*. Taasisi ya Elimu Tanzania.